**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

# RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**FEBRUARI, 2024**

**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

# RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**YALIYOMO**


1. UTANGULIZI ...- 6 -

1.1 UTARATIBU NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI ... - 7 -

1.2 MISWADA YA SHERIA NA TAARIFA ZA SERIKALI ... - 8 -

1.3 MUUNDO WA KAMATI ... - 8 -

1.4 HADIDU REJEA ... - 9 -

SEHEMU YA PILI ...- 10 -

2. MAUDHUI YA RIPOTI YA KAMATI ... - 10 -

2.1 OFISI YA RAIS – IKULU ... - 10 -

2.2 OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI ...- 12 -

2.3 OFISI YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA ... - 13 -

2.4 AFISI YA USALAMA WA SERIKALI (GSO) ... - 17 -

2.5 AFISI YA UFUATILIAJI NA USIMAMIZI WA UTENDAJI SERIKALINI (PDB) ZANZIBAR ... - 18 -

2.6 ZIARA KWA VIONGOZI WASTAAFU ... - 20 -

3. OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS ... - 21 -

4. OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI ...- 37 -

4.1 IDARA YA FARAGHA YA MAKAMU WA PILI WA RAIS ... - 37 -

4.2 KAMISHENI YA KUKABILIANA NA MAAFA ... - 38 -

4.3 IDARA YA SHEREHE NA MAADHIMISHO YA KITAIFA ...- 40 -

4.5 MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII KUPITIA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASIKINI (TASAF) ...- 43 -

4.6 BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR ... - 44 -

4.7 TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR ... - 46 -

5. OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA - 48 -

5.1 IDARA YA MIUNDO YA TAASISI, UTUMISHI NA MASLAHI YA WATUMISHI ...- 49 -

5.2 IDARA YA MIPANGO NA RASILIMALI WATU ... - 51 -

5.3 WAKALA WA SERIKALI MTANDAO ...- 51 -

5.4 KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA ... - 53 -

5.5 TUME YA UTUMISHI SERIKALINI ...- 54 -

**5.6 IDARA YA UTAWALA BORA** ....................- 56 -

**5.7 AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (CAG)** ....................- 56 -

**5.8 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR (ZAECA)**.................... - 59 -

**5.9 TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**.................... - 61 -

**5.10 IDARA YA URATIBU NA UENDESHAJI WA WIZARA**....................- 63 -

**5.11 OFISI KUU PEMBA**.................... - 63 -

**5.12 IDARA YA KATIBA NA MSAADA WA KISHERIA**....................- 64 -

**5.13 MAHAKAMA KUU** ....................- 65 -

**5.14 AFISI YA MWANASHERIA MKUU**.................... .- 68 -

**5.15 AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA**.................... - 70 -

**5.16 TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR** ....................- 72 -

**5.17 TAASISI YA SKULI YA SHERIA ZANZIBAR**....................- 74 -

**5.18 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA ZANZIBAR**.................... - 76 -

**5.19 OFISI YA MUFTI MKUU ZANZIBAR**.................... .- 78 -

**5.20 CHUO CHA UTAWALA WA UMMA (IPA)**.................... - 80 -

**6. OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ**.................... - 83 -

**6.1 JESHI LA KUJENGA UCHUMI *(JKU)* ZANZIBAR** ....................- 84 -

**6.2 WAKALA WA ULINZI WA JESHI LA KUJENGA UCHUMI**.................... - 88 -

**6.3 CHUO CHA MAFUNZO (MF) ZANZIBAR**.................... - 89 -

**6.4 KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)**.................... - 92 -

**6.5 KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU) ZANZIBAR** .................... - 94 -

**6.6 KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ)** ....................- 96 -

**6.7 OFISI YA MKOA WA MJINI MAGHARIBI** ....................- 98 -

**6.8 BARAZA LA JIJI LA ZANZIBAR**.................... - 99 -

**6.9 BARAZA LA MANISPAA MJINI** .................... - 100 -

**6.10 BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI "A"**.................... - 102 -

**6.11 BARAZA LA MANISPAA YA MAGHARIBI "B"**.................... - 103 -

**6.12 OFISI YA MKOA WA KUSINI UNGUJA**.................... - 105 -

**6.13 BARAZA LA MJI KATI** .................... - 106 -

**6.14 HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI UNGUJA** .................... - 107 -

**6.15 OFISI YA MKOA WA KASKAZINI UNGUJA................................ - 109 -**
**6.16 BARAZA LA MANISPAA KASKAZINI "A".................................... - 109 -**
**6.17 BARAZA LA MJI KASKAZINI "B".............................................. - 110 -**
**6.18 OFISI YA MKOA WA KUSINI PEMBA** ........................................................- 112 -
**6.19 BARAZA LA MANISPAA CHAKE CHAKE ................................... - 113 -**
**6.20 BARAZA LA MJI MKOANI – PEMBA.......................................... - 115 -**
**6.21 OFISI YA MKOA WA KASKAZINI PEMBA.................................. - 116 -**
**6.1 BARAZA LA MJI WETE................................................................ - 118 -**
**6.2 HALMASHAURI WILAYA YA MICHEWENI** .......................................................- 119 -
**6.3 WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR** ..............- 121 -
**6.4 AFISI YA MRAJISI WA JUMUIYA ZISIZO ZA KISERIKALI (NGO's)...** - 123 -
**7.0 MAONI , USHAURI NA MAPENDEKEZO YA JUMLA YA KAMATI.........** - 125 -
**8.0 HITIMISHO..........................................................................** - 133 -

## SEHEMU YA KWANZA

## 1. UTANGULIZI

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambayo imeundwa na kupewa majukumu kwa mujibu wa kifungu cha *85* cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka *1984* na Kanuni ya *107(1)* ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la mwaka *2020*.

Ripoti hii inaakisi kazi zote za Kamati ambazo zimefanywa kuhusiana na utekelezaji wa Taasisi ambazo zipo chini yake kwa kipindi cha mwaka wa fedha, 2023/2024 kwa kuzingatia Mipango mikuu ya Kitaifa ambayo inajumuisha Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 – 2025. Aidha, majukumu ya Kamati hii, yameelezwa katika *Jadweli la Kwanza* la Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar kama ifuatavyo:

(i) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.
(ii) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza.
(iii) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.
(iv) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.
(v) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.
(vi) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.
(vii) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.
(viii) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati hii ni ya Kisekta ambayo inasimamia utekelezaji wa majukumu ya wizara *Tano (5)* zifuatazo: -

*(a)* Ofisi ya Rais Ikulu;
*(b)* Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais;
*(c)* Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;
*(d)* Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora; na
*(e)* Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum.

## 1.1 UTARATIBU NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI

Sehemu hii inaelezea utaratibu uliotumiwa na Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika utekelezaji wa kazi zake ambazo zilifanywa kwa mujibu wa Kanuni ya 107(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la mwaka 2020. Shughuli hizo ni pamoja na:

(a) kupokea taarifa mbali mbali za kila robo mwaka (quarterly reports);
(b) kupokea taarifa za utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya kila Wizara;
(c) utekelezaji wa Maagizo ya Kamati;
(d) kukutana na wadau mbali mbali wa sekta zinazosimamiwa na Kamati;
(e) kukagua baadhi ya maeneo na miradi mbali mbali ya kimaendeleo inayosimamiwa na Wizara zinazohusika ili kuona hatua za utekelezaji zilizofikiwa, changamoto zilizopo na kutoa ushauri wa kutatua changamoto hizo; na
(f) kupitia Miswada mbali mbali ya sheria ambayo iliwasilishwa mbele ya Kamati katika kipindi chote hicho.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ilitekeleza kazi zake kwa kusimamia malengo yafuatayo:

*(a)* kufuatilia maagizo yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka *2022/2023*;
*(b)* kufuatilia ahadi za Serikali zilizotolewa katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka wa fedha *2023/2024*;
*(c)* kufuatilia utekelezaji wa Bajeti (kazi za kawaida na kazi za maendeleo) ya mwaka wa fedha *2023/2024*; na
*(d)* kufuatilia ukusanyaji wa mapato katika Taasisi za Serikali pamoja na kufanya ziara za ukaguzi katika Taasisi husika.

## 1.2 MISWADA YA SHERIA NA TAARIFA ZA SERIKALI

Miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati hii ni kushughulikia miswada ya sheria ambayo itahitaji kufanyiwa mapitio na kujadiliwa katika Baraza la Wawakilishi ili kuwa sheria kamili. Katika kipindi hiki, Kamati ilipitia Miswada ifuatayo:

*(a)* Mswada wa Kufuta Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar, Nam. 1 ya 2012;
*(b)* Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani Yake, Nam. 6 ya 2023;
*(c)* Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Nam. 11 ya 2003;
*(d)* Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahkama ya Kadhi, Nam. 9 ya 2017 na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo;
*(e)* Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar, Nam. 12 ya 2019;
*(f)* Ripoti ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kwa mwaka 2022/2023;
*(g)* Ripoti ya Tume ya Maadili kwa mwaka 2022/2023.
*(h)* Ripoti ya Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2022/2023.

## 1.3 MUUNDO WA KAMATI

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inaundwa na Wajumbe wafuatao:

| ***Nam.*** | ***Jina*** | ***Wadhifa*** |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Maryam Thani Juma | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Panya Ali Abdalla | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| *7.* | Mhe. Haji Shaaban Waziri | Mjumbe |
| *8.* | Suleiman Haroub Suleiman | Mjumbe |
| *9.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *10.* | Ndg.Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *11.* | Ndg. Shawana Mohammed Haji | Katibu |
| *12.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani wa Lugha za Alama. |

## 1.4 HADIDU REJEA

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika kutekeleza majukumu yake ilitumia:

*(a)* Katiba ya Zanzibar ya Mwaka *1984*;
*(b)* Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka *2020*;
*(c)* Ripoti ya Kamati ya Mwaka 2022/2023;
*(d)* Hotuba za Bajeti kwa Mwaka wa fedha *2022/*2023 na *2023/2024* za Wizara zifuatazo:

i. Ofisi ya Rais Ikulu,
ii. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais;
iii. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;
iv. Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora;
v. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ; na
vi. Taarifa za Utekelezaji wa bajeti za Wizara na Taasisi husika.

## SEHEMU YA PILI

## 2. MAUDHUI YA RIPOTI YA KAMATI

Sehemu hii inaelezea kwa kina mafanikio, changamoto na ushauri wa Kamati kwa kila taasisi ambayo ipo chini ya usimamizi wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kipindi cha mwaka 2023/2024. Taasisi hizo ni:

(a) Afisi ya Rais Ikulu.
(b) Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais;
(c) Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;
(d) Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora; na
(e) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ;

Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kipindi hiki imefanikiwa kutembelea na kukagua utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati kwa mwaka 2022/2023, kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, pamoja na kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila taasisi yenye kuhusika ukusanyaji wa mapato katika Ofisi hii kwa lengo la kuona utekelezaji wa malengo yaliyopangwa katika bajeti ya 2023/2024 yamefikiwa kwa kufuata sera za nchi na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Hivyo basi, kwa kutumia Kanuni ya 109 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la mwaka 2020 – 2025), Kamati imeweza kutembelea na kukagua utekelezaji wa bajeti na miradi ya maendeleo ili kufahamu mafanikio na changamoto za kila taasisi pamoja na kutoa maoni na ushauri kwa taasisi zifuatazo: -

### 2.1 OFISI YA RAIS – IKULU

Afisi ya Rais – Ikulu imeanzishwa kwa mujibu wa mamlaka aliyopewa Mheshimiwa Rais katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kifungu Namba 50(04). Afisi ya Rais Ikulu ni matokeo ya mabadiliko ya Miundo ya Wizara yaliyofanyika mara tu baada ya kuanza kwa Awamu ya Nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Afisi ya Rais Ikulu ina jukumu la kusimamia Afisi ya Faragha, Afisi ya Baraza la Mapinduzi (BLM), Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji, Idara ya Mawasiliano na Habari, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Shughuli za Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi, Afisi ya Usalama wa Serikali (GSO), Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu, Taasisi ya Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utendaji Serikalini (PDB) na Afisi ya Rais Ikulu - Pemba.

Katika utekelezaji wa kazi za kawaida na kazi za maendeleo, Kamati imefanikiwa kutembelea na kukagua shughuli mbali mbali ambazo zimepangwa kutekelezwa kwa kipindi hiki cha utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2023/2024.

**Afisi ya Rais Ikulu kupitia kitengo cha Faragha;** imeendelea kutekeleza kazi zake za kawaida pamoja na kushiriki kikamilifu katika kuratibu mapokezi ya wageni wanaomtembelea Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Sambamba na hilo, Mhe. Rais aliweza kufanya mazungumzo na wageni hao na kusisitiza juu ya umuhimu wa kuwepo kwa ushirikiano wa karibu na Mashirika ya kimaendeleo yanayosaidia kuziwezesha Taasisi za Serikali kutekeleza majukumu yake kitaalamu.

Kiujumla, Mhe. Rais, alitilia mkazo Sera Kuu ya Uchumi wa Zanzibar kuwa ni Uchumi wa Buluu na kuyataka mashirika hayo kuangalia fursa zaidi za kuunga mkono Sekta ya Utalii kwa lengo la kukuza uchumi na kuleta maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar.

Kwa upande wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano, Afisi imeendelea kushirikiana kikamilifu na wadau wa habari na mitandao ya kijamii binafsi wa ndani na nje ya nchi kwa kurusha na kusambaza kwa wakati na uhakika taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Vile vile, Kamati imeridhishwa na utendaji wa Mfumo wa Sema na Rais Mwinyi (SNR) ambao ulitengenezwa kwa lengo la kuwapa fursa wananchi kuwasilisha changamoto au maoni kupitia taasisi za umma, kuzifuatilia na kuzipatia ufumbuzi. Aidha, Kamati inaipongeza taasisi hii kwa kufanikiwa kutoa mafunzo ya namna nzuri ya kuwasilisha malalamiko ya wananchi kwa masheha wa Wilaya zote 11 za Unguja na Pemba.

**Idara ya Ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi:**

Kamati inatoa pongezi kwa Idara hii kwa kuendelea kutoa elimu kuhusiana na dhana ya diaspora na umuhimu wa ushiriki wao katika ajenda za maendeleo ya Zanzibar kupitia biashara, utalii, uwekezaji pamoja na misaada mbali mbali wanayoitoa kwa jamii. Sambamba na hilo, Idara imefanikiwa kufanya kikao na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kuhusu utaratibu na uendeshaji wa utoaji wa tuzo za diaspora, kikao hiki kilifanyika Jijini Dar es Salaam, mwaka 2023.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanikiwa kukamilisha kanuni za usajili wa wanadiaspora wa Zanzibar na kuweza kutiwa Saini na Mheshimiwa Waziri. Kanuni hizo zitatumika rasmi maraa baada ya kukamilika kwa mfumo wake ambao utakabidhiwa kwenye Idara Mwezi Februari, 2024.

Kamati inawapongeza kwa kuendelea kuratibu shughuli zake za kila siku zikiwemo kuwasajili wanadiaspora wanaofika ofisini ambapo mpaka sasa wanadiaspora 20 kutoka nchi za; Uiengereza, Oman, Kenya, Dutch, Falme za kiarabu, Ukraine na Denmark wamefanikiwa kusajiliwa.

Kupitia programu ya utawala na uendeshaji, ofisi imefanikiwa kutoa ushauri wa kisheria na maarifa (Legal Opinion) kwa Mhe. Rais na Serikali kwa ujumla kuhusiana na mambo mbali mbali yanayohusu Serikali Kuu. Ushauri huu wa kisheria umekuwa chachu muhimu katika kumuwezesha Mhe. Rais na Serikali kuchukua maamuzi sahihi na kufuata taratibu stahiki. Hii imeimarisha utawala bora na kuhakikisha Serikali inafanya maamuzi kwa kuzingatia misingi ya kisheria, haki na uwajibikaji.

## 2.2 OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI

Ofisi ya Baraza la Mapinduzi (BLM) limeundwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Kifungu cha 43 (1) cha Katiba kinaeleza kuwa "kutakuwa na Baraza la Mapinduzi ambalo litajumuisha Rais, Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais, Mawaziri pamoja na Wajumbe wengine kama atakavyoona inafaa.

BLM ina jukumu la kuratibu mambo yanayohusu Baraza la Mapinduzi pamoja na Kamati zake ikiwepo Kamati ya Makatibu Wakuu *(Inter Ministerial Technical Committee - IMTC)*.

Kamati inaipongeza Ofisi ya BLM kwa namna ilivyopata mafanikio makubwa kama vile kuiwezesha Sekretarieti ya Baraza la Mapinduzi kutekeleza jukumu la kuchambua nyaraka za Taarifa kabla ya kuwasilisha katika vikao vya Kamati ya Makatibu Wakuu na baadae katika Baraza la Mapinduzi.Lengo kuu la uratibu ni kuzifanya nyaraka ziwe taarifa zinazojitosheleza na za uhakika ili kuiwezesha Serikali kufanya uamuzi unaozingatia ushahidi (evidence – based decision).

Baraza la Mapinduzi linakabiliwa na changamoto ya upatikanaji mdogo wa fedha za matumizi ya ofisi (OC) na kuchelewa kupatikana fedha hizo zinazopelekea ofisi kushindwa kutimiza mahitaji yake kwa muda maalum.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inasikitishwa na Afisi kulazimika kukopa kwa baadhi ya wasambazaji wa huduma ili kuweza kukamilisha kazi husika, hivyo inashauri kwa Serikali kuiangalia Afisi hii na umuhimu wa kazi zake kwa kuwaingizia fedha za matumizi mengineyo kwa kadri watavyohitaji.

## 2.3 OFISI YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA

Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa Zanzibar imeundwa na kufanya kazi chini ya Sheria Nam. 3 ya Mwaka 2008 kwa madhumuni ya msingi ya kutunza na kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu kama urithi wa Taifa. Vile vile, kusimamia na kutoa miongozo juu ya namna bora ya utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka zote zinazozalishwa na kuhifadhiwa katika wizara, taasisi na mashirika ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na taasisi zote za Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mafanikio ya Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa:

*(i)* Taasisi ya Nyaraka imefanikiwa kufanya ukaguzi wa kumbukumbu na nyaraka kwa Wizara, Idara na Taasisi za Umma na kutoa ushauri juu ya namna bora ya uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka.
*(ii)* Taasisi imefanikiwa kutoa huduma na ushauri wa uhaulishaji wa kiutafiti kwa watafiti ambao wamepatiwa taarifa za skuli na taarifa za mirathi.
*(iii)* Taasisi imeratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za kila siku zilizopangwa kwa kuwapatia watumishi mahitaji na vitendea kazi.
*(iv)* Taasisi imefanikiwa kuhifadhi majalada kwa njia ya kielektroniki (kuhaulisha) ili yaweze kutumika kwa njia ya kimtandao.

(v) Kujenga uelewa kwa wasimamizi na watendaji wa kumbukumbu na nyaraka kwa Wizara, Idara na Taasisi zote za SMZ na SMT kwa ofisi za Zanzibar.
(vi) Kupunguza mrundikano wa majalada kwa baadhi ya taasisi zilizokaguliwa pamoja na kutoa miongozo inayohusiana na usimamizi na uendeshaji wa masjala.
(vii) Kuimarika kwa baadhi ya huduma na miundo mbinu ya ofisi ambapo imepelekea kuongeza idadi ya watafiti kutoka nchi za nje, taasisi za umma na jamii kuanza kupata uelewa wa kuitambua Taasisi na huduma zinazopatikana.

**ZIARA KWA IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA YA TAIFA, KANDA YA MASHARIKI JIJINI DAR ES SALAAM**

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imefanya ziara kwa Ofisi ya Rais, Idara ya kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Kanda ya Mashariki Jijini Dar es Salaam, kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu wa namna ya kutunza na kuhifahi nyaraka na kumbukumbu za Taifa.

Kufuatia ziara hiyo, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa umma na Utawala Bora Mhe. Ridhwan Kikwete ameahidi kamati kuwa Idara ya kumbukumbu na Nyaraka ya Taifa itatoa ushirikiano wa kutosha kwa Idara ya Nyaraka Zanzibar kwa kuzitambua, kuzikusanya, kuzihifadhi na kuzitunza kumbukumbu na nyaraka za waasisi na Viongozi Wakuu wa Zanzibar kwa maslahi mapana ya Taifa.

Aidha, ameitaka Idara ya kumbukumbu na Nyaraka Zanzibar kuhakikisha inaweka mikakati madhubuti ya kuhamasisha na kuuelewesha umma juu ya ofisi hizi ili kuzipa thamani inayoendana na kazi wanazozifanya. Sambamba na hilo, kamati imeridhika kufanya kazi kwa mashirikiano kwa ofisi hizi mbili na kuhakikisha zinaboreshwa kwa maslahi mapana ya pande zote mbili za Muungano.

**Changamoto za Taasisi ya Nyaraka Zanzibar**

Licha mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hiki, taasisi inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(a) Kamati imegundua uwepo wa mgongano wa kifikra baina ya idara ya kumbukumbu na baadhi ya Taasisi za Serikali zilizopewa miongozo na

mafunzo muhimu ya utunzaji kumbukumbu na nyaraka kwa kutozingatia vyema miongozo waliyopewa na idara hii kivitendo, jambo ambalo hupelekea upotevu na uharibifu wa kumbukumbu wa nyaraka muhimu.

*(b)* Kamati imebaini ufinyu wa Ofisi kwa watendaji na sehemu ya kuhifadhia nyaraka zinazokusanywa na zilizopo;

*(c)* Kamati inasikitishwa na kuona tatizo la ukosefu wa mfumo bora wa upatikanaji hewa katika chumba cha kuhifadhia nyaraka (strong room).

*(d)* Kamati imebaini taasisi ya nyaraka ina tatizo la kukosekana kwa Kitengo cha uhuishaji Nyaraka (Conservation Unit);

*(e)* Kamati wakati ikitembelea taasisi ya nyaraka imebaini kukosekana kwa Camera za Ulinzi (CCTV) katika afisi ya Pemba.

*(f)* Kamati imebaini taasisi ya nyaraka inakabiliwa na ufinyu wa upatikanaji wa Mgao wa Fedha ya Matumizi ya kawaida (OC).

*(g)* Kamati inasikitishwa na kuona ofisi inakabiliwa na tatizo la uhaba wa vifaa, maeneo na mazingira yasiyofaa kwa uhifadhi wa kumbukumbu kwa taasisi za Serikali zilizokaguliwa.

*(h)* Kamati imebaini tatizo la kutopewa kipaumbele kwa ripoti za ukaguzi zinazowasilishwa kwa wakuu wa taasisi za Serikali.

*(i)* Kamati imebaini taasisi inakabiliwa na ukosefu wa gari maalumu la kusafirisha nyaraka.

*(j)* Kamati inasikitishwa na kitendo cha baadhi ya taasisi zinazopoteza nyaraka muhimu za Serikali na za wafanyakazi hali ambayo inapelekea watendaji kukosa stahiki zao.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Taasisi ya Nyaraka Zanzibar**

*(i)* Kamati inatoa pongezi kwa Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu kwa uwekaji wa CCTV Camera. Kiukweli, jambo hili limeongeza nguvu zaidi za kiusalama ikiwa ni pamoja na kuhuisha mifumo ya utunzaji kumbukumbu katika ofisi. Hii ni dhahiri kwamba azma ya Serikali kuhusu mfumo wa usimamizi nyaraka inafikiwa kwa muda mchache.

Hata hivyo, Kamati inashauri mfumo kama huo kufungwa katika ofisi ya Pemba.

*(ii)* Kamati inaipongeza Taasisi ya nyaraka kwa jitihada zao za utunzaji wa nyaraka na uhifadhi wa kumbukumbu ulio bora na imara ambao utasaidia kutunza kwa muda mrefu na kwa vizazi vijavyo.

*(iii)* Kamati inaishauri idara hii kuendelea kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa viongozi, wakuu na watendaji wa wizara, idara, taasisi na mashirika mbali mbali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na taasisi za Muungano kwa ofisi zao zilizopo Zanzibar kwa lengo la kuhamasisha zoezi la uhamishaji wa taarifa zenye thamani katika Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu, jambo ambalo litasaidia sana kuratibu na kutunza kumbukumbu za taifa kwa ajili ya kizazi cha sasa na urithi wa baadae.

*(iv)* Kamati inashauri elimu iendelee kutolewa kwa Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali kwa ngazi zote za uongozi. Lengo ni kuwa na mfumo bora wa usimamizi wa nyaraka na kumbukumbu pamoja na kutoa huduma bora kwa Serikali kwa nia ya kuendeleza urithi wa kihistoria wa Zanzibar.

*(v)* Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho Sheria Nam. 3 ya Mwaka 2008 ili kuipa nguvu idara kufanya kazi kwa ufasaha, kuimarisha huduma ya miundombinu ya ofisi pamoja na kutoa miongozo inayohusiana na usimamizi na uendeshaji wa masjala kwa jumla.

*(vi)* Kamati inaipongeza taasisi kwa kuweka mfumo madhubuti wa kudhibiti upotevu wa nyaraka kwa kisingizio cha kufanya utafiti kwa watu wanaoingia na kutoka ofisini.

*(vii)* Kamati inaishauri Serikali na taasisi zake kwa ujumla kutoleta ugumu wakati watendaji wa nyaraka wanapokwendwa kuzifata kumbukumbu zinazohitajika.

*(viii)* Kamati inaishauri Serikali kusimamia maslahi ya watumishi wa Taasisi kulingana na ugumu wa kazi wanazozifanya.

*(ix)* Kamati haifurahishwi kuona bado kuna migongano ya taasisi mbali mbali katika kuhifadhi kumbukumbu kama vile taasisi ya Utumishi na

Msajili wa Hazina kutaka kuendelea kubaki na kumbukumbu hizo badala ya taasisi ya nyaraka.

*(x)* Kamati inashauri Serikali kuendeleza mpango wa ujenzi wa jengo jipya kwa haraka iwezekanavyo katika eneo la Kilimani baada ya kukamilika kwa taratibu za malipo ya nyumba za karibu na eneo la ofisi hiyo.

## 2.4 AFISI YA USALAMA WA SERIKALI (GSO)

Afisi ya Usalama wa Serikali inafanya kazi chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011, kifungu 78 (1-5) na Utaratibu wa Utendaji kazi wa GSO wa mwaka 1994 uliotolewa na Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

Aidha, Afisi hii ina jukumu la Kufanya Upekuzi wa Kiusalama, kufanya ukaguzi wa majengo ya makaazi ya Viongozi Wakuu wa Serikali, majengo ya Afisi za Serikali na miundombinu ya Serikali, kutoa Mafunzo ya kiusalama yanayohusu utunzaji wa siri na nyaraka za Serikali ikiwemo na kusimamia kiapo cha utunzaji wa siri katika Wizara, Idara, Mashirika ya Serikali ili kuwafanya watumishi wote wa Serikali na Mashirika yake kuwa na mwamko na uelewa wa majukumu yao ya kiusalama.

Afisi ya Usalama wa Serikali Zanzibar imefanikiwa kufanya yafuatayo:

*(i)* Imeelezwa kwamba Ofisi ya Usalama ya Serikali imefanya upekuzi wa watumishi kutoka Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali.

*(ii)* Ofisi pia, imefanya ukaguzi wa kiusalama wa majengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

*(iii)* Sambamba na hilo, ofisi imefanya semina tano (5) kwa watumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**Changamoto za Afisi ya Usalama wa Serikali (GSO) Zanzibar**

Mbali ya uwepo wa mafanikio tajwa Afisi ya GSO inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

*(i)* Kamati imebaini uchache wa fedha za matumizi ya kawaida (OC) hali inayopelekea kuchelewa kwa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa hasa kwa maeneo yalioko nje ya Zanzibar.

*(ii)* Kamati imebaini ukosefu wa uwezo wa kutosha kwa maafisa wa Ofisi ya Usalama wa Serikali.

*(iii)*Kamati imeelezwa kwamba kuna tatizo la kukosekana kwa mrejesho wa mapendekezo yanayotolewa na Afisi ya Usalama wa Serikali baada ukaguzi wa kiusalama wa majengo.

*(iv)* Kamati imebaini baadhi ya taasisi hazitekelezi kwa vitendo miongozo na mafunzo ya Utunzaji na Udhibiti wa Siri za Serikali yanayotolewa na GSO katika utendaji wao wa kazi wa kila siku.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Afisi ya Usalama wa Serikali (GSO) Zanzibar**

*(a)* Kamati inaishauri Serikali kuliangalia upya tatizo la OC ambalo limepitishwa katika Bajet Kuu ya Serikali kwa kuwapatia ofisi hii kama walivyokubaliwa na kwa wakati uliokusudiwa ili kazi za maendeleo ya ofisi hii ziweze kutekelezwa kwa urahisi.

*(b)* Kamati inaishauri Afisi hii kuwajengea uwezo maafisa wake kwa kuwapatia fursa za mijadala ya ndani ya kubadilishana uzoefu katika kazi za ukaguzi na utoaji wa mafunzo na vikwazo wanavyovipata katika kazi zao.

*(c)* Kamati pia, inashauri Afisi kuendelea na kazi ya kufanya ukaguzi katika majengo ya umma na yale ya kibishara hasa yenye muonekano wa kizamani kwa lengo la kuiweka nchi yetu katika hali ya kiusalama;

*(d)* Kamati imesikitishwa kuona zipo baadhi ya taasisi ambazo hazitekelezi kwa vitendo Miongozo na mafunzo ya Utunzaji na Udhibiti wa Siri za Serikali yanayotolewa na GSO katika utendaji wao wa kazi wa kila siku. Hivyo, Kamati inazitaka taasisi husika kuwachukulia hatua watumishi wote wanaokaidi miongozo hiyo kwa vitendo.

## 2.5 AFISI YA UFUATILIAJI NA USIMAMIZI WA UTENDAJI SERIKALINI (PDB) ZANZIBAR

Taasisi ya Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utendaaji Serikalini (PDB) Zanzibar imeundwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa lengo la kufanya ufuatiliaji na usimamizi utendaji kazi Serikalini ili kukidhi haja ya kuimarisha uwezo wa Serikali katika kufanikisha dira ya

mabadiliko na maendeleo endelevu ya visiwa vya Zanzibar, Pamoja na kuharakisha vipaumbele vya kimkakati vya Serikali na kutoa matokeo ya athari za mabadiliko ya kijamii na kiuchumi nchini.

Taasisi hii imekuwa ni chachu katika kuleta ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya kimkakati Zanzibar yenye wajibu wa kuhakikisha kwamba huduma na kazi za Serikali zinatolewa kwa wakati na kwa kiwango kilicho bora ili kuweka mazingira mazuri na ufanisi wa kiutendaji katika Sekta za Serikali kwa lengo kuimarisha utoaji huduma kwa umma.

Sambamba na hilo, Taasisi imekuwa ikishirikiana na Wizara na Taasisi za Serikali za pande zote mbili za Muungano, Serikali ya SMZ na Serikali ya SJMT.

**Mafanikio ya Ofisi ya PDB**

Imeelezwa kwamba katika kutekeleza majukumu ya taasisi kimkakati Taasisi imefanikiwa kushiriki katika mafunzo ya ufuatiliaji na tathmini yaliyoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa lengo la kujifunza nyenzo za ufuatiliaji wa Miradi ya Serikali ili iweze kutoa matokeo chanya.

Aidha, Taasisi imefanikiwa kuandaa ripoti ya utekelezaji ikiwemo ya "Stock take" ambayo inaelezea utekelezaji wa kazi za PDB tangu kuanzishwa kwa ofisi hiyo.

**Changamoto za Ofisi ya PDB**

Kama ilivyo kilio cha taasisi nyingi kwenye Wizara na taasisi za Serikali Ofisi hii pia inakabiliwa na uhaba wa fedha za matumizi mengineyo hali inayorudisha nyuma ufuatiliaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

**Maoni, ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

*(i)* Kwa dhati kabisa Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kubuni namna bora ya ufuatiliaji wa ahadi za miradi anayoitoa kwa kuunda Ofisi hii mapema Disemba 2022. Imani yetu kwake ni kuendeleza Zanzibar iliyobora kwa mustakbali mzuri wa wananchi wake.

*(ii)* Kamati inashauri kuwapatia fedha za matumizi mengineyo za kutosha ili kuimarisha uwezo wa utoaji huduma Serikalini katika utekelezaji wa ahadi za Rais ili kuleta mabadiliko na maendeleo Serikalini. Fedha hizo zitasaidia kuharakisha utekelezaji wa miradi ambayo inasuasua, kupanga mikakati ya utekelezaji kwa wakati na viwango bora, kusimamia vipaumbele vya Mhe. Rais, ili viweze kutekelezeka kwa wakati na kwa viwango.

*(iii)* Kamati inashauri katika ufuatiliaji wa miradi hii ya kimkakati kuwekwa vipaumbele kwa miradi ambayo itachangia mabadiliko na matokeo yanayoonekana ikiwa ni pamoja na uundwaji wa timu imara ya wataalamu wa ndani na kuweka mazingatio katika miradi ya miundombinu kama maji, barabara kwa ufanisi mkubwa ili lengo la Mhe. Rais liweze kufikiwa.

*(iv)* Kamati inaipongeza taasisi hii kwa kuendelea kuratibu na kuharakisha utekelezaji wa vipaumbele hivi pamoja na kuibua changamoto zinazozikabili wizara na taasisi mbali mbali kwa kutoa mapendekezo kwa ajili ya utekelezaji wa vipaumbele hivyo ikiwa na lengo la kutoa mafunzo, miongozo itakayosaidia kutekeleza majukumu ya taasisi. Hata hivyo, kamati inaishauri Taasisi ya PDB kufuatilia kwa karibu uwajibikaji wa watendaji wa Serikali.

*(v)* Kamati pia inaipongeza Taasisi hii kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali pamoja na Wizara ya Uwezeshaji kwa lengo la kupata takwimu sahihi ya walengwa wa miradi na kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa ipasavyo. Hata hivyo, Kamati inazidi kushauri kuendeleza ushirikiano huo ili changamoto ndogo ndogo zisiweze kujitokeza wakati wa kufanya tathmini ya miradi.

## 2.6 ZIARA KWA VIONGOZI WASTAAFU

Kamati imefanya ziara kwa viongozi wastaafu mbali mbali wa nchi, kwa lengo la kufahamu changamoto zao na kutafuta namna bora ya kuzipatia suluhisho, kujifunza masuala ya ukuzaji diplomasia ya nchi pamoja na kupata uzoefu wao kwenye masuala ya uongozi. Katika kuendelea kuwaenzi viongozi wetu, kamati imejiwekea utaratibu wa kuwatembelea wastaafu hao mara kwa mara kwa kuwa inatambua michango yao mikubwa katika kuitumikia nchi kwa vipindi vyote vya utumishi wao wa umma. Kwa mantiki hiyo, kamati inaishauri Serikali kuifanyia marekebisho Sheria ya Maslahi ya Viongozi Wakuu wa kitaifa ili kuendelea kuyatetea, kuyasimamia na kuyalinda maslahi yao.

Viongozi waliotembelewa ni pamoja na :

*(i)* Mhe. Rais Mstaafu wa Awamu ya Sita Dkt. Amani Abeid Karume, Kamati ilipokea ushauri wa kuendelea kuratibu mahusiano ya kimataifa kupitia sheria na mikataba ya kitaifa kwa maslahi ya nchi na kuiweka katika hali ya usalama, amani, maendeleo ya jamii na ya uchumi, haki za binaadamu, ushiriki wa watu wenye

ulemavu, uhuru na demokrasia ili Azma ya Serikali ya kuendeleza uhusiano wa kirafiki kati ya mataifa liweze kufikiwa.

*(ii)* Mhe. Rais Mstaafu wa Awamu ya Saba Dkt. Ali Mohamed Shein na kupokea busara na hekima kutoka kwa mstaafu wetu na kuusia kuendelea kulinda ustawi wa maendeleo kwa wananchi ikiwa ni pamoja kudumisha mazuri ya awamu zilizopita, kuyaendeleza mema yaliyopo na kuleta mengine mapya ili kukuza ufanisi na tija tukiongozwa na Dira ya Taifa na Ilani ya Uchaguzi wa wa Chama cha Mapinduzi.

*(iii)* Vile vile, Kamati imefanikiwa kufanya ziara kwa Mhe. Makamu wa Pili Mstaafu Balozi Seif Ali Iddi na kupokea busara na maneno ya hekima kutoka kwa kiongozi huyo. Mheshimiwa Balozi, ameiambia kamati kuwa uongozi ni dhamana, hivyo uwajibikaji, uzalendo, uaminifu na usimamizi wa kazi vinatakiwa kuwepo katika kiwango cha hali ya juu katika kufanya maamuzi yoyote ili kutoathiri utendaji kazi. Aidha, amesisitiza kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekua na imani ya kutupa dhamana, hivyo ni wajibu wetu kusimamia maslahi ya wananchi na kutekeleza ipasavyo. Sambamba na hilo, Mheshimiwa Balozi ametuusia kwamba hekima, busara, diplomasia na demokrasia zina matokeo chanya wakati wote wa kuongoza watu.

## 3. OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inashughulika na masuala mtambuka ya uhifadhi, usimamizi na utunzaji wa mazingira, masuala ya watu wenye ulemavu, masuala ya VVU na UKIMWI na masuala yanayohusu udhibiti wa dawa za kulevya. Aidha, Ofisi hii inasimamia na kuratibu Ofisi ya faragha ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na masuala ya Sera, Mipango na Tafiti za Ofisi.

Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inaundwa na Idara zifuatazo:

*i.* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
*ii.* Idara ya Utumishi na Uendeshaji.
*iii.* Idara ya Mazingira.
*iv.* Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar.

*v.* Mamlaka ya Kudhibiti na Kupamba na Dawa za Kulevya.
*vi.* Tume ya Ukimwi.
*vii.* Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu.
*viii.* Ofisi ya Faragha ya Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais.
*ix.* Ofisi Kuu Pemba.

## 3.1 IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

Idara hii imekua ikishughulika na kutoa huduma mbalimbali za utawala na uendeshaji, vitendea kazi, uratibu wa vikao na kugharamia safari za kikazi pamoja na matengenezo ya Ofisi na vyombo vya usafiri. Kamati inaipongeza idara hii kwa kuweza kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu watumishi wao.

Aidha kwa upande wa Ofisi ya Faragha, Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu ya Ofisi hii yakiwemo kuratibu na kusimamia upatikanaji wa huduma bora za ofisini na nyumbani kwa Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais, kutekeleza maagizo mbali mbali yaliyotolewa kupitia hotuba na mikutano, kufuatilia kero zilizowasilishwa na wananchi na kuzipatia ufumbuzi.

Sambamba na hilo, katika kukuza mashirikiano ambayo yamekuwa ni chachu ya maendeleo ya nchi, ofisi imeendelea kupokea wageni mbali mbali kutoka ndani na nje ya nchi. Kwa mwaka 2023/2024 Kamati inaipongeza Ofisi hii kwa kuweza kutekeleza vyema majukumu ya Ofisi.

Pamoja na hayo, Idara imeweza kutekeleza kazi mbali mbali zikiwemo:

*(i)* kuwapatia stahiki zao watumishi 20 (13 wanaume na 7 wanawake) ikiwemo stahiki za mishahara, malipo ya baada ya saa za kazi (watumishi 13), stahiki za likizo (watumishi 6) na stahiki ya ubani mtumishi mmoja.

*(ii)* Kuwawezesha watumishi watatu kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika ngazi ya Shahada ya Uzamili mtumishi mmoja, Shahada ya kwanza watumishi wawili na watumishi watatu (3) wamelipiwa mafunzo ya muda mfupi mmoja katika fani ya uongozi ambayo yalifanyika kibaha na wawili mafunzo ya awali (induction course).

*(iii)* Huduma mbali mbali za utawala zimetolewa zikiwemo ununuzi wa samani, vifaa vya kuandikia, vifaa vya gari, malipo ya umeme, mafuta na usafi. Ofisi imeendelea na matengenenzo ya lifti ambayo imefikia hatua ya asilimia 80.

*(iv)* Idara ilishiriki mafunzo ya siku moja kuhusu Utayarishaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu kwa mwaka 2024/2025

## 3.2 IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI

Kupitia programu ndogo ya uratibu wa Mipango Sera na Utafiti, imeelezwa Ofisi imekamilisha uandaaji wa programu ya urithi wa Zanzibar ya Kijani (Green legacy Initiative Program) ambayo tayari imepata ridhaa ya Serikali kuanza utekelezaji wake na inatarajia kuzinduliwa rasmi mwezi Machi 2024.

Aidha, katika kuratibu na kusimamia mapitio ya Sheria na Sera za Wizara Idara imekamilisha uwaandaji wa Sera ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya mwaka 2023 na kwa sasa ipo katika Ofisi ya Wakala wa Uchapaji wa Serikali kwa ajili ya kuchapishwa. Pamoja na hayo, Idara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti na kupambana na Dawa za Kuelvya, kupitia timu maalumu ya marekebisho ya Sheria ya Wizara imekamilisha marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Nam. 8 ya 2021. Sambamba na kukamilisha Kanuni za Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya 2023 na Kanuni za Watu Wenye Ulemavu za mwaka 2023 zimetayarishwa na zinasubiri kutangazwa rasmi.

Idara pia, imefanikiwa kufanya ziara za ufuatiliaji kwa miradi inayosimamiwa na Ofisi Unguja na Pemba kwa lengo la kuona hatua za utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na kukusanya taarifa zilizosaidia katika maandalizi ya Makala ya Maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi. Miongoni mwa miradi hiyo ni; Miradi wa Kuimarisha Jamii kwa Kuzingatia Ikolojia na shughuli za kujipatia kipato kwa wavuvi wadogo na usimamizi wa eneo la hifadhi la Mkondo wa Pemba, (UNEP) shughuli za mradi zilizopangwa kufanyika zimefikia asilimia 97, Mradi wa uhimili wa mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mfumo wa ikolojia vijijini (UNEP) ambapo umefikia asilimia 98 na Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia ambapo utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 96.

## 3.3 OFISI KUU PEMBA

Kwa mwaka huu Ofisi Kuu Pemba iliweza kutekeleza mambo mbali mbali yakiwemo: Kuwapatia stahiki zao watumishi 49 (28 wanaume na 21 wanawake) ikiwemo stahiki za mishahara, malipo ya baada ya saa za kazi (watumishi wawili) na stahiki zao za likizo (watumishi watatu). Aidha, Kuendelea kuwalipia watumishi watatu wanaoendelea na mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya shahada ya uzamili watumishi wawili shahada ya kwanza na mtumishi mmoja stashahada na mtumishi mmoja astashahada na Huduma mbali mbali za utawala zimetolewa zikiwemo ununuzi vifaa vya kuandikia, vifaa vya gari, malipo ya umeme, mafuta na usafi.

Ofisi imefanikiwa kuratibu ziara tatu ya Mheshimiwa Makamu wa kwanza wa Rais wa Zanzibar ikiwemo Ufunguzi wa Siku ya Chakula Duniani, kushiriki katika ugawaji wa Vifaa vya Uvuvi wa madagaa katika shehia ya Wesha na ziara ya kuwatembelea watu waliopata mafunzo ya kuogelea kwa ajili ya upandaji wa mwani katika kima kirefu huko Kilindi, kushiriki katika maonesho ya siku ya chakula Duniani.

## 3.4 MAMLAKA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ZANZIBAR (ZEMA)

Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA) imeanzishwa mwaka 2015 chini ya Kifungu cha 14 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar. Lengo Kuu la Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar ni kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria, kanuni, miongozo na viwango vya mazingira kwa ajili ya kupunguza uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

Aidha, Mamlaka ya ZEMA inasimamiwa na Bodi iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, 2015. ZEMA imepangiwa majukumu yake kwa mujibu wa kifungu cha 22(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, 2015.

Mamlaka imefanikiwa kufanya operesheni kadhaa za kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki kwa ajili ya kuondoa athari za kimazingira na kiafya zinazotokana na mifuko hiyo kwa Unguja na Pemba.

Mamlaka imeweza kufanya operesheni za kusimamia maliasili zisizorejesheka kwa lengo la kudhibiti uharibifu wa mazingira unaotokana

na uchimbaji na uchukuaji holela kwa kuwapa elimu ya namna gani ya kudhibiti uharibifu wa kimazingira.

Mamlaka pia imeweza kufanya ziara za ufuatiliaji wa maeneo ya kimazingira kwa ajili ya kupunguza uharibifu na uchafuzi wa mazingira kwenye jamii.

Aidha, kamati imeridhishwa na usimamizi wa Mazingira (ZEMA) uliowezesha kudhibiti uharibifu wa mazingira unaotokana na uchimbaji na uchukuaji holela wa maliasili zisizorejesheka.

Kamati wakati ikipokea taarifa zake za utekelezaji ilielezwa kwamba Ofisi imekuwa ikiendelea kuelimisha jamii juu ya uhifadhi na usimamizi bora wa mazingira kwa ujumla wake, kupitia vipindi vya redio, Tv na Mitandao ya kijamii ambapo imefanikiwa kurusha kipindi kilichozungumzia mazingira na maafa.

**Changamoto za Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA)**

*(a)* Kamati imebaini kuwa Mamlaka imeshindwa kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato hadi tunapokea taarifa hii kutokana na kuharibika kwa gari zote mbili.

*(b)* Kamati imebaini kuwa Ofisi inakabiliwa na ukosefu wa jengo la kudumu kwa watendaji wa ZEMA.

*(c)* Kamati imebaini kwamba Ofisi ina upungufu wa baadhi ya vifaa na vitendea kazi.

*(d)* Kamati imeelezwa tatizo la uchimbaji holela wa Mchanga na mali asili nyengine zisizorejesheka katika maeneo mbali mbali.

*(e)* Kamati imebaini upungufu wa wataalamu katika fani maalumu za kimazingira hasa mafuta, gesi na uhandisi.

*(f)* Kamati inaamini tatizo la uelewa mdogo wa jamii, taasisi za Umma na Binafsi katika uhifadhi wa mazingira jambo ambalo linapelekea kutokea kwa uharibifu mkubwa wa mazingira.

*(g)* Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kubwa ya usimamizi duni wa taka katika miji ya Zanzibar.

**Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati:**

*(i)* Kamati inaishauri Serikali kutafuta namna ya kuwapatia gari mpya mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira kwa bajeti ya mwaka 2024/2025.

*(ii)* Kamati inashauri Serikali kuwapatia fedha mamlaka kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya ambalo litaondosha tatizo la nafasi katika jengo.

*(iii)* Kamati inapendekeza kwa Serikali kuanzishwa kwa kitengo cha mazingira katika jeshi la polisi, mawakili wa Serikali wa mazingira na hakimu wa kimazingira ili kutatua migogoro na kesi za kimazingira.

*(iv)* Kamati inapendekeza Wizara kuwapatia Mamlaka fedha za matumizi mengineyo ya kutosha ili iweze kujinunulia nyenzo na vitendea kazi vya Ofisi ili kurahisisha utendaji kazi wa Mamlaka.

*(v)* Kamati inaishauri Serikali kuendeleza operesheni na ufatiliaji wa kimazingira ili kuweza kuchukuwa hatua za kisheria na kimazingira na uendelezaji wa mashimo yaliyochimbwa.

*(vi)* Kamati inaiomba Serikali kujengea uwezo wa kitaasisi juu ya kusimamia ipasavyo masuala ya uchimbaji mafuta na gesi kimazingira.

*(vii)* Kamati inaitaka Serikali kujenga uwezo wa maafisa wa ZEMA na ushirikiano wa taasisi nyengine ili kuleta ufanisi wa utendaji kazi.

## 3.5 IDARA YA MAZINGIRA

Idara ya Mazingira ni taasisi ya Usimamizi wa Mazingira yenye jukumu la kuandaa nyenzo za usimamizi wa Mazingira, kuratibu masuala ya mabadiliko ya Tabianchi ikiwa ni pamoja na shughuli za kuhimili mabadiliko hayo. Aidha Idara hii kwa mujibu wa kifungu cha Sheria Namba 13 cha cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2015 idara inaratibu utekelezaji wa Sera, mikakati na miongozo ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mazingira.

Idara ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi kupitia Mradi wa Kuimarisha Jamii kwa kuzingatia Ikolojia na shughuli za kujipatia kipato kwa wavuvi wadogo na usimamizi endelevu wa eneo la hifadhi ya mkondo wa Pemba (PECCA) (SAPPHIRE PROJECT).

Idara imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

*(i)* Kutekeleza miradi yenye lengo la kuongeza uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabiachi katika jamii za vijijini kwa kuimarisha mifumo ya ikolojia na kuwezesha njia mbadala za kujiongezea kipato nchini.

*(ii)* Kujenga vituo vya wajasiriamali wa vipodozi, ushoni na ufugaji katika shehia za miradi.

*(iii)* Kutolewa kwa elimu za vitendo juu ya maswala ya Mazingira NGO's kwa Kamati za Mazingira za Unguja na kutolewa vifaa vya usafi wa mazingira kwa jumuiya za uhifadhi wa mazingira.

*(iv)*kutolewa mafunzo ya usarifu na kuongeza thamani ya dagaa katika vijiji vya Wesha na Ndagoni.

*(v)* Mafunzo ya ulimaji wa zao la mwani kwenye kina kikubwa cha maji yaliyotolewa kwa kina mama wa shehia za Fundo na Kilindi.

**Changamoto za Idara**

Changamoto kubwa zilizopo zinazohusiana na Sera, Sheria na mifumo ya kitaasisi katika Usimamizi wa mazingira, miongoni mwao ni kama zifuatavyo:

*(a)* Kamati imebaini tatizo la ufinyu wa Ofisi kwa Idara ya Mazingira hali inayopelekea kukosekana kwa ufanisi wa utendaji kazi.

*(b)* Udhibiti mdogo wa uingiaji wa vifungashio vya mifuko ya plastiki inayosababisha mifuko hiyo kuonekana kwa wingi katika masoko na sehemu za maduka ya vitu vidogo vidogo sambamba na kuzagaa katika majaa.

*(c)* Ugumu wa maisha na kukosekana kwa elimu ya kutosha juu ya athari za matumizi ya uhifadhi wa mazingira, unaosababisha jamii kukata matofali kiholela ikiwa ni njia moja wapo ya kujipatia riziki.

*(d)* Kamati imeelezwa athari kubwa zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi yanapelekea maji chumvi kuingilia maeneo ya wananchi wanajishughulisha na kilimo kinachosaidia mahitaji yao ya kila siku.

*(e)* Taasisi nyingi zinazohusiana na usimamizi wa mazingira na maliasili hazina uwezo mkubwa wa vifaa na teknolojia bora kwa ajili ya kurahisisha ufuatiliaji wa mazingira.

*(f)* Kamati haikuridhishwa na namna wananchi wanavyoendelea kuharibu mazingira bila kujali nguvu kubwa za Serikali ambazo zinatumika kuyarudisha mazingira katika uasili wake.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kuendeleza matumizi bora na uhifadhi mzuri wa mazingira Kamati pia inashauri yafuatayo:

*(i)* Kamati inashauri taasisi zenye jukumu la kusimamia udhibiti wa uingizaji wa mifuko ya plastiki kusimamia vyema majukumu yako na kuweka udhibiti wa kutosha ikiwa pamoja na kuchukua hatua za kisheria madhubuti ili kukomesha suala hilo.

*(ii)* Kamati inashauri Serikali kuiangalia kwa karibu hali ya kipato cha maisha cha wananchi hasa wanajihusisha na shughuli za ukataji matofali kwa kuwatafutia kazi mbadala za kuwapatia kipato na pia kupanda miti sehemu zilizoathiriwa ili kuirudisha ardhi uasili wake.

*(iii)* Kamati inaishauri Serikali kuendelea kujenga kuta za kuzuia maji ya bahari kuingia katika maeneo ya nchi kavu hasa pembezoni wa kambi za KMKM kisiwa Panza pamoja na kuyalinda maeneo yaliyofaidika na kujengwa kuta hizo.

*(iv)* Kamati inashauri kwa Serikali kuendelea kutoa elimu ya kutosha juu ya uharibu wa mazingira na kuwashajihisha wananchi hao namna bora ya kulinda mazingira kwa kutokata misitu kiholela, kuchimba mchanga na kujenga katika vianzio vya maji.

*(v)* Kamati inapendekeza kwa Serikali kulisimamia eneo lililopimwa lilokuwepo nyuma ya Wizara ya Kilimo kujengwa kwa haraka kwaajili ya matumizi ya Idara.

*(vi)* Kamati inashauri kuongeza jitihada kwa Wizara ya upatikanaji wa vifaa vya Ofisi kupitia Miradi ya Washirika wa maendeleo na Fedha za Serikali.

*(vii)* Kamati inaishauri Serikali kuchukua juhudi za makusudi kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kutekeleza miradi ya maendeleo kupitia SMZ na Washirika wa Maendeleo.

*(viii)* Kamati inashauri Serikali kutafuta mbinu mbadala za kuwasaidia wananchi wa Wilaya ya Micheweni katika kujiongezea kipato ili waweze kuachana na biashara ya ukataji wa matofali pamoja na kuhamasishwa kupanda miti maeneo yaliyoathiriwa na biashara hiyo.

## 3.6 PROGRAMU YA URATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar ni taasisi iliyopo chini ya Ofisi ya makamu wa kwanza wa Rais. Taasisi hii imeanza kazi kwa mujibu wa Sheria Nam. 8 ya mwaka 2021 ambayo imeipa mamlaka na uwezo kisheria wa kuchunguza, kukamata, kupeleleza na kupeleka kesi zote za dawa za kulevya Mahakamani.

Mamlaka pia, katika jukumu la utekelezaji wa Sheria hii imewezesha kuendelea na juhudi za kudhibiti usafirishaji, usambazaji na utumiaji wa Dawa za Kulevya nchini. Aidha, imebainika kuwa mpaka sasa Zanzibar haizalishi dawa za kulevya ingawa imethibitika kwamba Dawa zote zinazokamatwa katika Visiwa vya Unguja na Pemba zinatoka nje ya Zanzibar.

**Mafanikio ya Mamlaka Kudhibiti na Kupambambana na Dawa za Kulevya:**

*(i)* Mamlaka imefanikiwa kufanya operesheni na kuwakamata wahalifu wanaojihusisha na kazi za usambazaji, usafirishaji na utumiaji wa Dawa za Kulevya.

*(i)* Mamlaka kwa kushirikiana na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imefanikiwa kuendesha mashtaka na kupeleka majalada Mahakamani.

*(ii)* Mamlaka imefanikiwa kuanzisha huduma ya mawasiliano kwa njia ya simu ya bure kwa lengo la kutoa taarifa zinazohusiana na dawa za kulevya.

*(iii)* Mamlaka imeendelea kuelimisha jamii juu ya athari ya Dawa za Kulevya kupitia njia mbali mbali kwa Unguja na Pemba.

*(iv)* Mamlaka kufanya ukaguzi wa vielelezo vya kesi za Dawa za Kulevya kwa kuhakikisha dawa zilizokamatwa hazirudi tena mitaani kuathiri jamii na vielelezo vyote vilivyohifadhiwa ambavyo kesi zake zimemalizika vimehakikiwa kwa ajili ya zoezi la kuteketezwa.

*(v)* Huduma za tiba na marekebisho ya tabia zimeendelea kutolewa kwa vijana walioachana na matumizi ya dawa za Kulevya katika kituo cha Serikali cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Kidimni na baadae kuwaunganisha tena na jamii waraibu waliopata nafuu.

*(vi)* Mamlaka inaendelea kuendesha miradi ya ujasiriamali kwa waraibu waliopata huduma ya upataji nafuu.

**Changamoto za Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar.**

Licha ya mafanikio mazuri yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake, Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar imekabiliwa na Changamoto zifuatazo:

*(i)* Kamati imebaini kuwepo kwa upungufu wa vitendea kazi vya vinavyosababisha Ofisi kukosekana kwa ufanisi wa kazi za Mamlaka.

*(ii)* Kamati imeelezwa kuwa jamii inaona muhali kutoa taarifa za uhalifu wa Dawa za Kulevya katika maeneo yao, licha ya juhudi kubwa za Serikali kutoa elimu ya athari za matumizi na usafirishaji wa dawa za kulevya.

*(iii)* Kamati imegundua baadhi ya Masheha kushindwa kutoa ushirikiano ukizingatia biashara hiyo inafanyika katika maeneo yao.

*(iv)* Kamati imeelezwa jamii kukataa kutoa ushahidi Mahakamani hasa linapokuja suala la mashahidi huru walioshuhudia mtuhumiwa wa dawa za kulevya amefanyiwa upekuzi kisheria jambo ambalo linasababisha kesi nyingi kufutwa.

*(v)* Kamati inasikitishwa kuona kwamba Mahakama zinazosimamia kesi za dawa za kulevya kushindwa kufikia maamuzi ya kutaifisha kisheria vyombo ambavyo vimekamatwa na dawa hizo.

*(vi)* Kamati imeelezwa baadhi wa wazazi kukataa kuwachukua watoto wao baada ya kurudi chuo cha urekebishaji wa tabia na kutaka kuwalipia tena ili waendelee kubaki chuoni hapo.

**Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati:**

Kutokana na changamoto hizo ambazo Mamlaka inakabiliana nazo katika mazingira mbali mbali, Kamati inashauri mambo yafuatayo:

*(i)* Kamati inaishauri Serikali kuimarisha fedha za OC kwa mamlaka ili waweze kujitafuta nyenzo za kufanikisha shughuli za Ofisi.

*(ii)* Kamati inashauri Mamlaka kuendelea kutoa elimu kwa jamii na kuongeza mashirikiano yatakayosaidia kupata taarifa za kudhibiti uingizwaji wa dawa za kulevya katika visiwa vya Zanzibar.

*(iii)* Kamati inaishauri jamii kujenga mazoea ya kuwaona waathirika wa Dawa za Kulevya kuwa ni watu wema na wenye kuaminiwa katika jamii baada ya kutolewa katika vituo vya kurekebisha tabia na sio kuwanyanyapaa.

*(iv)* Kamati inapendekeza Mamlaka ya Dawa za Kulevya kuwafundisha waraibu kazi za mikono ipasavyo ikiwemo kilimo, ufugaji, ushoni na kazi nyengine ili watapotoka chuoni hapo waweze kuendesha maisha yao bila utegemezi.

*(v)* Kamati inashauri Serikali kuharakisha marekebisho ya Sheria ya Dawa za Kulevya kwa baadhi ya vifungu ili kuondosha ugumu wa utekelezaji wa Sheria hiyo.

*(vi)* Kamati inashauri Serikali kuongeza mashirikiano na taasisi za haki jinai ili kuimarisha utendaji kazi.

## 3.7 TUME YA UKIMWI ZANZIBAR

Tume ya UKIMWI ya Zanzibar imeanzishwa Mwaka 2002 chini ya Sheria ya Tume ya UKIMWI ya Nam. 3 ya mwaka 2022 kwa lengo kuhakikisha kwamba maambukizo ya Virusi vya UKIMWI yanapungua kwa kuratibu shughuli za kupunguza maambukizo na kuelimisha jamii kuhusu kujikinga na maambukizo ya Virusi vya UKIMWI na athari za unyanyapaa kwa walioathirika

Tume ya Ukimwi imeandaa Mpango wa ufuatiliaji na tathmini wa Mkakati wa Tume ya UKIMWI kwa lengo la kufuatilia na kuimarisha utekelezaji wa Mkakati wa Ofisi. Kamati inaipongeza Tume kwa kuendelea na mchakato wa kutayarisha Mkakati wa Mawasiliano na Utetezi wa VVU na UKIMWI kwa vijana.

**Mafanikio ya Tume ya Ukimwi:**

*(i)* Kuwafikia vijana wengi kupitia midahalo, kongamano, vipindi vya redio na mitandao ya kijamii juu ya masuala mbalimbali ya UKIMWI.

*(ii)* Kuwepo Mkakati wa Mawasiliano wa Vijana ambao utasadia katika kubuni na kutekeleza programu zinazowalenga vijana na kushajihisha mabadiliko ya tabia.

*(iii)* Wadau wameelewa haki za watu wanaoishi na VVU katika upatikanaji wa huduma na wako tayari kushirikiana na Tume kuielimisha jamii.

*(iv)* Uhakika wa upatikanaji wa kondomu za kiume kwa wakati wote wa mwaka, lakini pia kuna changamoto ya ukosefu wa kondomu za kike katika Bohari kuu ya dawa

**Changamoto za Tume ya Ukimwi**

*(i)* Kamati imeelezwa kuwa Ofisi inakabiliwa na Uhaba wa fedha na hivyo kushindwa kutekeleza shughuli ilizopanga. Hata hivyo, shughuli nyingi zilizotekelezwa ni zile zinazogharamiwa na Washirika wa Maendeleo ambazo hazitoi nafasi ya kutekeleza programu zinazolenga jamii moja kwa moja na kuathiri upatikanaji wa huduma mbali mbali za UKIMWI.

*(ii)* Kamati baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji ya Tume imebaini kuongezeka kwa tabia hatarishi zinazoweza kuchochea maambukizo ya VVU hasa kwa jamii ambazo zinahitaji muitiko wa kijamii na kisera katika kupambana nazo.

*(iii)* Kamati pia imegundua tatizo la ukosefu wa gari kwa kuwa lilokuwepo hivi sasa limechakaa na husababisha hatari za kiusalama kwa wafanyakazi na watembea kwa miguu pamoja na kutumia fedha nyingi za utengenezaji kwa ununuzi wa vipuri.

*(iv)* Kamati wakati ikitembelea Tume hii imebaini Tume haina Ofisi yenye kukidhi mahitaji hali inayosababisha kukosekana kwa mazingira mazuri ya kazi na hivyo kuathiri ufanisi wa kazi. Hata hivyo, fedha nyingi zimekuwa zikitumika kwa ajili ya kulipia jengo walilokodi.

*(v)* Kamati imebaini kwamba kuna kiasi kikubwa cha maambukizo ya VVU kwa makundi maalumu.

*(vi)* Kamati imebaini kuna tatizo la kukinzana kwa mikakati ya kupunguza maambukizo ya VVU na mitazamo ya kidini/mila na desturi.

*(vii)* Kamati imebaini kuwa kuna ushiriki mdogo katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

*(viii)* Kamati imebaini mitizamo midogo dhidi ya jamii/uongozi wa ngazi mbali mbali kwamba UKIMWI sio tatizo tena katika nchi yetu.

*(ix)* Kamati imebaini Tume ya UKIMWI ina utegemezi mkubwa wa fedha za wadau wa Mashirika ya Maendeleo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

*(i)* Kamati inashauri Serikali kuongeza mafungu ya fedha za ndani kwa ajili ya muitiko wa Taifa wa UKIMWI.

*(ii)* Kamati inapendekeza kwa Serikali kuendelea kutoa elimu kupitia fursa mbali mbali ikiwemo mitandao ya kijamii na vyombo vya habari, vikundi vya sanaa na mikutano ya wanasiasa.

(iii) Kamati inaishauri Serikali ioneshe wajibu wake kupitia mapambano dhidi ya UKIMWI badala ya kusubiri wafadhili wa mashirika.

(iv) Kamati inaiomba Serikali kuitafutia Tume eneo la kujenga Ofisi kwa ajili ya uendeshaji bora wa shughuli zake ili kuepuka gharama zinazopotea kwa kukodi jengo la Ofisi.

(v) Kamati inashari Tume ya Ukimwi kufanya kazi kwa karibu na wadau wote wakiwemo viongozi wa dini.

(vi) Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio Sera na Sheria ya Ukimwi ili kuweka taraatibu za kisheria za kuwepo kwa mfuko maalumu wa UKIMWI .

(vii) Kamati inaishauri Tume kufanya mikutano na viongozi mbali mbali wakiwemo wanasiasa ya uhamasishaji wa tatizo la ugonjwa wa UKIMWI.

(viii) Kamati inaishauri Wizara kufanya kazi kwa karibu na Tume ya Mipango kuhakikisha miradi mikubwa ya maendeleo inazingatia mapambano dhidi ya UKIMWI.

## 3.8 BARAZA LA TAIFA LA WATU WENYE ULEMAVU

Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar ni moja ya taasisi inayounda Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na hutekeleza kazi zake kwa mujibu wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Haki na Fursa) Nam. 8 ya Mwaka 2022. Baraza linasimamia na kuratibu masuala ya watu wenye ulemavu ikijumuisha usimamiaji wa utekelezaji wa Programu za Ujumuishi, uwezeshaji na kukuza uelewa juu ya masuala ya Watu Wenye ulemavu. Sambamba na hayo, linafanya kazi kwa nia ya kuishauri Serikali juu ya maslahi yote na haki za Watu Wenye Ulemavu.

Kamati inaipongeza Ofisi kwa kuweza kutoa visaidizi kwa watu wenye ulemavu Unguja na Pemba ikiwemo fimbo nyeupe, magongo ya kwapani na baskeli za magurudumu mawili.

Kwa upande mwengine kamati imefarijika kuona mafunzo ya ukalimani wa lugha za alama yametolewa kwa walimu wanaofundisha wanafunzi wenye

Ulemavu wa Uziwi ambayo yaliandaliwa kwa kushirikiana na kitengo cha Elimu Mjumuisho iliyopo Jendele.

**Mafanikio ya Baraza la Watu Wenye Ulemavu:**

*(a)* Baraza kwa mwaka 2023 limefanikiwa kufanya ziara za ufatiliaji kuhusiana na masuala ya watu wenye ulemavu katika shehia mbalimbali kwa wilaya zote za Pemba.

*(b)* Baraza limefanikiwa kutoa msaada wa kijamii kwa kugawa chakula kwa walengwa ili kiweze kuwasaidi katika mlo wa siku kadhaa.

*(c)* Baraza limefanikiwa kuwahamasisha walengwa kujiunga na Vyuo vya Mafunzo ya Amali, kutoa udhamini wa ada ya masomo kwa muda wote, kujikwamua na umaskini na kujiongezea kipato.

**Changamoto za Baraza.**

*(i)* Kamati imebaini Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu linakabiliwa na Ufinyu wa nafasi katika Ofisi zake za Unguja na Pemba.

*(ii)* Kamati imebaini katika mji wa Zanzibar kumeongezeka kwa jamii za omba omba wanaoaminika ni watu wenye ulemavu ambao si wazanzibari.

*(iii)* Kamati imegundua miundo mbinu isiyo rafiki kwa watu wenye Ulemavu.

*(iv)* Kamati imebaini kuna upatikanaji mdogo wa vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu.

*(v)* Kamati imebaini kuwepo kwa udhalilishaji mkubwa katika jamii kwa watu wenye ulemavu wakiwemo wenye ulemavu wa akili.

*(vi)* Kamati imegundua jamii inakabiliwa na uelewa mdogo wa masuala ya watu wenye ulemavu, hivyo huwakosesha haki na fursa za lazima ambazo ndio msingi mkuu wa maisha ya wanaadamu.

*(vii)* Kamati imebaini watu wenye ulemavu wanakabiliwa na umaskini uliokithiri kiasi cha kushindwa kupata mahitaji yao ya lazima ya kila siku.

*(viii)* Kamati inasikitishwa kuona hadi sasa bado kuna ugumu wa upatikanaji wa ajira kwa watu wenye ulemavu kutokana na mitizamo hasi ya waajiri.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

*(i)* Kamati inashauri Serikali kwa kusaidiana na Baraza kufanya ukaguzi wa miundombinu rafiki kwa WWU.

*(ii)* Kamati inashauri Serikali isaidie kutafuta wahisani na wafadhili wataoweza kutoa vifaa visaidizi kwa WWU.

*(iii)* Kamati inazitaka Sekta zinazohusiana na masuala ya udhalilishaji kushirikiana na Baraza ili kutokomeza tatizo hilo kwa WWU.

*(iv)* Ili kuona watu wenye ulemavu wanaepukana na umaskini uliokithiri ni vyema Wakala wa Uwezeshaji Wananchi kiuchumi pamoja na Mfuko wa maendeleo kwa WWU kuhakikisha wanalisimamia vyema suala la umaskini.

*(v)* Kamati inaliomba Baraza la watu wenye Ulemavu kutochoka kutoa elimu kupitia vyombo vya mawasiliano ikiwemo mitandao ya kijamii na majukwaa ya mikutano.

*(vi)* Kamati inaishauri Wizara inayosimamia masuala ya ajira na taasisi binafsi kuhakikisha ajira kwa watu wenye ulemavu zinapewa kipaumbele.

## 4. OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi imeanzishwa mwaka *2010* kutokana na mabadiliko ya *kumi na moja (11)* ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka *1984* toleo la *2010*. Jukumu la msingi la Ofisi hii ni kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na masuala ya Muungano kwa upande wa Zanzibar.

Aidha, majukumu makhsusi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni pamoja na kutoa huduma bora kwa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais; kujenga uhimili wa jamii katika kukabiliana na maafa; kuandaa na kuratibu sherehe na maadhimisho ya kitaifa; kuratibu masuala ya Muungano; kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wa Tanzania Bara. Vile vile, inaratibu na kusimamia shughuli za Baraza la Wawakilishi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Ofisi inaundwa na Idara zifuatazo:

*(i)* Idara ya Huduma za Makamu wa Pili wa Rais.
*(ii)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
*(iii)* Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
*(iv)* Idara ya Maafa.
*(v)* Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa.
*(vi)* Idara ya Kuratibu Shughuli za Serikali.
*(vii)* Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ.
*(viii)* Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba.

Ofisi pia, inasimamia Taasisi zinazojitegemea zifuatazo:

*(i)* Baraza la Wawakilishi la Zanzibar (BLW).
*(ii)* Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).

### 4.1 IDARA YA FARAGHA YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Katika utekelezaji wa programu ya uratibu wa shughuli za Makamu wa Pili wa Rais, Idara hii imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

i) Kufanikiwa kuratibu ziara mbali mbali za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais.

ii) Idara pia, imeratibu Mikutano na Vikao mbali mbali baina ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais na wageni mbali mbali wakiwemo watendaji wa Serikali, Wawekezeji na wageni Mashuhuri.
iii) Idara pia, imepokea na kuratibu ufumbuzi wa malalamiko au migogoro mbali mbali baina ya pande mbili tofauti.
iv) Aidha, Idara imefanikiwa kuhifadhi kumbukumbu za matukio, hotuba na picha mbali mbali za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais kwa ajili ya kumbukumbu na matumizi ya baadae.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Idara ya Faragha:**

Kamati inashauri Idara kuongeza bidii katika kuratibu shughuli za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais kwa kutangaza na kuchapisha taarifa mbali mbali katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii zinazohusu kazi zake akiwa Zanzibar na nje ya Zanzibar lengo kuu ni kuitaarifu jamii habari kuhusiana utendaji wa Serikali.

## 4.2 KAMISHENI YA KUKABILIANA NA MAAFA

Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa ni miongoni mwa Taasisi za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ambayo imeanzishwa chini ya Sheria ya Kukabiliana na Maafa Nam. 1 ya mwaka 2015. Kwa mujibu wa Sheria hii, Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa ndio taasisi yenye jukumu la kuainisha, kuimarisha na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya kukabiliana na maafa hapa Zanzibar.

**Mafanikio ya Kamaisheni ya Maafa:**

i) Kamisheni, imeratibu utoaji wa huduma na misaada ya kibinaadamu katika matukio mbali mbali ya majanga/maafa yaliyotokea Unguja na Pemba.

ii) Katika kuimarisha ghala za vifaa vya operesheni na misaada ya kibinadamu, Kamisheni kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Watoto Ulimwenguni UNICEF imenunua vifaa mbali mbali kwa ajili ya kujiandaa katika kukabiliana na maafa.

iii) Kamisheni imeshiriki katika maonesho ya Siku ya Wakulima nane nane yaliyofanyika Kizimbani Unguja kwa kushirikiana na Kikosi Maalum cha

KMKM kwa ajili ya kuielimisha jamii juu ya shughuli mbali mbali zinazotekelezwa na Kamisheni na wadau wake.

iv) Kamisheni imeratibu zoezi la utoaji wa taarifa za tahadhari za mapema juu ya muelekeo wa mvua za Vuli na athari za El Nino kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

v) Kamisheni imefanya vikao viwili na wahusika wa masuala ya Kukabiliana na maafa Unguja na Pemba katika ngazi ya Wilaya na Shehia, wanasiasa na jamii.

vi) Kamisheni imetoa elimu ya kukabiliana na maafa kwa makundi mbali mbali ya jamii wakiwemo waendesha boda boda wa Wilaya ya Magharibi 'A' ili kupunguza ongezeko la ajali za barabarani.

**Changamoto za Kamisheni ya Maafa Zanzibar**

i) Uhaba wa vyombo vya usafiri ikiwemo gari za kufanyia kazi za operesheni kwa matukio ya majanga na maafa yanayotokea;

ii) Ukosefu wa jengo la Ofisi ambapo kwa sasa Kamisheni inatumia jengo la kituo cha operesheni za dharura iliopo Maruhubi kwa ajili ya ofisi na kupelekea Kituo hicho kutofikia lengo la kuanzishwa kwake.

iii) Ongezeko la matukio ya majanga hasa majanga ya moto, hali inayopelekea uhaba wa misaada ya kibinadamu kwa waathirika wa majanaga hayo; na

iv) Udogo wa bajeti ya Kamisheni ya Maafa na uhaba wa wafanyakazi katika baadhi ya sehemu/vitengo inapelekea taasisi hii kukosa ufanisi wa majukumu yake katika ngazi ya Wilaya, Mikoa na Kitaifa.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Kamisheni ya Maafa**

i) Kamati inashauri Kamasheni kuzidisha kasi ya kutoa taarifa za tahadhari kwa wananchi ili waweze kujikinga na majanga na maafa.

ii) Kamati inashauri Kamisheni kuzidi kutoa elimu kwa jamii juu ya namna bora ya kujikinga na maafa.

iii) Kamati inashauri Serikali kusimamia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mfuko wa maafa kutokana na bajeti ndogo ambayo haikidhi mahitaji ya Kamisheni.

iv) Kamisheni iandae miradi ambayo itaiwezesha kupata vifaa na fedha kwa ajili ya shughuli zake za kila siku. Aidha, Kamisheni iongeze kasi ya kuunga mokono juhudi za wahisani ambao wanajitolea kukabiliana na majanga mbali mbali katika jamii.

v) Serikali kupitia Kamisheni ya Maafa ifanye utafiti wa kina wa kitaalamu kuhusu mfumo wa umeme na miundombinu ya maji taka kwa majengo ya umma ikiwemo skuli na hospitali ili kukabiliana na majanga ya moto ambayo kwasasa kumekuwa yakitokea kila siku.

## 4.3 IDARA YA SHEREHE NA MAADHIMISHO YA KITAIFA

Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa ina jukumu la kuratibu Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na shughuli za Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa. Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa yanayoratibiwa na Idara hii ni Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar pamoja na ushiriki wa Viongozi na wananchi wa Zanzibar katika Sherehe za Uhuru wa Tanzania Bara.

Aidha, kwa upande wa shughuli za kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, Idara inaratibu mazishi ya Viongozi kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Kuwaenzi Viongozi Wakuu wa Kitaifa Nam. 10 ya Mwaka 2019.

Kwa nafasi ya pekee kabisa, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inatoa pongezi za dhati kwa Idara hii kutokana na mafaikio makubwa yaliyopatikana katika kuazimisha sherehe za miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanziabar.

**Changamoto za Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa:**

(i) Uhaba wa vifaa vya sherehe na mapambo kwa ajili ya Serikali na sherehe binafsi.
(ii) Kutokamilika kwa uzio wa jengo la ofisi jambo ambalo linafanya usalama mdogo wa matumizi ya ofisi.
(iii) Uhaba wa vyombo vya usafiri kwa ajili ya sherehe na shuhguli za ofisi.

**Maoni na ushauri wa Kamati kwa Idara:**

(i) Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuandaa bajeti maalumu ambayo itaiwezesha Idara hii kupata vifaa vya kisasa na vyenye kukidhi mahitaji kwa sherehe za kitaifa na zile za binafsi.

(ii) Serikali pia isaidie Idara hii kupata vyombo vya usafiri kwa ajili ya kuendesha shughuli zake za kitaifa.

(iii) Idara iandae mpango maalumu katika bajeti yake ili iweze kuitangaza vyema wiki ya kuwaenzi viongozi wakuu wa kitaifa kwani wananchi waliowengi hawafahamu kuhusu wiki ya kuwaenzi viongozi na shughuli zinazofanyika.

## 4.4 IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI NA OFISI YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SMZ DODOMA

Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali inatekeleza shughuli za kawaida na shughuli za Serikali Dodoma kwa upande wa Tanzania Bara na inasimamia utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini, Zanzibar.s

**Mafanikio ya Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali:**

(i) Kufanya ufuatiliaji wa miradi ya Mfuko wa Jimbo (CDF) kwa ajili ya kubaini changamoto za utekelezaji na kuangalia miradi iliyotekelzwa na hatua iliyofikiwa.

(ii) Kuratibu na kusimamia utoaji wa vibali vya utafiti.

(iii) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika ngazi za Wizara.

(iv) Kupitia afisi za Dodoma, kamati inaipongeza Idara kwa kufanikiwa kupata hati ya kiwanja cha ujenzi wa Ofisi za Uratibu Dodoma katika mji wa Serikali Mtaa wa Mtumba.

(v) Idara imefanikiwa kuitangaza SMZ kupitia mashirika na makampuni mbali mbali yanayotekeleza shughuli zake hapa Tanzania na hivyo kusaidia kutanuka kwa wigo wa uwekezaji hapa Zanzibar.

(vi) Idara pia, imechapisha nakala za vitabu vya Taarifa ya Tathmini ya Sera za Kisekta Zanzibar 2022 na vya Muongozo wa Uwasilishaji na Uandishi wa Sera za Kisekta, Zanzibar.

**Changamoto za Idara ya Uratibu wa SMZ Dodoma**

Kamati katika kufuatilia taarifa za utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024 ilifanikiwa kutembelea Idara ya Uratibu wa SMZ Dodoma kwa lengo la kufahamu hali ya utendaji wa majukumu yake. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kadhaa ambazo zinaleta athari katika kazi zao.

Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo:

(i) Uhaba wa watendaji katika kada mbali mbali ikiwemo wenye uzoefu wa masuala ya ushirikiano wa Kimataifa.
(ii) Uchakavu na uhaba wa usafiri.
(iii) Ukosefu wa makaazi ya uhakika kwa watendaji wa idara.
(iv) Uchakavu wa miundombinu ya maji taka, mfumo wa umeme na mawasiliano ya ndani ya ofisi.
(v) Uhaba wa vitendea kazi vya ofisi.

**Maoni na ushauri wa Kamati kwa Idara ya Uratibu wa SMZ**

(i) Licha ya ofisi ya uratibu wa SMZ kuhamia Dodoma Kamati inashauri ofisi ya Dar Es Salaam iendelee kuwepo kutokana na idadi kubwa ya watumiaji wake kuwepo Dar Es Salaam.

(ii) Kamatia pia inaishauri Serikali kuweka kipaumbele maalumu kwa ofisi ya Uratibu katika kupatiwa fedha za matumizi mengineyo.
(iii) Kamati inashauri Idara hii kuzishawishi taasisi za SMZ hapa Zanzibar kushiriki kikamilifu katika mikutano na makongamano mbali mbali yanayofanyika Tanzania Bara kwa ajili ya kujenga utendaji bora wa Serikali kwa wananchi.

(iv) Katika ugawaji wa gari kwa taasisi za umma, kamati inaishauri Serikali kuwapatia Idara ya Uratibu Dodoma gari mpya kwa ajili ya matumizi yake ya kawaida.

(v) Idara pia izishawishi taasisi za SMZ kuandika miradi kwa kuzingatia vipaumbele vya nchi na Dunia kwa ujumla ili kupatiwa ufadhili wa miradi husika.

## 4.5 MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII KUPITIA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASIKINI (TASAF)

Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali pia inasimamia Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini ambapo mpango huu umejikita katika kuhakikisha unapunguza umasikini uliokithiri katika Kaya za Walengwa wa Mpango kwa kuzipatia ruzuku na fursa mbali mbali hapa nchini ikiwemo afya bora, elimu bora na kujikimu kwa kupata mlo kamili.

**Mafanikio ya Utekelezaji wa Mpango**

(i) Kamati inatoa pongezi katika utekelezaji wa Mpango kwani zaidi ya asilimia 98 ya Kaya za Walengwa zimeendelea kupokea ruzuku na kuzitumia kulingana na maelekezo na miongozo ya Mpango Kitaifa.

(ii) Kaya za Walengwa zimeanzisha miradi ya kuongeza kipato cha Kaya na hivyo kuweza kuyafikia malengo ya Mpango.

(iii) Miradi ya kijamii imeweza kutelekezwa katika Shehia mbali mbali Unguja na Pemba kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za kijamii, miongoni mwa Shehia hizo ni Shehia, Chuini, Shehia ya Uzi, Shehia za Donge kwa upande wa Unguja na Shehia ya Piki, Shehia ya Kiwani na Shehia ya Kinyikani kwa upande wa Pemba.

(iv) Kwa namna nyengine mpango wa Kunusuru Kaya Masikini umeziwezesha Kaya za Walengwa kuweza kupata mahitaji yake ya msingi kwa kaya husika.

(v) Watoto wa Kaya za Walengwa wameweza kutimiza masharti ya msingi ya elimu na afya ya Mpango hivyo, kuweka misingi imara ya rasilimali watu ya baadae.

(vi) Kuwepo kwa mashirikiano mazuri baina ya Utekelezaji wa Mpango kwa Tanzania Bara na Zanzibar jambo linapelekea mradi kutekelezeka kwa wepesi na weledi mkubwa.

**Changamoto za Utekelezaji wa Mpango**

(i) Kamati imebaini baadhi ya Kaya za Walengwa kutoshiriki katika zoezi la tathmini/uhakiki wa Kaya, hivyo kupelekea kaya hizo kusimamishwa kupokea ruzuku.

(ii) Kamati pia, imebaini baadhi ya kaya za walengwa kutoshiriki katika vipindi vya warsha jamii wakati wa malipo ya kaya, hivyo kutopata maelekezo na miongozo ya Mpango.

(iii) Kamati imebaini baadhi ya walengwa kutotumia rasiliamali fedha wanazolipwa kwa malengo ya mradi na badala yake hutumia nje ya malengo, athari inayojitokeza ni baadhi ya Walengwa kushindwa kutoka kwenye Mpango au kuwepo kwa malalamiko wakati wanapotolewa.

**Maoni na Ushauri wa Kamati katika Utekelezaji wa Mpango**

(i) Kamati inashauri katika utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini jamii kupatiwa elimu ya kutosha juu ya umuhimu wa mradi huu na kufahamu malengo yake katika kupunguza umasikini uliokithiri nchini.

(ii) Kamati inashauri idara isisite kuwatoa walengwa ambao wamedumu kwa muda mrefu katika Mpango na badala yake watoe fursa kwa walengwa wengine kuweza kushiriki na kuimarisha hali zao za maisha.

(iii) Kamati inashauri katika utekelezaji wa Mpango changamoto zinapojitokeza kuchukuliwa hatua kwa haraka ili kuweka mazingira bora ya utekelezaji wa miradi.

(iv) Vile vile, Kamati inashauri Serikali kutoweka mwanya kwa baadhi ya watendaji wa Umma au viongozi kuingia katika Mpango na ikitokezea hivyo basi hatua za haraka ziweze kuchukuliwa.

## 4.6 BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ni miongoni mwa mihimili *mitatu (3)* ya Serikali ambapo lilianzishwa kwa ajili ya kustawisha demokrasia na

uwakilishi wa watu wa Zanzibar. Majukumu makuu ya Baraza ni kutunga sheria, uwakilishi wa wananchi na usimamizi wa Serikali.

Baraza la Wawakilishi Zanzibar katika kazi zake za msingi kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar Mwaka 1984 ni kutunga sheria, kuihoji Serikali, kupitisha bajeti ya Serikali pamoja na kuidhinisha matumizi ya Serikali.

Katika mafanikio ya Afisi ya Baraza; Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa majukumu yake kwa muda wote, kwani imeweza kutekeleza ipasavyo malengo yake kwa kuratibu vikao vya Baraza pamoja na Kamati zake kwa ufanisi zaidi.

Vile vile, Kamati inaipongeza Afisi kwa kukamilisha mradi wa lifti ambayo itawasaidia zaidi watu wasiojiweza ili kuwapunguzia usumbufu wanapokuwa Barazani.

Aidha, Afisi imekamilisha uwekaji wa mfumo wa CCTV kamera katika jengo la ofisi na hivyo kuimarisha suala la ulinzi na usalama kwa wajumbe na watumiaji wa majengo ya Baraza. Sambamba na hilo afisi imeanza kuongeza ukuta kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na usalama.

**Changamoto za Baraza la Wawakilishi Zanzibar**

Bila shaka kila penye mafanikio hapakosi kuwa na changamoto na hii ndio hatua muhimu ambayo itakufanya uweze kufikia mabadiliko.

Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo:

*(a)* Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa nafasi za ofisi kwa watendaji na wadau wakuu wa Baraza akiwemo Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kumbi za kamati za Baraza.

*(b)* Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa vyombo vya usafiri hususan gari za Kamati kwa Unguja na Pemba na hivyo kulazimika kuazima au kukodi usafiri kwa ajili ya shughuli za Baraza.

*(c)* Kamati imegundua kuendelea kuwepo kwa hali ya joto katika eneo la mapokezi kutokana na kukosekana kwa mfumo mzuri wa kupoza hewa.

*(d)* Kamati imebaini kuwepo kwa uchakavu mkubwa wa Ukumbi wa Mikutano wa afisi ya Pemba, jambo ambalo linapelekea kutumika fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo ya kila siku.

(e) Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa wafanyakazi katika afisi ya uratibu Pemba.
(f) Kamati inasikitishwa na kutokamilika kwa muda mrefu mpango wa maslahi ya wafanyakazi tokea kupitishwa kwa muundo wa afisi ya Baraza.
(g) Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa vifaa vya ofisi ikiwemo fotokopi na printa kwa baadhi ya ofisi hali inayopelekea kuzorota kwa baadhi ya majukumu.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar**

*(a)* Kamati inashauri Serikali kuangalia umuhimu wa usafiri wa Baraza katika shughuli za Kamati.
*(b)* Kamati inashauri mradi wa ujenzi wa jengo jipya la ofisi kuanza haraka kutokana na ufinyu wa nafasi kwa sasa.
*(c)* Kamati inashauri Tume ya Utumishi ya Baraza kushughulikia tatizo la uhaba wa wafanyakazi katika afisi ya Pemba ili kusaidia kuratibu vyema majukumu yao.
*(d)* Kamati inashauri Afisi ya Baraza kuzidisha kasi ya kutoa mafunzo kwa watendaji wa Baraza kwa lengo la kujenga uzoefu katika mazingira ya kibunge.
*(e)* Kamati inashauri afisi kufanya marekebisho katika mfumo wake wa kupoza hewa katika eneo la mapokezi.
*(f)* Kamati inashauri afisi kushughulikia suala la upatikanaji wa vitendea kazi kwa wakati na kwa mujibu wa mahitaji yake.
*(g)* Kamati inaishauri afisi kuongeza kasi ya kusimamia maslahi ya watumishi wake kwa wakati kulingana na muundo mpya wa afisi.

## 4.7 TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR

Tume ya Uchaguzi Zanzibar ni chombo kilicho anzishwa mwaka *1979* chini ya kifungu cha *73* cha Katiba ya Zanzibar ya *1979*. Kwa hivi sasa Tume ya Uchaguzi Zanzibar inafanya kazi kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya *1984*, Sheria ya Kuanzishwa kwa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Nam. 1 ya *2017*, Sheria ya Uchaguzi, Nam. *4* ya *2018* na Sheria ya Kura ya Maoni, Nam. *6* ya *2010*.

Miongoni mwa majukumu makuu ya Tume ni kukuza na kusimamia mienendo ya uchaguzi wa Rais wa Zanzibar, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.

Kamati imeridhishwa na utendaji wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwa namna ilivyofanikiwa katika kutekeleza majukumu yake na hivyo kukamilisha ile azma kuu ya nchi ya kuijenga Zanzibar kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Kamati inaipongeza Tume kwa kufanikiwa kusimamia na kukamilisha vyema uchaguzi mdogo wa Jimbo la Mtambwe na Wadi ya Welezo kutokana na kufanyika kwa misingi ya uhuru na haki ambapo kila mwananchi mwenye sifa aliweza kuitumia fursa hii ipasavyo.

Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuipatia Tume ya Uchaguzi Zanzibar usafiri wa uhakika kwa ajili ya ufuatiliaji na utekelezaji wa majukumu yake kwa afisi za Unguja na Pemba.

**Changamoto za Tume ya Uchaguzi**

Kamati imebaini changamoto kubwa ya Tume ya Uchaguzi ni uhaba wa ofisi za kudumu za Wilaya kwa upande wa Unguja na Pemba jambo linalopelekea ugumu wa kazi za Tume kwa siku za uchaguzi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar**

*(a)* Kamati inashauri Tume kuharakisha kusimamia mradi wa ujenzi wa afisi za Wilaya ya Mkoani, Wilaya ya Chake Chake, Wilaya ya Micheweni na Wilaya ya Wete kwani Wilaya hizi tayari zimeshapata viwanja kwa ajili ya ujenzi.

*(b)* Tume inashauriwa kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kutumia haki ya kupiga kura na kuiasa jamii kulinda amani na utulivu uliopo kipindi cha uchaguzi.

*(c)* Kamati inashauri Serikali kuongeza nguvu ya utendaji kwa Tume kwa kuwapatia wafanyakazi wa kutosha katika vituo vya Wilaya na Makao Mkuu kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kazi zake.

## 5. OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora (OR – KSUUB) ina jukumu la kusimamia na kuhakikisha kuwa masuala ya Katiba na Sheria, Utumishi na Utawala Bora yanaimarika kwa kasi kubwa ili kuweza kuleta ufanisi na faida pamoja na maendeleo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wananchi kwa ujumla. Aidha, jukumu kubwa la wizara hii kuhakikisha dhana kamili ya utawala bora imesimama na kumfikia kila mmoja katika misingi ya haki na sheria ili kujenga misingi iliyo bora ya demokrasia katika nchi yetu.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inasimamia jumla ya programu 15, kati ya hizo, programu sita (5) zinasimamiwa na kutekelezwa kupitia idara zilizo chini ya Katibu Mkuu na programu kumi (10) zinatekelezwa na taasisi zinazojitegemea kama ifuatavyo:

i. Programu ya Masuala ya Sheria;
ii. Programu ya Usimamizi na Utawala Bora;
iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa ARKSUUB;
iv. Programu ya Uendeshaji wa Utumishi wa umma;
v. Programu ya Usimamizi na Upatikanaji haki;
vi. Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria;
vii. Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai
viii. Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria;
ix. Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini;
x. Programu ya Huduma za Serikali Mtandao;
xi. Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi wa Umma;
xii. Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma;
xiii. Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi;
xiv. Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma;
xv. Programu ya Uajiri Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini.

Aidha, Wizara hii inaunda na Idara zifuatazo:

*(a)* Idara ya Utumishi na Uendeshaji,
*(b)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti,
*(c)* Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi,
*(d)* Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu,
*(e)* Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria,
*(f)* Idara ya Utawala Bora,
*(g)* Afisi Kuu Pemba.

Aidha, Chuo cha Utumishi wa Umma (IPA) kinapokea ruzuku kutoka Serikalini ili kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

Vile vile, Wizara hii inasimamia Taasisi zinazojitegemea zifuatazo:

*(a)* Mahkama Kuu,
*(b)* Afisi ya Mwanasheria Mkuu (AGC),
*(c)* Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP),
*(d)* Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
*(e)* Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar,
*(f)* Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma,
*(g)* Ofisi ya Waqfu na Mali ya Amana,
*(h)* Wakala wa Serikali Mtandao,
*(i)* Tume ya Kurekebisha Sheria,
*(j)* Kamisheni ya Utumishi wa Umma,
*(k)* Tume ya Utumishi Serikalini,
*(l)* Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA).

Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imegawika katika sekta kuu nne (4) ambazo ni Sekta ya Sheria, Sekta ya Utumishi, Sekta ya Utawala Bora na Sekta ya Uratibu na Uendeshaji.

## 5.1 IDARA YA MIUNDO YA TAASISI, UTUMISHI NA MASLAHI YA WATUMISHI

Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi imeanzishwa kwa Sheria ya Utumishi wa Umma nam. 2 ya mwaka 2011. Kimsingi idara hii pamoja na majukumu mengine inawajibu wa kutayarisha na kufanya mapitio na kufanya Tathmini ya Muongozo za Fomu ya Upimaji Utendaji Kazi. Kutayarisha Miundo ya Utumishi na Taasisi pamoja na kuifanyia mapitio na kutoa miongozo kabla ya miundo hiyoo kuwasilishwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Aidha Idara hii inahusika na kufanya marekebisho ya Mshahara, maposho, kuweka na kuondoa kiuizi cha Mishahara pamoja na kusimamia mfumo wa malipo kwa watumishi wa umma.

**Mafanikio ya Idara ya Miundo**

Kamati imeelezwa Idara imeweza kufanya marekebisho ya jumla ya mishahara kwa Watumishi wa Umma mwezi wa Julai 2022 yaliyowahusisha Watumishi wa Serikali Kuu, Taasisi na Mamlaka zinazojitegemea pamoja na taasisi nyengine. Kufanya marekebisho ya mishahara kwa watumishi wanaolipwa mshahara pungugu iliyotokana na kasoro zilizojitokeza wakati wa marekebisho ya jumla ya watumishi, kuwapanga watumishi katika miundo ya watumishi kuhusiana na vyeo vyao vipya, madaraja, ngazi za mishahara pamoja na majukumu yao.

**Changamoto za Idara ya Miundo**

Pamoja na Mafanikio yaliyopatikana, Idara inakabiliwa na Changamoto zifuatazo:

*(a)* Kamati imebaini kuwa idara inakabiliwa na tatizo la uwasilishwaji wa baadhi ya taarifa za watumishi zisizo sahihi, katika kipindi cha marekebisho ya jumla ya mishahara na kusababisha marekebisho ya mshahara kutofanyika kwa usahihi.

*(b)* Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la kuchelewa kuwasilishwa kwa taarifa za watumishi katika marekebisho ya mishahara kutoka Taasisi za Serikali.

*(c)* Imeelezwa kwamba baadhi ya maombi ya marekebisho ya maslahi ya watumishi yanayowasilishwa hukosa vielelezo vinavyohitajika na hivyo kurudisha nyuma zoezi la marekebisho.

**Maoni, ushauri na Mapendekezo ya kamati.**

*(i)* Kamati inashauri na kupendekeza kwa Taasisi za Serikali kuhakikisha taarifa wanazo ziwasilisha Ofisi kuu ya Utumishi zimehakikiwa na kwa usahihi;

*(ii)* Kamati inawataka Wakuu wa Taasisi wanaosimamia taarifa za Watumishi zinazoombwa kuziwasilishwa kwa wakati pamoja na kutumia njia za kielektroniki katika uwasilishaji wa taarifa hizo ili kurahisha upatikanaji wa taarifa husika;

*(iii)* Kamati pia inapendekeza kwa taasisi za Serikali kutumia Mfumo wa Taarifa za watumishi na malipo katika uwasilishaji wa taarifa.

*(iv)* Kamati inashauri Idara kusimamia ipasavyo kwa taasisi ambazo zinachukua muda kutekeleza marekebisho ya maombi ya Mishahara.

## 5.2 IDARA YA MIPANGO NA RASILIMALI WATU

Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ni kiungo muhimu katika Wizara hii pamoja na Taasisi zake. Idara hii ina jukumu la kuratibu shughuli zote za Wizara.

Katika kipindi hiki Idara ya Mipango, Sera na Uafiti imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo: -

*(a)* Kufanya kikao cha awali cha ushirikiano kati ya SMZ na SMT kwa wataalamu na Makatibu Wakuu wa Sekta ya Sheria kimefanyika na baadae kumalizika kwa Mawaziri wa Sekta ya Sheria;

*(b)* Idara imefanikiwa kuwafanyia majaribio jopo la wataalamu katika Programu ya Kupambana na Uhalifu unaohusiana na masuala ya fedha na makosa mengine ya jinai ya kupangwa.

## 5.3 WAKALA WA SERIKALI MTANDAO

Wakala wa Serikali Mtandao imeanzishwa kwa mujibu wa sheria Nam. 12 ya mwaka 2019. Ikiwa na jukumu la kuandaa na kusimamia Sera, Kanuni na Miongozo ya maendeleo na matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa Umma, kuandaa Mipango ya Kitaifa ya maendeleo na matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa umma pamoja na kuratibu utekelezaji wa mipango hiyo na kuishauri Serikali katika matumizi bora ya TEHAMA katika uendeshaji na utoaji huduma kwa umma.

Katika kuleta tija kwenye matumizi mazuri ya TEHAMA, Wakala wa Serikali Mtandao imeweza kuandaa jumla ya miongozo minne ikiwemo Rasimu ya Muongozo wa kiufundi wa usalama, Usimamizi wa huduma, uendeshaji wa kamati na viwango na miongozo ya Utayari wa TEHAMA katika Miundombinu inayomilikiwa na Serikali.

Kamati inaipongeza Wakala wa Serikali Mtandao kwa kuweza kufanyiwa marekebisho ya sheria yake Nam. 12 ya mwaka 2019 na kupitishwa rasmi

katika Baraza hili tukufu ambapo badala ya Wakala sasa itakuwa na muundo mpya wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar.

**Changamoto za Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar**

Mbali na mafanikio yaliyopatikana kwa Wakala wa Serikali Mtandao mwaka huu, bado Wakala inakabiliwa na changamoto ambazo kwa namna moja au nyengine zinaathiri utekelezaji wa majukumu ya kila siku kama ifuatavyo:

*(i)* Kamati imeelezwa Wakala inakabiliwa na uhaba wa Wafanyakazi katika fani za TEHAMA na kada nyenginezo hivyo hupelekea mrundikano wa kazi;

*(ii)* Kamati imebaini Sheria ya sasa inayotumika Wakala wa Serikali Mtandao haiendani na kasi na mahitaji ya mfumo ambao unakusudiwa kutumika kwa taasisi zote za Serikali;

*(iii)* Nafasi ndogo ya ofisi inachangia kutokuwepo kwa mazingira mazuri ya kufanyia kazi, hali iliyopelekea kukodi ofisi katika jengo la Michenzani Mall ambapo hatua za uwekaji wa miundombinu ya TEHAMA pamoja na uwekaji vitu vya samani umeshakamilika;

*(iv)* Uelewa mdogo wa matumizi ya mifumo ya TEHAMA imebainika kuwa ni changamoto wakati Wakala ilipofanya zoezi la tathmini la utumiaji wa mifumo ya pamoja ya Serikali. Mpaka sasa bado kuna watendaji ambao hawatumii e-mail rasmi za Serikali na baadhi ya Taasisi zinatumia njia za kawaida za kutuma, kupokea na kuhifadhi barua badala ya kutumia Ofisi Mtandao (e-Office).

**Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati:**

*(i)* Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kuwasilisha ndani ya Baraza la Wawakilishi Mswada wa Kubadilisha Wakala kuwa Mamlaka. Hata hivyo, Kamati inasisitiza mswada huu utapokamilika na kuwa Sheria kuhakikisha inatekeleza wajibu wake ipasavyo na kuzitaka taasisi zote za Serikali kutumia mfumo wa (e-Office) katika utekelezaji wa kazi zao;

*(ii)* Kamati inasisitiza Wakala kuendelea na zoezi la kujenga uelewa juu ya umuhimu wa kutumia mifumo rasmi ya Serikali kwa lengo la kulinda na

kutunza siri za Serikali, kurahisisha mawasiliano na kuimarisha utoaji wa huduma za jamii;

*(iii)* Kamati inashauri kuupa umuhimu mpango wa muda mrefu na wa kudumu wa kutafuta eneo la ardhi kwa ajili ya kujenga jengo la Afisi ya Serikali Mtandao (e- Government Building).

*(iv)* Kamati inapendekeza kwa Wakala kuendelea na mpango wa kuajiri wafanyakazi kwa kada wanazozihitaji kwa mujibu wa kibali cha utumishi kilichotolewa kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

*(v)* Kamati inashauri Wakala kuweka mifumo madhubuti ya TEHAMA kwa Taasisi zote za Serikali kwa faida ya nchi yetu.

## 5.4 KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

Kamisheni ya Utumishi wa Umma ni chombo cha kikatiba kilichoanzishwa chini ya kifungu cha 116 cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 (Toleo la Mwaka 2010) na kifungu cha 17 cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya Mwaka 2011, kama ilivyorekebishwa na Sheria Nam. 5 ya Mwaka 2012. Aidha, Uanzishwaji wa Kamisheni hii ni moja ya jitihada za Serikali katika kuleta mageuzi katika Utumishi wa Umma kwa kusimamia Tume zote za Utumishi pamoja na kuratibu mambo mbali mbali ya Utumishi wa Umma ili kuleta tija kwa wananchi.

Kufuatia Mafanikio yaliyopatikana kwa Mwaka huu kwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeridhishwa na utendaji wa kushughulikia mapendekezo ya Miundo ya Taasisi na Miundo ya Utumish kutoka Taasisi za Umma ikiwemo ZAWA, DPP, ZIC, Kamisheni ya Ardhi na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Aidha, Kamisheni imefanikiwa kufanya ukaguzi maalumu wa masuala ya kiutumishi katika Wizara nane (8) na Taasisi kumi na sita (16) zinazojitegemea za SMZ Unguja na Pemba pamoja na kushughulikia rufaa na malalamiko yaliyowasilishwa Kamisheni.

### Changamoto za Kamisheni ya Utumishi wa Umma

Pamoja na mafanikio makubwa ambayo yamepatikana katika utekelezaji wa shughuli za Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati wakati ikifuatilia utekelezaji wa Taasisi hii imebaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo:

*(a)* Kamati imebaini bado Kamisheni inakabiliwa na Ukosefu wa fedha za kukidhi kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa muda uliopangwa.

*(b)* Kamati imegundua Ofisi inakabiliwa na uchakavu wa jengo ambalo halipo katika hali nzuri na hivyo, hupelekea uhaba wa nafasi kwa watendaji wake.

*(c)* Kamati pia, imebaini kuwa kamisheni inashindwa kukidhi vyema suala la utoaji wa huduma za kiutawala hasa katika ununuzi wa vifaa vya ofisi ikiwemo kompyuta, vifaa vya kuandikia, zulia na samani za Ofisi.

**Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati:**

*(a)* Kamati inashauri Kamisheni kulisimamia suala la muda wa kazi kwa watumishi wa Serikali kuingia na kutoka kazini.

*(b)* Kamati inaiomba Serikali kusimamia upatikanaji wa fedha kwa kamisheni kwani kushindwa kuwajibika kwa taasisi hiyo ni sawa na kurudisha nyumba Taasisi zote za Serikali.

*(c)* Kamati inaishauri Kamisheni kuzifuatilia kwa kina taasisi ambazo zinaidhinishiwa Muundo ili ziweze kutekeleza miundo ya maslahi mapya na ngazi mpya kwa watendaji.

## 5.5 TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Tume ya Utumishi Serikalini ni chombo kinachojitegemea kilichoanzishwa na Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 chini ya kifungu 117, Toleo la 2010 na kifungu 33 cha Sheria ya Utumishi wa Umma, nambari 2 ya mwaka 2011. Tume kwa ujumla ina jukumu la kusimamia Utumishi katika Serikali kwa uadilifu na kufuata misingi ya Utawala Bora.

Katika kipindi hiki Tume imekuwa ikitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria pamoja na miongozo kutoka Serikalini. Sambamba na hayo, Kamati imeridhishwa na utendaji wa Tume kwa kipindi hiki licha ya changamoto kadhaa ambazo zimekuwa zikiathiri sekta ya Utumishi nchini.

### Changamoto za Tume ya Utumishi Serikalini

Kamati wakati ikifuatilia utekelezaji wa kazi zake imegundua Tume ya Utumishi Serikalini inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Kamati wakati ikipokea taarifa imebaini uelewa mdogo wa Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 na Kanuni zake kwa baadhi ya watendaji wa Taasisi na Watumishi wa Umma.

*(ii)* Kamati imebaini tatizo la Ukosefu wa jengo na uchache wa nafasi ya kuweza kukidhi watumishi waliopo.

*(iii)* Kamati imebaini Ufinyu wa bajeti ambao unasababisha kutotekeleza majukumu yao kwa mipango iliyowekwa.

*(iv)* Kamati imebaini changamoto ya maombi ya nafasi za ajira hayatekelezwi ipasavyo kwa mujibu wa matakwa ya taasisi.

*(v)* Kamati imeelezwa kuwa Tume inakabiliwa na upungufu wa wafanyakazi ambao wameshindwa kupatikana kutokana na ukosefu wa nafasi.

### Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Tume ya Utumishi Serikalini

*(i)* Kamati inashauri Tume kutoa elimu kwa watendaji wa Taasisi na Watumishi wa umma kila mwaka kutegemea na uajiri unaofanyika kwa Sheria ya Utumishi wa Umma pamoja na Kanuni zake.

*(ii)* Kamati inashauri Serikali kutoa vibali vya ajira kwa mujibu wa maombi ya ajira ya taasisi husika.

*(iii)* Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwapatia mazingira mapya ya Ofisi Tume ya Utumishi. Hata hivyo, Kamati inashauri kupatiwa jengo la kudumu litalokidhi mahitaji ya watendaji.

*(iv)* Kamati inapendekeza kwa Serikali kuipa kipaumbele changamoto ya ufinyu wa fedha linalokwamisha shughuli nyingi za kiutendaji maofisini.

## 5.6 IDARA YA UTAWALA BORA

Idara ya Utawala Bora katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2023/2024, imefanikiwa kurusha hewani vipindi 17 kupitia Shirika la Utangazaji ZBC na Redio jamii Mkoani na Micheweni Pemba. Aidha, posti kadi zimeandaliwa na kurushwa kwenye mitandao ya kijamii zinazozungumzia masuala ya Utawala Bora.

Idara pia, imefanya semina juu ya mafunzo ya Utawala Bora kuhusu umuhimu wa utunzaji wa rasilimali za nchi kisiwani Pemba kwa Watendaji wa taasisi binafsi, imetoa elimu juu ya usuluhishi wa migogoro kwa shehia na Kamati ya polisi jamii, Afisa wa Polisi wa Shehia na Wananchi wa Shehia ya Finya Wilaya ya Wete.

Idara imepokea na kufanya uchunguzi wa tuhuma za malalamiko ya ukiukwaji wa sheria ya maadili ya viongozi wa umma, ambapo malalamiko hayo yanayohusiana na matumizi mabaya ya madaraka uchunguzi wake bado unaendelea.

Kamati kupitia Idara hii imefarijika kuona imeandaa na kuwasilisha Ripoti ya Saba ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka 2022/2023 kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hatua zake kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma inavyoelekeza na hatimae Ripoti hii kuiwasilisha Barazani.

Kamati ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inaipongeza Idara pia kwa kushiriki na kutoa elimu kuhusu Sheria ya Maadili katika maonesho ya Siku ya Mapambano dhidi ya Rushwa Barani Afrika yaliyofanyika Jijini Arusha, kupitia maonesho hayo, wananchi na viongozi mbali mbali wa kitaifa na kimataifa wasiopungua 280 walitembelea katika banda la maonesho ya Tume ya Maadili na kupatiwa vipeperushi na vijarida vilivyoandaliwa.

## 5.7 AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (CAG)

Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ina wajibika kikatiba kufanya ukaguzi wa hesabu za Serikali kwenye Sekta za umma za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuzingatia matakwa ya Ibara

112 ya katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Aidha, Afisi hii inafanya kazi zake kwa kuzingatia sharia na miongozo mbalimbali.

Kamati imefarijika kuona Afisi hii inaendelea kufanya kazi za ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2022/2023, kufuatilia na kusimamia stahiki za wafanyakazi, kuendelea kuwajengea uwezo wa wafanyakazi na kufanya utekelezaji wa maagizo mbali mbali yanayotolewa na Serikali.

Kwa upande wa Pemba, Kamati imeridhishwa na kuona Afisi inaendelea kufanya kazi za ukaguzi wa hesabu za Serikali pamoja na ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo, kwa lengo la kudhibiti matumizi ya fedha na rasilimali za Umma katika Taasisi mbalimbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**Mafanikio ya Afisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali:**

*(a)* Afisi imefanikiwa kufanya ukaguzi wa kiufundi unaohusiana na ujenzi wa Hospitali za Wilaya kwa Unguja na Pemba.
*(b)* Afisi katika utekelezaji bora wa kazi zake imefanikiwa kufanya ukaguzi wa kiufundi kuhusiana na ununuzi na usambazaji wa vifaa vya kisasa.
*(c)* Afisi imeweza kufanya ukaguzi wa kiufundi unaohusiana na ukarabati wa Uwanja wa Gombani Stadium Pemba.
*(d)* Kufanya ukaguzi wa majalada 590 ya wanachama wastaafu wa Mfuko wa Hifadhi ya jamii ZSSF.

**Changamoto za Afisi ya CAG Zanzibar**

Mbali na mafanikio yaliyopatikana Afisi bado inakabiliwa na changamoto mbali mbali katika kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

*(i)* Kamati imebaini Ukosefu wa vitendea kazi vya kupimia ubora wa majengo, vifaa vya kupimia urefu wa visima na ubora wa maji;

*(ii)* Kamati imebaini kuwepo tatizo la usafiri;

*(iii)* Kamati wakati ikitembelea Ofisi ya CAG Unguja imebaini Ubovu na uchakavu wa jengo la udhibiti unaotokana na uvujaji wa paa unaopelekea watendaji kushindwa kufanya kazi zao kipindi wa mvua;

*(iv)* Kamati wakati ikipokea taarifa ya Utekelezaji imebaini kwamba ofisi inakabiliwa na uchache wa uingizwaji wa fedha za matumizi mengineyo (OC) na kupelekea utekelezaji hafifu wa kazi zilizoainishwa katika mpango wa bajeti;

*(v)* Kamati pia imebaini kuwepo kwa uchache wa wafanyakazi kwa muda mrefu hasa katika Afisi ya Pemba jambo linalozorotesha kasi ya ufanyaji kazi.

**Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati:**

*(a)* Kamati inaipongeza Afisi ya CAG kwa kushirikishwa kufanya kazi za ukaguzi katika Balozi za Tanzania zilizopo katika nchi mbali mbali;

*(b)* Kamati inaipongeza Afisi kwa kupata nafasi za kuajiri wafanyakazi katika kada za Kimahakama na kiuchunguzi. Hata hivyo, inaiomba Serikali kulitafutia ufumbuzi suala la watendaji wapya zaidi wenye utaalamu unaohitajika ili kupunguza uzorotaji wa kazi za Afisi;

*(c)* Kamati inaiomba Serikali kuingalia Ofisi ya CAG kutokana na ugumu wa kazi wanazozifanya kwa kuwawezesha ipasavyo ili waweze kupata vitendea kazi vya kupimia kulingana na kazi zao.

*(d)* Kamati inasikitishwa na ubovu wa Jengo la Afisi ya CAG na kuishauri Serikali kutafuta uwezekano wa kuyafanyia ukarabati majengo ya Afisi hiyo au kuwapatia eneo la kujenga upya;

*(e)* Kamati pia, inaishauri Serikali kuangalia kwa kina umuhimu wa fedha za matumizi mengineyo kwa taasisi hii, kwani kiwango wanachopata hakilingani na majukumu yao;

*(f)* Kamati kwa mara nyengine inasikitishwa na hali mbaya ya basi linalotumika katika Afisi ya CAG ambalo halikidhi kwa matumizi ya Afisi. Hivyo, tunashauri, Serikali kuweka mkakati maalumu wa kuipatia taasisi hii usafiri wa uhakika ili iwe ni nyenzo muhimu katika kazi zao. Aidha, katika suala hili ni vyema CAG akapewa uwezo wa kununua gari zake mwenyewe badala ya kusubiri mgao wa magari kutoka Serikalini.

## 5.8 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR (ZAECA)

Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar inafanya kazi zake kwa kuzingatia sharia iliyoanzisha mamlaka hiyo pamoja na Sheria mbali mbali kwa lengo la kuimarisha utawala bora ambao ndio ajenda ya kitaifa kwa kuweka lengo kuu na malengo mahsusi na hatimae kujenga jamii isiyo na rushwa na maendeleo ya kiuchumi endelevu.

Aidha, mamlaka hii inafanya kazi zake kwa kufanya uchunguzi dhidi ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi, kufanya udhibiti, utafiti na kuzishauri taasisi za umma na binafsi juu ya namna bora ya kudhibiti mianya ya rushwa na uhujumu uchumi pamoja na kutoa elimu kwa umma juu ya athari za rushwa na uhujumu uchumi kwa lengo la kuishirikisha jamii katika kuzuia rushwa.

Kamati inaipongeza ZAECA kwa kupata Sheria mpya Nam. 5 ya Mwaka 2023 pamoja na Muundo mpya ambao utawasaidia kuweka sawa miongozo ya kazi zao.

Kamati inaipongeza ZAECA kwa mafanikio makubwa waliyoyapata katika Mikoa ya Kaskazini na Kusini Pemba ambapo imefanikiwa kukuza uelewa kwa wananchi kwa kutoa elimu jambo lililopelekea wananchi kutoa taarifa za vitendo vya rushwa vinavyotokea katika jamii zetu.

Kamati pia, katika kufanya udhibiti wa sehemu mbalimbali za makusanyo ya Mapato kwa upande wa Pemba imefanikiwa kuokoa jumla ya Tsh. 133,273,210/- pamoja na kutembelea miradi kumi na tano (15) ambayo ilibainika na mapungufu kadhaa na kuyatolea ushauri wa kuwataka wakandarasi kuzingatia vigezo vya miongozo ya ujenzi wakati wa utekelezaji wa ujenzi ili kupatikana thamani halisi ya fedha.

### ZIARA YA KAMATI KATIKA TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA (TAKUKURU)

Kamati ilipata nafasi ya kutembelea TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA (TAKUKURU) iliyopo Dodoma kwa kuambatana na watendaji wa MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI ZANZIBAR akiwemo Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ndugu Ali Abdalla Ali. Kwa pamoja tulifanikiwa kujifunza

mambo kadhaa huku tukielezwa kwamba Dira na Dhima ya Taasisi hiyo ni kuwa na Tanzania isiyokuwa na Rushwa.

Kwa upande mwengine ilipata kujua kuwa Takukuru inakabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo Uadilifu na Uwajibikaji wa Watendaji, Mtazamo mbaya wa Jamii kuhusu rushwa unaopelekea kukosa mashirikiano na Taasisi hiyo. Huku ikizungumzwa kiini cha rushwa kinatokana na uelewa mdogo na hali duni ya maisha kwa jamii ya wa Tanzania.

**Changamoto za Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu ya Uchumi Zanzibar**

Licha ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika mwaka huu, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), imekuwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Kamati imebaini ZAECA inakabiliwa na ugumu wa kubadili tabia na mitazamo ya wananchi juu ya rushwa na uhujumu uchumi;

*(ii)* Kamati imebaini uhaba wa vifaa vya kisasa vya utendaji kazi zao za kila siku ikiwemo vifaa vya uchunguzi unaoathiri Mamlaka licha ya jitihada kubwa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha inavipata vifaa hivyo.

*(iii)* Aidha, Kamati imegundua kuwa Mamlaka inakabiliwa na tatizo sugu la uhaba wa wataalamu katika fani tofauti jambo ambalo linarudisha nyuma maendeleo ya kazi zao.

*(iv)* Kamati imeelezwa Mamlaka inakabiliwa na ukosefu wa fedha ambazo hutumika kupatia taarifa zinazohusiana na masuala ya rushwa.

**Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati:**

*(i)* Kamati inashauri ZAECA kuendeleza zoezi la utoaji wa elimu kwa wananchi kupitia ngazi za masheha kwa kuwa wao ndio viongozi katika jamii juu ya kupata ufahamu wa Sheria ndogo ndogo;

*(ii)* Kamati inaishauri ofisi ya ZAECA kufanya uchunguzi wa miradi mbali mbali ili kupunguza ubadhirifu unaotokana na miradi mikubwa ya Serikali;

(iii) Kamati inaishauri mahusiano ya ZAECA na Taasisi za Haki yanadumishwa ili walengwa waliothibitika na kukamatwa kwa makosa ya dawa za kulevya wadhibitiwa kwa mujibu wa sheria.

(iv) Kamati inapendekeza ZAECA kusimamia upatikanaji wa vitendea kazi vya kisasa kwa kusihirikiana na Serikali juu ya umuhimu wa vifaa hivyo katika kuimarisha maendeleo ya uchumi wetu.

(v) Aidha, Kamati inaitaka ZAECA kuhakikisha wanajipanga ipasavyo kwa ajili ya kudhibiti utoaji na upokeaji wa rushwa katika vipindi vya uchaguzi na mifumo ya upatikanaji wa ajira;

(vi) Kamati inaishauri ZAECA kuharakisha uchunguzi wa mashauri wanayapeleka kwa haraka na kukamilika ili yaweze kupelekwa Kwa Muendesha Mashtaka ya Serikali na hatimae Mahakamani pindipo kosa likibainika.

## 5.9 TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni Taasisi iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria Nam. 4 ya Mwaka 2015 na imepewa mamlaka ya kusimamia maadili ya viongozi wa umma.

Tume kwa mwaka huu imeweza kupokea, kusajili na kuhifadhi Tamko la Mali na Madeni ya viongozi wa Umma, kufanya uhakiki wa taarifa za mali na Madeni ya Viongozi wa Umma, Kupokea na kufanya uchunguzi wa tuhuma na malalamiko ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kujenga uelewa kwa viongozi wa Umma na wananchi Unguja na Pemba kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili.

Kwa upande wa Pemba kamati imefarijika kuona Tume imetoa elimu kwa viongozi wa umma 341, juu ya masuala ya maadili ya viongozi, kwa lengo la kusimamia haki, uwajibikaji na nidhamu katika sehemu za kazi.

### ZIARA YA KAMATI KWA SEKRETSIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA – DODOMA TANZANIA BARA

Kamati ilibahatika kufanya ziara katika Sekriterieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kushirikiana na watendaji wa TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA Zanzibar kwa pamoja tunashukuru

kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kulifanikisha hilo, jambo ambalo limetupa muamko na ari ya kufanya kazi kama sisi viongozi kwa kuwa waadilifu na kufuata sheria za nchi bila kusahau wajibu wa kujaza fomu za Mali na Madeni kwa kila Mwaka.

**Changamoto za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

Kamati wakati wa ufatiliaji wa utekelezaji wa kazi zake imegundua bado zipo changamoto ambazo zinahitaji mikakati maalumu ya kuweza kuzitatua. Miongoni mwao nikama zifuatazo:

*(i)* Kamati imebaini Ofisi ya Tume inakabiliwa na upungufu wa baadhi ya vitendea kazi na vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya msingi.

*(ii)* Kamati imeelezwa kwamba Tume inakabiliwa na wakati mgumu wa utoaji wa elimu kwa wananchi, kufanya uchunguzi, usajili na uhakiki wa taarifa za viongozi kutokana na kukosekana kwa gari kwa ajili ya matumizi ya Ofisi. Aidha, Kamati haikuridhishwa na usafiri uliopo kwa ajili ya matumizi ya Katibu wa Tume kutokana na gari hiyo kuirithi kutoka Tume ya Kurekebisha Sheria inakipindi kirefu imelala haitumiki.

*(iii)* Kamati imegundua kuwa Ofisi inakabiliwa na upungufu wa vifaa vya usikilizaji wa mashauri ya malalamiko yanayowasilishwa mbele ya Tume kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi.

**Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati:**

*(i)* Kamati inaiomba Serikali kupitia Bajeti wanayoidhinishiwa Tume ya Maadili kuipatia kikamilifu fedha kwa mujibu wa matakwa yao ili waweze kupata mahitaji ya vifaa vya kutosha kwa ajili ya matumizi ya Ofisi za Unguja na Pemba.

*(ii)* Kamati inashauri Serikali kuwapatia gari kwa ajili ya matumizi ya kazi za ofisi pamoja na usafiri wa uhakika kwa shughuli za Katibu wa Tume.

*(iii)*Kamati inaishauri Tume kuendelea kutoa elimu kwa viongozi wa umma na wananchi kwa ujumla juu ya haki na wajibu katika kukuza na kulinda maadili yao.

## 5.10 IDARA YA URATIBU NA UENDESHAJI WA WIZARA

Idara ya Uratibu na uendeshaji wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora unatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Ofisi Kuu Pemba.

Idara ya Uratibu wa Mipango Sera na Utafiti imetekeleza shughuli zake ikiwemo kuratibu na kutayarisha Sheria ya Kufuta Kamati za Mapinduzi na kuanzisha Kamati ya Uongozi, kufanya vikao vya kupitia mikataba ya wazo linalohusu Programu ya Kupambana na Uhalifu unaohusiana na masuala ya fedha na makosa mengine ya jinai ya kupangwa pamoja na kukusanya taarifa za utafiti wa sababu zinazopelekea wananchi kuchelewa kurithi katika jamii kwa upande wa Unguja na Pemba.

## 5.11 OFISI KUU PEMBA

Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba inajukumu kuu la kusimamia na kuratibu shughuli zote za Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kisiwani Pemba.

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inapongeza sana juhudi za Ofisi kuu Pemba kwa kufanya ziara katika taasisi nane (8) za Pemba kwa lengo la kukumbushana kusimamia na kutekeleza wajibu wa kazi kwa kufuata misingi ya sharia na kanuni za utumishi wa umma pamoja na kupunguza malalamiko ya watumishi juu ya kudai stahiki zao. Aidha, Ofisi imefanikiwa kutoa mafunzo mtambuka kwa watumishi yenye lengo la kuelimisha masuala ya kupiga vita udhalilishaji katika jamii pamoja na vitendo vya rushwa.

Sambamba na hilo, Afisi kuu Pemba imefanikisha zoezi la kufanya ziara maalumu ya chuo cha mafunzo kwa kusikiliza changamoto za kisheria kwa wale wote walowekwa vizuizini kwa kushirikiana na Mahakama, DPP, ZAECA, Idara ya Utawala Bora na Idara ya Katiba na Msaada wa Sheria. Afisi pia imefanikiwa kufanya uhakiki wa watumishi na kuelekeza kupangwa kwa mujibu wa kada zao ili kuweza kuboresha utendaji kazi.

Vilevile, Ofisi imeratibu mkutano juu ya umuhimu wa kuwa na bima na vyombo vya moto, nyumba za kuishi sambamba na kuzifahamu sharia za bima pamoja na umuhimu wake kwa jamii.

### 5.12 IDARA YA KATIBA NA MSAADA WA KISHERIA

**Idara ya Msaada wa kisheria** imeanzishwa rasmi mwaka 2019 chini ya Sheria ya Msaada wa Kisheria Nam. 13 ya mwaka 2018 kwa lengo la kuratibu, kuendesha na kusimamia huduma za msaada wa kisheria. Aidha Idara hii ilibadilishwa jina na kuitwa Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria kupitia Toleo la Hati ya Kisheria Nam. 137 ya tarehe 24 Agosti, 2021.

Kamati imeridhishwa na mafanikio waliyopatikana ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa wataka huduma ya msaada wa kisheria Ofisini. Matunda ambayo yametokana na kurusha kipindi cha Baraza la Msaada wa kisheria kupitia ZBC. Aidha, Idara imeweza kuaminika katika jamii jambo ambalo limerahisisha upatikanaji wa huduma na haki kwa watu wasiojiweza hususan wanawake, watoto na makundi mbali mbali;

Sambamba na hilo, kupitia Jukwaa la jamii kwenye masuala ya kijinsia na kuripoti kesi za udhalilishaji kumepelekea kupatika namna bora ya utoaji msaada wa kisheria kuhusu masuala ya kesi za udhalilishaji.

**Changamoto za Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria**:

*(i)* Kamati haikuridhishwa kuona Ofisi hii inakabiliwa na uhaba wa watumishi katika Idara hali ambayo inakwamisha shughuli zao kutekelezeka ipasavyo;

*(ii)* Kamati imebaini tatizo la Kuchelewa kuingiziwa fedha za OC kwa wakati jambo linalorudisha nyuma utendaji wa kazi za Ofisi.

*(iii)* Kamati imegundua Idara hii inakabiliwa na Uhaba wa Mawakili wa kesi za kujitolea na hivyo jamii kukosa watu wa kuwasimamia na kuwaongoza namna ya kutatua migogoro yao;

*(iv)* Kamati wakati ikipokea taarifa ya utekelezaji za Idara hii imeelezwa kuwepo kwa Ukosefu wa vitendea kazi vya ofisi;

*(v)* Kamati imebaini tatizo la uhaba wa Ofisi ya kudumu kwa baadhi ya watoaji wa msaada wa kisheria na hivyo kulazimika kutumia ofisi za kuazima kwa muda.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

*(a)* Kamati inaishauri Serikali kujitahidi kuingiza fedha za matumizi mengineyo kwa wakati ili kuondosha uzorotaji wa kazi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu;

*(b)* Kamati inaishauri Serikali kusaidia kupatikana kwa washirika wa maendeleo na kukamislisha uandaaji wa Kanuni za Malipo ya Wakili na Vakili kwa lengo la kurahisha utekelezaji wake;

*(c)* Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kufanikisha baadhi ya vifaa vikiwemo printer, kompyuta na vishkwambia, hata hivyo inashauri kuwaongezea vifaa hivyo hasa ili kuweza kuletwa ufanisi wa kazi;

*(d)* Kamati inashauri Wizara kuharakisha upatikanaji wa Ofisi za kudumu kwa watoaji wa huduma za Msaada wa Kisherii ikiwa ni pamoja na kuwaomba Wakuu wa Mikoa kulipa kipaumbele suala hilo kwa kuliratibu katika ofisi za Mikoa.

## 5.13 MAHAKAMA KUU

Mahakama Kuu Zanzibar ni moja kati ya mihimili mitatu uliobeba dhima ya kutafsiri sheria na kusimamia upatikanaji wa haki katika ngazi mbali mbali unaotokana na kusikiliza kesi na kutoa uamuzi wa kesi zote zinazohusiana na masuala ya jinai na madai kufuatana na sheria za nchi.

Kamati inaipongeza Mahakama Kuu Zanzibar kwa kuweza kuratibu vikao mbali mbali vya ushirikiano wa wadau wa haki jinai vinavyopelekea kuharakisha mienendo ya mashauri ambayo vimejadili changamoto mbalimbali na kuzipatia ufumbuzi ikiwa ni sehemu ya kuimarisha usimamizi wa haki hizo.

Kamati pia imeridhishwa na vipindi mbali mbali ambavyo hurushwa kupitia Shirika la Utangazaji la ZBC ambavyo vilijadili mada mbali mbali yakiwemo masuala ya udhalilishaji, dawa za kulevya, mashauri ya madai, ushahidi wa kielektroniki, mashauri ya watoto na idhini katika Mahakama za Kadhi.

Kwa mwaka 2023/2024 Kamati inaipongeza Mahakama kwa kutekeleza mambo yafuatayo:

*(i)* Kufanikiwa kuitisha vikao vya wadau na kujadili masuala ya haki jinai;

*(ii)* Kuanza kutumika kwa Muundo Mpya wa Mahakama na kupelekea ufanisi wa shughuli za mahakama katika ngazi ya utawala na ile ya uendeshaji mashauri;

*(iii)* Kuimarika kwa usimamizi wa haki umekuwa na kasi na hivyo kupunguza idadi ya mashauri yaliyopo Mahakamani kwa muda mfupi; na

*(iv)* Kukua kwa ushirikiano wa wadau unaopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Mahakama.

**Changamoto za Mahkama Zanzibar**

Mbali ya kuwepo kwa mafanikio yaliyoelezwa hapo juu, Mahkama inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(a)* Kamati imebaini ukosefu wa sehemu ya kutunzia majalada kwa mashauri yaliyomalizika katika Mahakama za Mikoa, kwa madhumuni ya kuhifadhi na kuweka kumbukumbu vizuri na hata kurahisisha upatikanaji wake pale yanapohitajika kwa marejeo au kuwasilishwa mbele ya Mahkama za juu.

*(b)* Kamati imebaini adhabu zinazotolewa katika Mahakama za Watoto hazifiki kwa walengwa ili kujifunza badala yake kutengeneza wahalifu sugu baada ya kuizoea Mahakama kutokana na adhabu hizo kwenda kwa wazazi.

*(c)* Kamati imebaini kuwa katika Mahakama kuna ukosefu wa madaftari halisi ya kufungulia kesi "Case Register books" kwa mashauri ya jinai na madai kunasababisha kuwa na mfumo dhaifu wa kuweka kumbukumbu za mashauri yaliyofunguliwa na kusababisha ukosekanaji wa taarifa muhimu na zilizo sahihi kwa kesi zilizomalizika.

*(d)* Kamati imebaini upungufu wa vitendea kazi vya kutosha na upungufu wa wafanyakazi katika kada mbali mbali hususan kada ya Sheria;

*(e)* Kamati inasikitishwa na ufinyu wa bajeti unaopelekea upatikanaji mdogo wa fedha za mashahidi na uendeshaji wa kazi za ofisi;

*(f)* Kamati imegundua uchakavu mkubwa wa majengo ya Mahakama ambao umedumu kwa muda mrefu sasa hasa katika Mahakma za Wete, Kengeja, Mkoani, Konde na Mkokotoni; na

*(g)* Kamati imebaini uchakavu na ukosefu wa vyombo vya usafari kwa watumishi wa Mahakama katika ngazi mbali mbali kwa ajili ya kuendesha shughuli za ufuatiliaji wa kesi za Mahakama;

**Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati:**

*(a)* Kamati inashauri Mahakama kuongeza jitihada katika kusikiliza mashauri kwa wakati na kuwapatia wananchi mienendo ya kesi zao kwa muda mfupi zaidi.

*(b)* Kamati inashauri Serikali kuandaa sera ya masuala ya kutumikia adhabu jamii kwa watoto ambao wapo chini ya miaka 17 na watu wazima wenye vifungo vya chini ya mwaka mmoja.

*(c)* Kamati inapendekeza kwa Mahakama za watoto kuendelea kutoa adhabu ikiwa pamoja na kutoa amri za kurudi kuendelea na masomo kwa wale walioacha masomo na umri wao unaruhusu kurudi skuli.

*(d)* Kamati inashauri Mahakama kuanza kutumia kwa haraka madaftari mapya katika mwaka huu wa 2024 pamoja na kuyasimamia vyema kwa madhumuni ya kuondoa matatizo yaliyopo katika mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu za kesi zinazofunguliwa ambayo yatawezesha utaratibu wa ukusanyaji wa taarifa zinazohitajika kwa urahisi.

*(e)* Kamati inapendekeza Mahakama ziendelee kusimamia shughuli za ujenzi na kufanya matengenezo ya majengo ya Mahakama yaliyochakaa ili kurahisisha upatikanaji wa haki kwa wananchi.

*(f)* Kamati inatoa ushauri kwa watendaji wa Mahakama kupita katika shehia za vijijini na mijini kutoa elimu juu ya suala zima la uendeshaji wa kesi badala ya kusubiri kipindi cha Wiki ya Sheria;

*(g)* Kamati inaipongeza Mahakama kwa kumaliza baadhi ya mashauri kwa muda mfupi hata hivyo inaishauri kuongeza juhudi za uendeshaji wa mashauri yaweze kumalizika kwa haraka na kupunguza ongezeko la Mahabusu;

*(h)* Kamati inashauri Serikali kuwasaidia vyombo vya usafiri ili waweze kutekeleza na kufuatilia majukumu yao kwa ufanisi mkubwa;

*(i)* Kamati haikuridhisha na vifaa vinavyotumika kuhifadhia nyaraka kutokana na uchakavu wake hasa katika mahakama ya Wete na kushauri kutafutwa njia mbadala wa uhifadhi wa majalada hayo ili kuepusha upotevu unaoweza kufanyika kwa urahisi;

*(j)* Kamati inashauri Serikali kuandaa mradi kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Mahakama ili ziweze kujengwa kwa pamoja na baadae waweze kurudisha fedha hizo kidogo kidogo; na

*(k)* Kamati inashauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuupa umuhimu wa kipekee Muhimili wa Mahakama kwa kuwapatia fedha za kuagiza vyombo vya usafiri vyao wenyewe.

## 5.14 AFISI YA MWANASHERIA MKUU

Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 ndio Mshauri Mkuu wa Serikali kwa mambo yote ya Kisheria. Afisi inafanya shughuli mbali mbali za kisheria ikiwa pamoja na kutoa ushauri wa kisheria kwa Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali, Uandishi wa Miswada ya Sheria, Kusimamia Kesi na Mashauri ya Madai kwa niaba ya Serikali, Kuandaa Hati za Nyaraka za Kisheria, Kusimamia Mikataba yote ambayo Serikali ni sehemu ya Mikataba hiyo na kufanya mambo mengine ya Kisheria kwa niaba ya Serikali.

Katika kipindi hiki Kamati inaipongeza Afisi ya Mwanasheria Mkuu imeweza kufanikisha mambo yafuatayo:

*(i)* Afisi imeweza kukuza mashirikiano na Ofisi nyengine za umma jambo lililopelekea watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kupata mafunzo maalumu kuhusiana na kujenga uwezo katika masuala ya mikataba ya mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

*(ii)* Kufanyika kwa Kongamano la Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria kutoka katika Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa lengo la kujadili changamoto zinazoikabili sekta ya sheria.

(iii) Kuandaa miongozi ya kazi kwa ajili ya kutoa maelekezo ya namna bora ya utendaji kazi.

(iv) Kukumilika na kukabidhiwa kwa Muundo wa Afisi baada ya kuidhinishwa na Serikali kwa matumizi rasmi hali itayoiwezesha kuleta ufanisi wa Afisi na Taifa kwa ujumla.

**ZIARA YA KAMATI KATIKA OFISI YA MWANASHERIA MKUU – DODOMA**

Kwa upande wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Dodoma Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa kitaifa ikishirikiana na Watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar ilipata nafasi ya kusikiliza maelezo kuhusu Vitengo mbalimbali vya Afisi hiyo ikiwemo, Ushauri na Uratibu wa Kisheria Uandishi wa Sheria, ambapo *Drafter Mkuu* huteuliwa na Mheshimiwa Rais na pia ni Mualikwa wa kudumu wa Baraza la Mawaziri.

Kamati ilipata ilifahamu majukumu ya Kitengo cha Mawasiliano Serikalini ambacho kinashughulikia Mikataba inayofikishwa kwa ajili ya kufanyiwa upekuzi kwa mujibu wa Sheria yao ya Manunuzi ya Umma.

Kitengo hiki kinakabiliwa changamoto zifuatazo:

- Kupeleka barua za kufanyiwa kazi mikataba bila ya kuambatanisha Mikataba husika.
- Kusainiwa mikataba bila ya kupitishwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu.
- Kuwasilishwa kwa taarifa za mikataba kabla ya taratibu za zabuni kukamilika.

**Changamoto za Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Zanzibar**

Mbali ya kuwepo kwa mafanikio yaliyoelezwa hapo juu, Afisi ya Mwanasheria Mkuu inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(a) Uchache wa uingizwaji wa fedha za matumizi mengineyo (OC) hali inayosababisha kutokufanyika kwa baadhi ya shughuli zilizopangwa katika mpango kazi wa ofisi hiyo;

(b) Kuchelewa kuwasilisha kwa rasimu za mikataba kwa ajili ya kutolewa ushauri jambo linaloathiri utendaji kazi wa Afisi.

**Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati:**

*(a)* Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Wizara husika kuliangalia kwa karibu suala la matumizi ya fedha nyenginezo ili iweze kurahisisha utendaji kazi wa Afisi.

*(b)* Kamati inaishauri Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuandaa miongozo kwa taasisi zote zenye tabia ya kuchelewesha mikataba ili iweze kupunguza tatizo hilo.

## 5.15 AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar imeundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 56A cha Katiba ya Zanzibarya mwaka 1984 na kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria Namba 2 ya Mwaka 2010. Aidha, Afisi hii ina jukumu la kuendesha kesi za jinai kwa Mahakama Kuu hapa Zanzibar na Mahakama za Mikoa kuanzia tarehe 1 Julai 2019 kwa upande wa Pemba, pamoja na kuratibu uendeshaji wa mashtaka za Mahakama za Mwanzo kwa kufuata utaratibu uliowekwa kisheria.

Katika utekelezaji wa majukujmu yake Afisi hii pia, inapokea majalada ya uchunguzi ya makosa ya jinai kutoka vituo vya polisi na mamlaka ya kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar pamoja na Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya.

**ZIARA YA KAMATI KATIKA OFISI YA TAIFA MASHTAKA DODOMA**

Kwa upande wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Dodoma ambayo Kamati na Mwendesha Mashtaka Mkuu na Watendaji wa Ofisi ya Mkurugenzi Mashtaka pia ilipata fursa ya kwenda kutembelea na kujifunza ilielezwa majukumu ya Ofisi hii ni pamoja na kusimamia na kuendesha mashtaka ya jinai katika Mahakama zote isipokuwa mahakama za Mwanzo. Miongoni mwa kazi zao ni kukagua Magereza na Vituo vyote vya Polisi.

Katika kipindi hiki Kamati imebaini kwamba Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeweza kufanikisha mambo yafuatayo:

**Mafanikio ya Ofisi ya DPP**

katika uendeshaji wa shughuli zake, ofisi imepata mafanikio mbali mbali ikiwa ni pamoja na:

(a) Wananchi wamekuwa wakitoa mashirikiano mazuri kwa ofisi ikiwa ni pamoja na kutoa ushahidi mahkamani jambo lililopelekea baadhi ya kesi kuisha ndani miezi mitatu.

(b) Kuendelea kupunguza muda wa kukaa majalada ya uchunguzi Afisini kutoka siku 14 hadi siku mbili tu.

(c) Kuendelea na utaratibu wa kukutana na Mahakimu kabla na baada ya kuanza usikilizaji wa mashauri mahakamani kila siku.

(d) Kuimarika kwa mashirikiano pamoja na mafunzo kati ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Mamlaka za upelelezi pamoja na wadau wengine wa haki jinai.

(e) Kuanzisha utaratibu wa kukaa na mashahidi siku moja kabla ya kusikilizwa kesi Mahakamani.

(f) Kupungua kwa maombi ya kufutisha kesi hususan za udhalilishaji ambazo zimefunguliwa mahakamani;

(g) Kuwafuatilia na kukutana na zaidi ya wahanga 16 wa makosa ya udhalilshaji kwa lengo la kujua maendeleo yao baada ya kesi zao kumalizika mahakamani.

(h)Kufanya mafunzo kwa wanasheria kuhusiana na namna bora ya uendeshaji na usikilizaji wa kesi sambamba na utekelezaji wa mkakati wamageuzi katika uendeshaji wa kesi.

**Changamoto za Afisi ya Mkurugenzi wa Mashataka Zanzibar**

Pamoja na kuwepo kwa mafanikio yaliyoelezwa hapo juu, Afisi ya DPP inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(a)* Kamati imebaini tatizo la Mashahidi kutofika Mahakamani na kupelekea mashauri kuondoshwa hususan mashauri yanayohusu makosa ya udhalilishaji kuwakana;

*(b)* Kamati imeelezwa kwamba Afisi inakabiliwa na uhaba wa watendaji hasa wa kada ya sheria;

*(c)* Kamati imegundua uhaba na uchakavu wa gari za Afisi ambazo zinarudisha nyuma shughuli za ufuatiliaji.

*(d)* Kamati imeelezwa kwamba kuna uelewa mdogo wa wananchi juu ya umuhimu wa kutoa ushahidi Mahakamani.

*(e)* Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la ufinyu wa bajeti unaopelekea ofisi kutofikia malengo yake ililojipangia.

*(f)* Kamati imegundua kuwepo kwa uchache wa wafanya kazi, mfano waendesha mashtaka, Mtakwimu, IT na Katibu Muhtasi hasa upande wa Pemba.

*(g)* Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la vitendea kazi mfano uchache wa vyombo vya usafiri, *computers* na *printers.*

*(h)* Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya uchakavu wa majengo pamoja na ufinyu wa nafasi upande wa Pemba.

*(i)* Kamati imebaini Afisi ya DPP kutokuwa na Afisi katika Mkoa wa Kaskazini Pemba.

**Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati:**

*(a)* Kamati inashauri Afisi kushirikiana na taasisi zinazohusika kwa ajili ya kuendesha programu za kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kutoa ushahidi katika Mahakama ili kurahisha uendeshaji wa kesi za jinai;

*(b)* Kamati inashauri Serikali kuwapatia kibali cha kuajiri watendaji wapya wa kada za sheria kama utaratibu wa kujaza nafasi kwa kuomba watumishi kutoka katika taasisi nyengine umeshindikana;

*(c)* Kamati pia inaishauri Serikali kufuatilia kwa haraka Wizara ya Fedha changamoto ya usafiri na kulipatia ufumbuzi kwa kadri hali inavyoruhusu;

*(d)* Kamati inapendekeza kwa Serikali kuwapatia fedha wanazoziomba kupitia bajeti ya afisi ili waweze kufanya manunuzi ya vitendea kazi vya Afisi.

*(e)* Kamati inashauri Serikali kuisaidia Afisi iweze kutafuta jengo Wete kwa lengo la kuirudisha Afisi ya Kaskazini ilikuweza kwenda sambamba na malengo ya Serikali ya kusogeza huduma karibu na wananchi.

*(f)* Kamati inaishauri Serikali kuwaongezea fedha za matumizi mengineyo ili waweze kuzisimamia ufatiliaji wa kesi.

## 5.16 TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar ina jukumu la msingi la kufanya mapitio ya Sheria mbalimbli za Zanzibar ili kuzifanya Sheria hizo ziendane na wakati wa sasa na wa baadae na kufikiwa malengo ya

kutungwa kwake, ikiwemo kuakisi mabadiliko ya kisiasa, kijamii na kiuchumi.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 4 cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria namba 16 ya Mwaka 1986 ina uwezo wa kuondoa mambo yasiyotekelezeka na dosari katika Sheria ziliopo, kuzifuta Sheria zilizopitwa na wakati au zisizotumika, kuziweka sheria katika lugha rahisi na nyepesi ili ziweze kufahamika kwa urahisi, kuzishauri taasisi mbalimbali juu ya umuhimu wa kufanya mapitio ya Sheria na kutoa mapendekezo juu ya mapitio hayo, kuimarisha mashirikiano na wadau mbalimbali wa ndani na nje katika mapitio ya sheria pamoja na kufanya mijadala mbalimbali inayohusiana na mapitio ya sheria.

Aidha, Kamati imeridhika na kazi za mapitio ya sheria mbali mbali walizozifanyia utafiti kwa kipindi hiki cha mwaka 2023/2024

**Changamoto za Tume ya Kurekebisha Sheria:**

Palipo na mafanikio hapakosi changamoto hivyo Tume ya Kurekebisha Sheria inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(a)* Kamati imebaini kwa Tume ina upungufu wa watumishi kwa baadhi ya Divisheni na Vitengo kutokana na muundo mpya wa Tume.

*(b)* Kamati imebaini kwaba kuna tatizo la uelewa mdogo wa jamii kuhusu masuala ya Sheria pamoja na kutofahamika kwa Tume na majukumu yake kwa Jamii.

*(c)* Kamati imegundua uwepo kwa Sheria nyingi zenye mapungufu na zinazohitaji kufanyiwa mapitio.

*(d)* Kamati imefahamishwa kuwa Tume inakabiliwa na changamoto ya utumiaji wa mifumo kutokana na hitilafu zinazojitokeza wakati wa matumizi na mafunzo kwa baadhi ya watendaji katika kutumia mifumo hiyo.

*(e)* Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa upatikanaji wa fedha kwa mujibu wa mahitaji yanayokusudiwa.

*(f)* Kamati imeona Tume inakabiliwa na ufinyu wa nafasi kwa watendaji katika jengo la Vuga.

**Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati:**

(a) Kamati inashauri Tume kutoa mafunzo zaidi kwa wataalamu wa ICT waliomo ndani na nje ya Tume na kuhakikisha watendaji wa Tume wanatumia vifaa vya kisasa katika utendaji wa shughuli zao za kila siku ili kuondoa changamoto ya utumiaji wa mifumo.

(b) Kamati inaiomba Serikali kuipatia fedha kwa wakati na mujibu wa mahitaji yaliyoombwa.

(c) Kamati inaishauri Tume kuwapatia mafunzo ya ndani wafanyakazi ili kuongeza ueledi na ufanisi katika majukumu yao;

(d) Tume ya Kurekebisha Sheria tayari imeshachukua jitihada mbali mbali za kupatiwa watumishi ambao watajaza nafasi katika Idara, Vitengo na Divisheni kwa kupeleka maombi ya nafasi hizo katika mamlaka husika kutokana na utaalamu unaohitajika. Kamati inashauri Serikali kulisimamia suala hili la wataalamu ili liweze kukamilika kwa urahisi.

(e) Kamati inaipongeza Tume kwa kuendelea na uendeshaji wa programu mbali mbali za ushajihishaji wa masuala ya sheria pamoja na kuielezea jamii uwepo wa Tume na majukumu yake. Hata hivyo, inashauriwa elimu iendelee kutolewa kwa wananchi ili ufanisi wa kazi uweze kupatikana.

(f) Kamati inapendekeza kwa Serikali kufanya uharaka wa kurekebisha Sheria ambazo zimepitwa na wakati mara tu baada ya kufanyiwa utafiti na Tume ili nguvu za Tume hiyo zisiweze kupotea.

(g) Kamati inaishauri Serikali kuifanyia uharaka Sheria ya Ndoa na Talaka kwa kuwa suala la utafiti limeshafanyiwa kazi na Ripoti yake imekamilika.

(h) Kamati inaishauri Serikali kufanyia mapitio Sheria ya adhabu kwa kurekebisha vifungu ambavyo vinatoa adhabu kwa vijana ambao hukutwa na makosa wamefanya pamoja na watoto wakike kwa kuridhiana.

## 5.17 TAASISI YA SKULI YA SHERIA ZANZIBAR

Skuli ya Sheria Zanzibar imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria namba 13 ya mwaka 2019. Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 4(1) (a) Skuli imefanikiwa kuwapeleka wanafunzi wa kundi la pili katika mafunzo ya vitendo katika Taasisi mbali mbali za Serikali ikiwemo Mahakama Kuu

Zanzibar, Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na Sekta Binafsi.

Sambamba na hilo, Skuli imeweza kufanya mitihani na kukabidhi vyeti kwa wahitimu kumi na tano baada ya kuhitimu mafunzo ya uwakili kwa mwaka 2023 – 2024.

Kamti inaipongeza Skuli ya Sheria kwa kuweza kupata Muundo wao wa Utumishi na inaamini utawaongezea ufanisi wa kazi na kuwaengezea maslahi watendaji wao.

**Mafanikio ya Skuli ya Sheria:**

*(a)* Skuli imefanikiwa kufanya mapitio (Moderation) ya mitihani ya mwisho (final examinations) ya wanafunzi wa Skuli ya Sheria wa kundi la pili kwa mwaka wa masomo 2023 – 2024;

*(b)* Skuli imefanikiwa kutoa Mafunzo ya "Risk Management" kwa lengo la kuwajengea uwezo Wajumbe wa Baraza la Skuli ya Sheria Zanzibar;

*(c)* Skuli imefanikiwa kuwasilisha Ripoti ya kwanza ya kazi za ushauri elekezi ya mapitio ya Kanuni za Usimamizi wa Upelelezi, Uendeshaji na Usikilizaji wa Kesi za Udhalilishaji wa Wanawake, Wasichana na Watoto Zanzibar kwa Katibu Mkuu wa AR – KSUUB;

*(d)* Skuli pia, imefanikiwa kutoa mafunzo ya "kuskani" vitabu kwa ajili ya kuingizwa na kutumika katika Mfumo wa Maktaba Mtandao (E – Library).

**Changamoto za Skuli ya Sheria Zanzibar:**

Mbali ya kuwepo kwa mafanikio yaliyoelezwa hapo juu, Skuli ya Sheria inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(a) Kamati imeelezwa kwamba Skuli inakabiliwa na uhaba wa Raislimali Fedha na kupelekea ufinyu wa Bajeti;

(b) Kamati imegundua ufinyu wa nafasi ya Maktaba na uhaba wa vitabu vya kujifunzia katika maktaba ya Skuli iliyopo katika jengo la Ofisi za Kamisheni ya Utumishi;

(c) Kamati imebaini ukosefu wa jengo la kudumu la Ofisi za Skuli ya Sheria pamoja na samani za Maktaba Mtandao (E- learning) baada ya kutembelea ofisi hiyo katika eneo la "Michenzani Mall".

**Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati:**

*(a)* Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti ya Skuli ya Sheria kwa mujibu wa makisio yao wanayopeleka Wizara ya fedha ili Skuli hiyo iweze kujiendesha.;

*(b)* Serikali isimamie ujenzi wa jengo la kudumu la Skuli ya Sheria na Ofisi zao kwa haraka zaidi kwa kutafuta wafadhili ili kuepuka fedha nyingi wanazolipia kodi kwa ajili ya ofisi zao;

*(c)* Kamati inaiomba Serikali kuharakisha suala la usafiri kwa skuli ya Sheria ili iweze kurahisisha ufatiliaji wa kazi zao.

## 5.18 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA ZANZIBAR

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar ni miongoni mwa Taasisi za kidini ambazo zinafanya kazi kwa maslahi ya waumini wa Dini ya Kiislamu Zanzibar. Katika awamu hii ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Kamisheni imekuwa mstari wa mbele katika kusimamia na kukuza uchumi wa nchi tofauti na ilivyozoeleka kwa taasisi za kidini kushiriki katika masuala ya kukuza uchumi wa nchi.

Aidha, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hii kwa Unguja na Pemba kwa kipindi hiki na kuona jamii ina unga mkono juhudi za Kamisheni kutokana na kuitumia kila inapostahiki.

Kamati imeona mafanikio mbali mbali wakati ikipokea taarifa za utekelezaji wa kazi za kawaida na maendeleo ikiwemo:

- Uzinduzi wa Shughuli za Mfuko wa Hijja ambazo zimezinduliwa rasmi na Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mhe. Mwl. Haroun Ali Suleiman mwezi Oktoba 2023 wakati akipokea ripoti ya utekelezaji wa shughuli za Hijja kwa mwaka 2023.

- Uwekezaji kwa kutumia miamala ya fedha ya kiislamu kwa kupitia mfumo wa fedha wa kiislamu ni miongoni mwa mambo yaliyopewa kipaumbele na yanayoendelea kuzingatiwa na Kamisheni katika shughuli za utekelezaji wa miradi yake ya kimkakati.

**Changamoto za Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar**

Sambamba na mafanikio yaliyopatikana katika Ofisi hii, bado Kamisheni inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Kamati imebaini kupitwa na muda kwa Sheria Nam. 2 ya mwaka 2007, Sheria ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.

*(ii)* Kamati imebaini uchache wa wafanyakazi wenye fani zinazotakiwa kulingana na mahitaji na muundo.

*(iii)* Kamati imebaini uwepo wa maslahi madogo kwa watendaji ukilinganisha na unyeti, uzito, hatari, ugumu, ushawishi na dhima iliyopo katika majukumu ya watendaji waliowengi.

*(iv)* Kamati imegundua tatizo la jamii kutorithi kwa wakati au kutorithi kabisa kinyume na maamrisho ya Dini yetu ya Kiislamu ambapo hupelekea migogoro mingi ya mirathi katika jamii,

*(v)* Kamati imebaini uhaba na uchakavu wa vyombo vya usafiri kwa ofisi zote za Kamisheni ya Wakfu Unguja na Pemba;

*(vi)* Kamati imebaini kuwa familia nyingi hushindwa kuitumia Ofisi hii kwa lengo la kufanya mirathi kisheria na mambo mengine yanayohusika;

*(vii)* Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa watumishi wenye fani ya uchumi katika misingi ya Kiislamu,

*(viii)* Mfumo wa ZAN malipo kwa Kamisheni ya Wakfu unaathiri shughuli za matumizi ya Ofisi,

**Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati:**

*(i)* Kamati inasisitiza Kamisheni baada ya kupata kibali cha uajiri kujairi watendaji kulingana mahitaji halisi na yenye sifa

*(ii)* Kamisheni izidishe bidii katika kutoa elimu ya mirathi kwa jamii kupitia vyombo vya habari masheha na hotuba za miskitini.

*(iii)* Kamati inaishauri Kamisheni kusimamia ipasavyo na kuweka taarifa sahihi za mashamba ya Wakfu kwa Unguja na Pemba sambamba na kuzitambua mali zote za Wakfu ambazo kwa muda mrefu hazitumiki kisheria,

*(iv)* Kwa kuwa, maslahi ya watendaji yamezidi kushuka ikilinganishwa na mwaka uliopita. Hii ni baada ya Kamisheni kuondoshwa katika orodha ya taasisi zilizokuwa zikilipwa mshahara kupitia utaratibu wa mashirika. Hivyo, Kamati inashauri Wizara kulisimamia suala la maslahi ya watendaji wa Kamisheni ili utendaji kazi uzidi kuimarika.

*(v)* Kamati inaishauri Serikali kupitia Afisi ya Mwanansheria Mkuu kuwatambua wanasheria wa Kamisheni kama Mawakili wa Serikali ili kwenda sambamba na taasisi nyengine za umma ambazo zimekuwa na wanasheria wa kuzisaidia taasisi zao kusimamia haki na fursa zao. Aidha, Kamisheni inapaswa kufuatilia kwa ukaribu suala hili ambalo zaidi limeiathiri ofisi ya Pemba kiutendaji.

*(vi)* Kamati inahimiza kuajiri vijana wa kutosha wakiwemo wataalamu wa mirathi ili kuwawezesha kutoka hatua waliyosasa na kwenda hatua nyengine ya kiuzalishaji baada ya kupata wataalamu wa kiuchumi kutoka Serikalini.

*(vii)* Kamati inapendekeza kwa Serikali kuangalia Kamisheni ya Wakfu kwa njia iliyo bora ya utaratibu wa malipo ambao hautosumbua shughuli za utekelezaji wa Ofisi hiyo.

*(viii)* Kamati inaiomba Serikali kuharakisha marekebisho ya Sheria ili iweze kukidhi haja ya masuala yote ya mirathi na mambo mengine.

## 5.19 OFISI YA MUFTI MKUU ZANZIBAR

Ofisi ya Mufti Mkuu ni Taasisi ya Serikali inayofanya kazi chini ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora yenye jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli mbalimbali za dini ya kiislamu zinazohusu utatuzi wa migogoro ya kidini, ndoa, talaka pamoja na kutoa Fatwa za masuala tofauti yanayofikishwa ofisini kwa kupatiwa ufumbuzi. Pamoja na majukumu mengine Ofisi hii, inafanya kazi ya kupitia Programu ya Usimamizi wa mambo ya kiislamu kwa mujibu wa Sheria ya Mufti nam. 4 ya mwaka 2021.

Kwa upande wa Pemba Kamati imeelezwa kwamba Ofisi imefanikiwa kufanya ukaguzi na usajili wa Misikiti na Madrasa, kutoa vibali vya kuombea Misaada ya Ujenzi wa Misikiti na Madrasa. Aidha, Masuala mbali mbali yanayohusina na Mambo ya kidini, ikiwemo ndoa na talaka yamepelekwa na kufanyiwa kazi.

**Mafanikio ya Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar:**

*(a)* Ofisi imefanikiwa kuendelea kutoa elimu katika jamii kwa kutumia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii;

*(b)* Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendeleza ujenzi wa jengo la ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar hali ambayo itaondosha kabisa changamoto ya nafasi kwa ofisi hii;

*(c)* Kuimarika kwa mashirikiano baina ya Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar na Taasisi mbalimbali za kidini.

**Changamoto za Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar:**

Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa samani na vitendea kazi vya ofisi kama vile kompyuta, fotokopi na Printa na vyombo vya usafiri.

*(ii)* Kamati imebaini uwepo wa uhaba wa wafanyakazi ambao wataweza kufanikisha shughuli za ofisi kitaalamu.

*(iii)* Kamati imebaini kuwa Ofisi inakabiliwa na uhaba wa fedha za matumizi mengineyo ya uendeshaji sambamba na kukosekana kwa uhakika wa kupatikana fedha hizo;

**Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati:**

*(i)* Kamati inaipongeza Serikali kwa kuja na uamuzi wa kuendeleza ujenzi wa Ofisi ya Mufti iliyopo Mazizini baada ya kwenda kutembelea Ofisi hiyo, ambayo itasaidia kuondosha chanagamoto ya ukosefu wa nafasi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwaongezewa fedha za matumizi ya kawaida (OC) ili waweze kununua samani za Ofisi pindi jengo litakapomalizika.

*(ii)* Kamati inaishauri Serikali kuipatia Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar watendaji kwa njia ya uhamisho na kuwapatia kibali cha uajiri kwa nafasi mpya za wataalamu.

*(iii)* Kamati inashauri Serikali kulisimamia suala la upatikanaji wa gari kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kutokana na fedha kwa ajili ya gari hizo tayari zimeshalipwa kupitia bajeti ya mwaka 2022/2023.

*(iv)* Kamati inaishauri Serikali kuharakisha suala la upatikanaji wa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Pemba utayoipa hadhi sawa na ya ofisi ya Mufti Mkuu, Unguja.

*(v)* Kamati inaishauri Ofisi ya Mufti Mkuu kushirikiana na Ofisi za Kadhi kutatua migogoro ya ndoa na talaka inayopelekwa kwa ajili ya usuluhishi.

*(vi)* Kamati inaishauri Ofisi kuendelea na suala la ukaguzi wa vyuo vya Madrasa na kutovifumbia macho vitendo viovu ambavyo vimekuwa vikiendelea kwa baadhi ya walimu.

*(vii)* Kamati inashauri Ofisi kutafuta utaratibu wa mashekhe wanaofungisha ndoa kutoa elimu ya umuhimu wa kujisajili kisheria na kupatia vyeti katika Ofisi za Matukio ya kijamii.

*(viii)* Suala la Matumizi Mengineyo imekua ni kilio kwa kila taasisi, hivyo, Kamati inaiomba Wizara kuangalia uwezekano wa uhakika wa kupatikana fedha hizo kwa wakati unaohitajika.

## 5.20 CHUO CHA UTAWALA WA UMMA (IPA)

Chuo cha Utawala wa Umma kimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 1 ya mwaka 2007, ikiwa na jukumu la kuwaendeleza Watumishi wa Umma na Watumishi wa sekta binafsi kwa kuandaa Programu za mafunzo ya muda mrefu na mafunzo ya muda mfupi pamoja na kufanya tafiti na kutoa ushauri elekezi katika masuala yanayohusiana na usimamizi wa utawala wa umma na kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa jamii.

Kwa upande wa Pemba Kamati ilipata fursa ya kukagua kiwanja kipya cha Ujenzi wa Chuo cha IPA kilichopo eneo la Pujini. Aidha, imeelezwa chuo kimeendesha shughuli zake za kawaida kama vile kutoa mafunzo ya muda mrefu, mafunzo ya muda mfupi na kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wengi wa Taasisi mbali mbali za Serikali zaidi ya makadirio.

Kamati inawapongeza IPA kwa kupatiwa “SITE PLAN” ya eneo lake la kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Tawi lao, pamoja na kupata Hesabu Benki

(account number) ambayo itarahisisha upatikanaji wa fedha za matumizi kwa upande wa Pemba.

**ZIARA YA KAMATI KATIKA CHUO CHA UTUMISHI MAGOGONI – DSM**

Sambamba na hayo, kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ikiongozana na watendaji wa Wizara ya ORKSUUB pamoja Mkuu kilifika Chuo cha Menejmenti ya Utumishi wa Umma Tanzania Magogoni Dar- es Salaam huku ikielezwa chuo hicho kinakabiliwa na Uchakavu wa Miundombinu ya Kampas za kujifunzia, uhaba wa rasili mali fedha, uhaba wa miundombinu, uhaba wa vifaa vya kufundishia na kutendea kazi, huku chuo kikikabiliwa na gharama kubwa za uendeshaji.

Kamati ilipata fursa ya kuuliza masuala tofauti pamoja na kushauri kuwapatia mafunzo watumishi wanaotarajia kupanda vyeo kulingana na kada mbalimbali kwa upande wa Chuo cha Utumishi wa Umma (IPA).

**Changamoto za Chuo cha Utumishi wa Umma (IPA)**

Licha ya mafanikio ambayo Chuo kimeyafikia kwa mwaka huu, lakini bado zipo changamoto ambazo zinahitaji mikakati maalumu ya kuweza kuzitatua. Miongoni mwao nikama zifuatazo:

*(i)* Kamati imebaini kuwa chuo kinakabiliwa na tatizo la kukosa usafiri wa uhakika kwa upande wa Unguja na Pemba ambao unahitajika kwa uendeshaji wa chuo na wakati wa dharura za wafanyakazi na wanafunzi;

*(ii)* Kamati imebaini chuo kina ukosefu wa rasilimali fedha za kuendesha ofisi hali inayosababishwa na kukosekana kwa muhasibu ama mshika fedha wa kudhibiti fedha hizo kwa upande wa Pemba;

*(iii)* Kamati imegundua uchache wa wafanyakazi wa kudumu katika kada za taaluma za uhasibu, uchumi, teknolojia ya mawasiliano, maktaba, usimamizi wa rasilimali watu na utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka.

*(iv)* Kamati wakati ikifanya ziara katika chuo Tawi la Pemba imegundua uchache wa vitabu rejea katika Maktaba na hivyo kulazimika kutumia mfumo wa maktaba mtandao.

*(v)* Kamati imebaini uwepo wa madeni ya muda mrefu kwa baadhi ya Taasisi za Serikali ambazo hupeleka wafanyakazi wao kupata mafunzo ya awali baada ya uajiri.

**Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati:**

*(a)* Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kuwatafutia kiwanja chengine katika eneo la Pujini kwa ajili ya ujenzi wa Chuo kwa upande wa Pemba baada ya kile kiwanja cha Mfikiwa kushindikana kutokana na kasoro zilizojitokeza;

*(b)* Kamati inaishauri Serikali kuongeza kazi ya utafutaji wa wafanyakazi wa kudumu katika kila kada husika mara tu watakapopata kibali cha uajiri;

*(c)* Ili Chuo kuweza kukusanya mapato na kujiendesha kama taasisi ya elimu, Kamati inashauri wanafunzi ambao hawalipi ada ya masomo kuzuiliwa matokeo yao ya mitihani au kuzuiliwa vyeti vyao vya masomo mpaka watakapokamilisha malipo ya ada.

*(d)* Kamati inashauri Chuo kuongeza idadi ya vitabu rejea, kuendelea kuwahimiza wanafunzi kusoma kwa njia ya huduma ya Maktaba mtandao ambayo inawawezesha kupata vitabu mbali mbali, pamoja na kuwapatia "shelves" za kuwekea vitabu hivyo kwa Tawi la Pemba.

*(e)* Kamati inashauri Serikali kutafuta uwezekano wa kuandaa na kutolewa mapema mafunzo ya wastaafu ili waweze kujiandaa na hali hiyo.

*(f)* Kuhusiana na mafunzo katika ngazi za awali Kamati inashauri Serikali kuandaa utaratibu wa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wapya kabla ya kuanza safari yao ya ajira ili kujiepusha na tamaa za utajiri wa haraka mara tu baada ya kuingia kazini.

## 6. OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ina jukumu la kusimamia Sera, Sheria na Kanuni za Ofisi ili kuhakikisha kuwa inaweka mazingira mazuri ya kutoa huduma za kijamii na kiuchumi sambamba na kuimarisha ulinzi na usalama kwa wananchi na wageni wanaoingia na kutoka Zanzibar. Aidha, Ofisi hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli zinazotekelezwa na Taasisi zisizo za Kiserikali (NGO's) ambazo zinasaidia kupunguza umasikini na kukuza uchumi wa wananchi.

Dira ya Ofisi hii ni kuwa Taasisi imara katika kusimamia amani, usalama, usajili wa wakaazi na upatikanaji wa huduma karibu na wananchi.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inaundwa na Idara zifuatazo zilizo chini Katibu Mkuu:

*(a)* Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa.
*(b)* Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ.
*(c)* Tume ya Utumushi wa Idara Maalum za SMZ.
*(d)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
*(e)* Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
*(f)* Ofisi Kuu Pemba.

Aidha, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inasimamia Taasisi 11 zinazojitegemea kama zifuatavyo: -

*(a)* Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU),
*(b)* Chuo cha Mafunzo (MF),
*(c)* Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM),
*(d)* Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU),
*(e)* Kikosi cha Valantia (KVZ),
*(f)* Ofisi ya Mkoa wa Mjini Magharibi,
*(g)* Ofisi ya Mkoa wa Kusini Unguja,
*(h)* Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Unguja,
*(i)* Ofisi ya Mkoa wa Kusini Pemba,
*(j)* Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Pemba,
*(k)* Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2023/2024

imefanikiwa vyema katika kusimamia na kutekeleza sera na mipango mbali mbali ya Serikali kwa lengo la kuleta maendeleo.

## 6.1 JESHI LA KUJENGA UCHUMI *(JKU)* ZANZIBAR

Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar *(JKU)* limeanzishwa chini ya kifungu cha *121* cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka *1984* pamoja na Sheria Nam. *6* ya mwaka *2003*. Kwa mujibu wa Sheria, JKU imepewa jukumu la kutoa mafunzo kwa vijana katika nyanja za uzalishaji wa kilimo, mifugo na uvuvi. Vile vile, Idara hii imepewa jukumu la kuwafunza vijana ufundi, kazi za amali na uzalendo kwa ajili ya kuwafanya vijana hao waweze kujitegemea, kuitumikia na kuijenga nchi.

Aidha, Kamati imeridhishwa na utendaji wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) kwa namna wanavyotekeleza majukumu waliyopewa kwa mujibu wa sheria, na kuwaendeleza vijana kuwa na uzalendo na wenye kuleta tija kwa jamii. Idara hii pia, imefanikiwa kuondosha kabisa changamoto ya makaazi kwa askari wake na kuboresha kwa kiasi kikubwa mazingira ya vijana waliopo makambini.

Pia, Kamati imeridhishwa na juhudi za JKU katika kuimarisha majukumu ya uzalishaji mali kupitia sekta ya kilimo na mifugo katika Kambi mbali mbali ikiwemo Msaani, Upenja, Bambi Kim, Bambi Matola, Cheju, Dunga na Kama.

Kwa upande wa sekta ya ujenzi na miuondo mbinu; JKU ni Idara ambayo imekuwa mstari wa mbele katika kuimarisha huduma za ujenzi na miundombinu na imefanikiwa kujenga majengo mbali mbali ya ofisi zake na mahanga ya Askari. Aidha, kikosi hiki kimeaminiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwapa miradi mikubwa ya kimaendeleo ikiwemo ujenzi wa Soko la Mwanakwerekwe ambalo linajengwa chini ya ushirikiano mkubwa kutoka Wakala wa Majenzi Zanzibar (ZBA) kama Mshauri Elekezi. Aidha, JKU wamepewa miradi ya ujenzi wa skuli za Mkoa wa Mjini Magharibi.

Vile vile, JKU licha ya kutekeleza shughuli za kilimo na mifugo sasa imeanza kuingia katika harakati za uvuvi kwa kuanza na boti mbili ambazo zinatumika kupitia Kambi ya Chokocho Kisiwani Pemba.

Aidha, JKU kwa kiasi kikubwa imefanikiwa kukuza sekta ya elimu kwa kuimarisha miundombinu ya skuli pamoja na kudahili wananfunzi wanaojiunga masomo ya elimu ya sekondari kwa kila mwaka.

Sambamba na hayo, Kamati inatoa pongezi kwa Wakala wa Ulinzi wa JKU kwa juhudi zake wanazochukua katika kuimarisha suala la ulinzi na usalama kwa viongozi wetu hapa nchini, lakini pia kwa wananchi wenye kuhitaji ulinzi au huduma kutoka kwa wakala.

**Changamoto za Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) Zanzibar**

Katika utekelezaji wa kazi za JKU Zanzibar na kutimiza malengo yaliyoainishwa katika bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/2024, Kamati imebaini kuwa zipo baadhi ya changamoto zinazoikabili JKU kutofikia malengo yake kwa hatua inayoridhisha. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo: -

*(i)* Uhaba wa wataalamu katika sekta ya kilimo, mifugo, afya, vifaa vya kufanyia kazi na wahandisi.

*(ii)* Kuwepo kwa ubovu wa miundombinu ya barabara isiyo ridhisha katika Kambi mbali mbali. Kwa mfano, ubovu wa barabara ya kuelekea Kwa Pweza, kambi ya Chambani, kambi ya Makangale na Kambi ya Dunga.

*(iii)* Kuwepo kwa athari za kimazigira kutokana na mabadiliko ya tabianchi na jinsi yanavyoathiri shughuli za kilimo na kupunguza kasi ya uzalishaji wa chakula, mboga mboga na matunda.

*(iv)* Uhaba wa vyombo vya usafiri na vitendea kazi kwa ujumla. Hali hii inahusisha pia ukosefu wa matrekta na pembejeo nyengine za kilimo katika kambi zetu zote za uzalishaji.

*(v)* Wapiganaji wengi kutokupatiwa likizo zao za mwaka kwa wakati pamoja na kutolipwa fedha za likizo kama inavyoelekezwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake.

*(vi)* Ukosefu wa miradi ya umwagiliaji katika kilimo ambapo imesababisha maeneo makubwa ya kambi za JKU kutotumika kwa uzalishaji. Kamati imebaini kuwa sehemu kubwa ya Kambi ya Msaani Pemba haitumiki kwa shughuli za kilimo wala mifugo kutokana na ukosefu wa maji.

*(vii)* Ukosefu wa hatimiliki katika kambi za JKU; ambapo maeneo ya ardhi yanayotumiwa na JKU kwa baadhi ya Kambi kuchukualiwa na wananchi na kuyatumia kwa shughuli za kilimo kinyume na taratibu. Kamati imebaini eneo kubwa linaloizunguka kambi ya Chambani Pemba limechukuliwa na wananchi kinyume na taratibu jambo ambalo hofu ya Kamati ni baadae kusababisha mgogoro wa ardhi kati ya Jeshi na wananchi.

*(viii)* Aidha, Kamati imesikitishwa na kuona eneo kubwa la kilimo katika kambi ya Chambani halijatumika kwa kilimo na mifugo na hivyo, kuifanya kutofikia malengo kutokana kutumia wastani wa hekta 10 mpaka 15 tu kwa kilimo na kuacha zaidi ya hekta 500 ikiwa hazitumiki kwa kazi yoyote ya JKU.

*(ix)* Kuwepo kwa changamoto ya huduma za afya katika kambi za JKU kutokana na mgao mdogo wa dawa kutoka Serikalini na upungufu wa wafanyakazi katika kada ya afya.

*(x)* Uhaba wa fedha matumizi mengineyo na upungufu wa dawa za matumizi ya binadamu.

*(xi)* Kuwepo mkataba baina ya SMZ na Serikali ya Misri kuhusu uendelezaji wa sekta ya kilimo katika shamba la JKU Bambi Kim na kutofikia malengo yaliyokusudiwa katika makubaliano na hivyo kusababisha hasara kwa jeshi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa JKU Zanzibar**

*(i)* Kamati inashauri JKU kufuatilia kikamilifu upatikanaji wa wataalamu ambao watasaidia kutimiza malengo yao. Katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 JKU iandae mpango maalum wa watumishi (scheme of service) ambao utasaidia kujua mahitaji yote wa wataalamu wanaohitajika kuanzia makao makuu mpaka ngazi za chini.

*(ii)* Kamati pia, inashauri JKU kuandaa miradi ambayo itasaidia kupunguza changamoto za mabadiliko ya tabianchi kwa kupata visima vya kisasa vyenye maji ya kutosha kwa lengo la kuimarisha kilimo na ufugaji. Aidha, Kamati inaitaka Idara hii kuhakikisha wanatumia vyema wataalamu wake kufanya tafiti na kubaini ni mazao na mifugo ya aina gani inahitajika kwa kila kambi badala ya kufanya shuhguli hizo kwa mazoea.

*(iii)* Kamati pia, inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuisadia JKU kuandaa sera ya muda mrefu ambayo italenga kuboresha kazi za uzalishaji na kukuza uwezo wa ubunifu kwa vijana wanaojitolea kwa kuwashirikisha washirika mbali mbali wa maendeleo kutoka Zanzibar na Tanzania Bara.

*(iv)* Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya samani katika mahanga ya askari wetu; hivyo, Kamati inashauri JKU kuhakikisha wametafuta njia mbadala itayosaidia upatikanaji wa samani katika mahanga yaliyojengwa ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha mazingira ya askari wetu.

*(v)* Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kufuatilia kwa karibu changamoto ya maeneo yanayokaliwa na raia sambamba na maeneo yanayutomika kwa shughuli za kilimo kinyume na taratibu katika Kambi ya Chambani na kulisadia Jeshi kuyarejesha maeneo hayo bila ya kuwepo kwa migogoro na wananchi.

*(vi)* Kamati inashauri Serikali kusaidia nguvu za JKU kwa kuwapatia vyombo vya usafiri au kuandaa mazingira ambayo yatawasaidia kupata vyombo vya usafiri kupitia mapato yake ya ndani.

*(vii)* Kamati pia, imeridhishwa na kazi za ujenzi zinazofanywa na JKU katika soko la Mwanakwerekwe hivyo, Kamati inashauri ujenzi huu kukamilika kwa wakati na kuzingatia viwango vya ubora ili kupata nafasi ya kutekeleza miradi mengine inayofuata.

*(viii)* Kamati inaipongeza zoni ya JKU Pemba kwa kuanzisha shughuli za uvuvi katika Kambi ya Chokocho. Kamati inashauri shughuli hizi zifanyike kwa kuzingatia weledi na utaalamu mkubwa wa uvuvi ili iwe ni kichocheo cha maendeleo ya kikosi.

*(ix)* Kamati inashauri Wizara kuupitia upya mkataba huo na kuangalia maslahi ya nchi na JKU kwani mkataba huu umeisha muda wake na haujawahi kufanyiwa mapitio.

*(x)* Kamati haijaridhishwa na biashara ya uzalishaji na uuzaji wa miwa kwa JKU, hivyo tunaomba Serikali kuangalia makubaliano kati ya mnunuzi na muuzaji kwa manufaa ya pande zote mbili.

*(xi)* Kamati inaishauri Serikali kusimamia upatikanaji wa dawa na uimarishaji wa huduma za afya katika kambi za JKU hususan Makao Makuu Saateni na Wawi kwa zoni ya Pemba sambamba na kuboreshwa kwa huduma za maji safi na salama katika vituo vya afya.

*(xii)* Aidha, Kamati inaishauri JKU kuanzisha skuli nyengine mpya ya sekondari katika kambi ya Kama au Upenja ili kuongeza kasi ya usajili wa wanafunzi na kuendelea kutoa elimu yenye ubora kwa wananchi.

*(xiii)* Kamati inaiomba Serikali kuwapatia JKU fedha za matumizi kwa wakati na kwa namna walivyoidhinishiwa katika bajeti yao ili waweze kutekeleza majukmu yao kwa ufanisi zaidi.

## 6.2 WAKALA WA ULINZI WA JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Wakala wa Ulinzi JKU ni Taasisi ya uzalishaji mali inayotoa huduma ya Ulinzi kibiashara kwa Taasisi za Serikali na watu binafsi, Jumuiya na wawekezaji waliopo Zanzibar kwa lengo la kuwekeza. Wakala imeanzishwa kwa agizo la Mheshimiwa Rais wa awamu ya saba (7) Dr. Ali Moh'd Shein kwa Mujibu wa Sheria Namba 2 ya Mwaka 2015.

### Changamoto za Wakala wa Ulinzi wa JKU Zanzibar

Katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku Wakala inakabiliwa na changamoto ndogo ndogo ambazo Kamati imezibaini na zinafaa kuchukuliwa hatua. Changamoto zenyewe ni kama zifuatavyo:

*(a)* Ufinyu wa nafasi za ofisi ya Wakala;
*(b)* Kuchelewa kuondoka walinzi Makao Makuu siku zenye vikao jambo ambao huleta usumbufu kwa wateja;
*(c)* Uchakavu wa magari yanayowapeleka walinzi vituoni;
*(d)* Kukosekana kwa gari la dharura lenye viashiria juu;
*(e)* Kukosekana kwa askari wa akiba wa wakala wa ulinzi;

### Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Wakala wa Ulinzi

*(i)* Kamati inashauri Wakala kuingizwa katika Programu za miradi ya maendeleo ili kuweza kupatiwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi zake.

*(ii)* Kamati inashauri Serikali kutafuta utaratibu mzuri wa kuwapatia mafunzo askari wake kila inapohitajika kwa lengo la kuondosha migogoro inayojitokeza baina ya walinzi na wapewa huduma.

*(iii)* Kamati inaishauri Serikali kununua vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuboresha kazi za Wakala.

## 6.3 CHUO CHA MAFUNZO (MF) ZANZIBAR

Chuo cha Mafunzo *(MF)* Zanzibar ni miongoni mwa Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 121 cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 na imeundwa chini ya Sheria Nam. *1* ya mwaka *1980* na Sheria Nam. *3* ya marekebisho ya mwaka *2007*. Idara hii ina jukumu kubwa la kuwapokea wale wote wanaoletwa Chuo cha Mafunzo kwa mujibu wa Sheria, kuwalinda pamoja na kuwarekebisha tabia ili wanaporudi katika jamii wawe raia wema.

Katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2023/2024 Chuo Cha Mafunzo Zanzibar kimepanga kutekeleza programu kuu mbili ambazo ni programu kuu ya Urekebishaji Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo na programu kuu ya Utawala na Uendeshaji ambapo lengo kuu ni kuimarisha taaluma za urekebishaji wa wananfunzi wa Chuo Cha Mafunzo kuwa raiya wema wanaporudi katika jamii.

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeridhishwa na utendaji kazi wa Chuo Cha Mafunzo Zanzibar kutokana na hatua kubwa waliyofikia katika kuwajengea uwezo wanafunzi katika stadi mbali mbali za maisha. Aidha, ujenzi wa gereza jipya kambi ya Kangagani na kukamilika kwa jengo la Makao Makuu Wete ni dhahiri kuwa Idara hii imedhamiria kuleta mabadiliko makubwa katika kukuza na kuendeleza utawala bora.

Aidha, Kamati inawapongeza Chuo cha Mafunzo katika mradi mkubwa wa ujenzi soko la Jumbi Wilaya ya Magharibi B kwa ushirikiano na Wakala wa Ujenzi Zanzibar.

**Changamoto za Chuo cha Mafunzo Zanzibar**

Kwa kuwa mafanikio makubwa na mazuri yamepatikana katika utekelezaji wa majukumu yake, hata hivyo, Chuo cha Mafunzo Zanzibar kimekabiliwa na Changamoto zifuatazo: -

*(i)* Uhaba wa fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo na fedha za kuendesha kazi za maendeleo kama vile uchimbaji wa visima kwa ajili ya umwagiliaji na ununuzi wa pembejeo za kilimo.

*(ii)* Mabadiliko ya hali ya hewa ambayo yamepelekea baadhi ya mazao kuharibika na mengine kufa kabisa katika vituo mbali mbali vya uzalishaji.

*(iii)* Kuwepo kwa uchakavu na upungufu wa vitendea kazi kama vile magari ya kuwabebea wanafunzi wanapotaka kwenda Mahakamani, samani zinazotumika vituoni na vifaa vya kilimo.

*(iv)* Kuwepo kwa ukosefu wa miundombinu ya umwagiliaji kama vile visima, mashine za maji na paipu za drip hali inayopelekea kuzorota kwa shughuli za kilimo na kukosa mavuno bora.

*(v)* Kuwepo kwa upungufu wa wataalamu wa kilimo na mifugo ambapo kwa sasa wataalamu waliopo ni wachache na hawatoshelezi kabisa katika mahitaji ya Idara.

*(vi)* Upungufu wa vifaa tiba hasa vya uchunguzi wa afya za binadamu ni tatizo kubwa kwa upande wa huduma za afya na zaidi katika vituo vya Kangagani, Wete na Hanyegwamchana.

*(vii)* Uchakavu wa gereza la Wete sambamba na miundombinu iliyopitwa na wakati katika magereza mbali mbali ikiwemo gereza kuu la Kiinua Miguu, Zanzibar

*(viii)* Vile vile, kuwepo kwa mrundikano mkubwa wa mahabusu katika gereza la Kiinua Miguu pia changamoto katika shughuli za Chuo kutokana na kuongeza kwa gharama za uendeshaji na ulishaji.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Chuo cha Mafunzo Zanzibar:**

Katika kukabiliana na changamoto hizo Kamati inashauri yafuatayo:

*(i)* Serikali iweke mkazo katika kuwapatia Chuo cha Mafunzo fedha za matumizi ili kuweza kutoa huduma kwa mahabusu na wanafunzi waliopo magerezani sambamba na kusaidia kuongeza kasi ya kuibua miradi mipya ambayo itapunguza changamoto ya fedha.

*(ii)* Kamati inashauri Serikali kufanya utaratibu wa kulihamisha gereza la Kiinua Miguu na kulipeleka Hanyegwamchana kutokana na uchakavu mkubwa na ukongwe wa gereza hili. Aidha, Kamati inashauri kutumiwa Chuo cha Hanyegwamchana kama gereza kuu la Zanzibar kwa kupatiwa miundombinu yenye kukidhi vigezo vya kisasa vya gereza.

*(iii)* Kamati inashauri Chuo kujikita katika kilimo cha umwagiliaji ili kuweza kulima katika muda wote wa mwaka na kuongeza kiwango cha uzalishaji.

*(iv)* Kamati inashauri Chuo kufanya ununuzi wa vifaa vya matumizi ya ofisi pamoja na pembejeo za kilimo kwa awamu kwa namna hali ya fedha itakavyoruhusu.

*(v)* Kamati pia, inashauri Serikali kutumia utaratibu uliopo wa mgao wa magari na kuwapatia Chuo cha Mafunzo kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa mahabusu na wananfunzi ambao ndio msingi wa shughuli zao kwa mujibu wa sheria.

*(vi)* Kamati inashauri Chuo cha Mafunzo kuwapatia mafunzo watumishi wake ili kwenda sambamba na mabadiliko ya kiuchumi na kimaendeleo.

*(vii)* Aidha, Kamati inaishauri Chuo Cha Mafunzo kuzidi kusimamia wanafunzi kujifunza stadi za maisha na kuhakikisha baada ya kurudi katika jamii wawe ni nyenzo muhimu katika kukuza maendeleo ya jamii.

*(viii)* Kamati inashauri kuchukuliwa hatua za mara kwa mara katika kuyatembelea magereza ya watoto na kujua maendeleo yao pamoja kuhakikisha kesi za watoto zinapungua kwa kujenga mashirikiano mema kati ya Wazazi, Mahakama na Chuo cha Mafunzo.

(ix) Aidha, Kamati inashauri Serikali kuielimisha jamii juu ya malezi bora ya watoto kwa kupunguza mashauri yanayofunguliwa dhidi ya watoto pamoja na kuifanya jamii kuwa na watoto bora wenye kufuata mila na desturi za kizanzibari.

## 6.4 KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo *(KMKM)* ni miongoni mwa Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 121 cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 na kimeundwa chini ya Sheria Nam. *1* ya mwaka *2003* ambapo kina majukumu ya kulinda usalama wa bahari ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, kuzuia njia zote zinazoweza kutumika kupitishia magendo, kusaidia vyombo vya baharini vya abiria na kufanya uokozi baharini pamoja na kushirikiana na Jeshi la Wananchi pale itakapotakiwa kufanya hivyo katika kuilinda mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kikosi cha KMKM kimefanikiwa kuimarisha shughuli za Ulinzi wa Bahari na nchi kavu kwa kufanya doria mbali mbali na kufanikiwa kukamata baadhi ya mali za magendo katika juhudi za kupambana na uhujumu wa uchumi.

Aidha, KMKM wamefanikiwa kuimarisha makaazi kwa Maafisa na Wapiganaji wake wa Unguja na Pemba katika hatua ambayo Kamati inapongeza sana juhudi za Serikali kwa kuimarisha makaazi ya Askari hawa pamoja na ujenzi wa jengo jipya la ghorofa kwa ajili ya ofisi kuu Wete, Kamandi ya Pemba.

Sambamba na hayo, Kamati imeridhika na namna kikosi hiki kilivyofanikiwa katika kutoa huduma bora za afya kwa askari wake pamoja na raia wanaoishi karibu na kambi zake. Aidha, pongezi za pekee ziende kwa uongozi wa KMKM Makamo Makuu kwa kuimarisha huduma za afya katika Hospitali ya Kibweni kwa kuweka madaktari bingwa wa magonjwa mbali mbali pamoja na uwepo wa vipimo vya kisasa na vifaa tiba vyenye kuridhisha kwa huduma za binadamu.

### Changamoto za Kikosi cha KMKM Zanzibar

Kama tunavyofahamu kuwa kuimarika kwa amani, usalama na utuivu wa nchi yetu umetokana na juhudi za Idara Maalum katika kuisimamia

na kuilinda ili nchi iweze kutekeleza harakati zake za maendeleo. Licha ya mafanikio mbali mbali ambayo Kamati imeyaona pamoja na mikakati ambayo inatumika katika utekelezaji wa majukumu yao.

Kamati imebaini kuwa KMKM inakabiliwa na changamoto zifutazo:

*(i)* Uhaba wa vyombo vya usafiri kwa Kambi zote za KMKM Unguja na Pemba jambo ambalo linakwaza kufanyika kwa doria za nchi kavu.
*(ii)* Uhaba wa wataalamu katika fani za afya, uchumi wa buluu, usanifu wa majengo na mawasiliano.
*(iii)* Ubovu wa miundombinu ya barabara za kuingilia Kambini pamoja na muingiliano wa shughuli za Kikosi na wananchi hususan katika sehemu za visiwa vidogo vidogo kama vile Kisiwa Panza, Fundo na Kojani.
*(iv)* Kutekeleza miradi mingi kwa wakati mmoja pia kunapelekea baadhi ya miradi kutofanyika kwa ubora na kutokamilika kwa wakati kwa mfano mradi wa uvuvi wa bahari kuu na mradi wa ufugaji matango bahari.
*(v)* Uhaba wa masoko ya uhakika kwa bidhaa zinzozalishwa katika kiwanda cha boti cha Bububu licha ya bidhaa zao kuwa bora na za kisasa zaidi.
*(vi)* Kutokamilika kwa miradi ya ujenzi nyumba za askari na mahanga ambapo ujenzi wake ulinaza katika Serikali ya awamu ya saba. Kwa mfano kambi ya kisiwa cha Fundo na Kisiwa Panza Pemba zimeachwa bila muendelezo wowote sambamba na kutumika kwa kambi hizo kwa shughuli za kikosi.
*(vii)* Kamati pia imebaini kuwa mgao wa mafuta wanaopewa KMKM katika kuendeleza doria zake za baharini ni mdogo na haukidhi mahitaji yao.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa KMKM**

*(i)* Kamati inashauri kikosi kuzidisha bidii katika operesheni za baharini na nchi kavu ili kukabiliana na vitendo vya uhujumu uchumi.
*(ii)* Kamati inashauri kikosi kwa kushirikiana na Wizara yake kutafuta wataalamu ambao watasaidia kuboresha sekta za Uchumi wa Buluu, Uhandisi Majengo pamoja na wataalamu wa Afya ili kufanya kikosi kuwa na nguvu na chenye kujitegemea zaidi.
*(iii)* Kamati pia, inaishauri Serikali kusimamia matengenezo ya barabara za ndani ambazo zinatumiwa na Kikosi ili kupunguza changamoto ya miundombunu ya barabara.
*(iv)* Kamati inashauri Kikosi kuandaa miradi na kutekeleza miradi hiyo kutokana na uwezo wake wa kitaalamu na rasiliamali watu ili kuikamilisha kwa wakati na yenye kuleta tija cha Serikali.

*(v)* Aidha, Kikosi kinashauriwa kuzidisha kasi ya kutoa mafunzo ya ubaharia kwa askari wake kwa ajili ya kuwaweka katika mazingira bora ya kazi ambazo kwa aslimia kubwa zinategemea bahari.

*(vi)* Kamati inaishauri Serikali kuboresha kiwanda cha boti (fibre boat) cha KMKM kilichopo Bububu kwa kuhamasiha taasisi zake kununua bidhaa kupitia kiwanda hiki pamoja na kuwajengea mazingira bora ya uzalishaji.

*(vii)* Vile vile, Serikali kupitia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi iongeze kasi ya mashirikiano na KMKM kwa kuwapatia wataalamu na vifaa ambavyo vitaongeza kasi ya uzalishaji kwa mazao ya baharini.

*(viii)* Kamati pia, inaishauri Serikali kuongeza mgao wa mafuta na kuweka fungu maalumu kwa ajili ya mafuta ya doria za baharini na nchi kavu.

*(ix)* Mwisho, Kamati inaishauri Serikali kusimamia ukamilishaji wa mradi wa ujenzi wa Kambi ya Fundo na Kambi ya Kisiwa Panza kutokana na kusimama kwa muda mrefu bila kuainshwa mbele ya Kamati sababu za msingi za kutokamilika mkwa ujenzi huo.

## 6.5 KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU) ZANZIBAR

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi *(KZU)* Zanzibar kimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Nam. 7 ya mwaka *1999* na kina jukumu la kusimamia shughuli zote za uzimaji moto na uokozi wa maisha na mali za watu, kusimamia na kuhakikisha kuwa huduma za zimamoto kwenye Viwanja vya Ndege na Bandarini zinakwenda sambamba kulingana na masharti ya Kitaifa na Kimataifa. Aidha, Kamati ilifanikiwa kutembela na kukagua maeneo mbali mbali ya Kikosi hiki na kujionea baadhi ya shughuli zake ambazo zilipangwa katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa mwaka 2023/2024.

**Mafanikio ya utekelezaji wa shughuli za Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, Zanzibar**

*(a)* Kufanikiwa kutoa huduma za kiusalama kwa ndege zinazotua na kuruka katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Abeid Amani Karume Kiembesamaki na uwanja wa ndege wa Karume Pemba pamoja na kiwanja kidogo cha ndege cha Nungwi.

*(b)* Aidha, Kikosi kimetoa huduma kama hizo za kiusalama katika bandari za Zanzibar ikiwemo bandari ya Malindi, bandari ya Mkoani na bandari ya Wete.

*(c)* Kufanikiwa kutoa huduma katika matukio yote ya ajali za moto na ajali nyengine na kuokoa maisha ya watu na mali zao kwa kushirikiana na raia wema waliokuwa karibu ya matukio.

*(d)* Kikosi kimeendelea kutoa elimu kwa taasisi za kiserikali na binafsi juu ya majanga ya moto na jinsi ya kujikinga.
*(e)* Kikosi kimeendelea kufanya ukaguzi katika taasisi mbalimbali za Serikali na Taasisi binafsi na kuona jinsi zilivyojipanga kukabiliana na hali za dharura za majanga ya moto.
*(f)* Katika kuboresha mazingira ya kazi, Kikosi kimeanzisha ujenzi wa jengo la ofisi katika eneo la Mahonda na kufikia katika hatua nzuri.
*(g)* Aidha, kikosi kimefanikiwa kujenga jengo moja la ofisi na maegesho ya gari la kuzimia moto katika kituo cha Mahonda.

**Changamoto za Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar**

Pamoja na mafanikio ya kikosi hiki bado kuna changamoto kadhaa zinazowakabili ambazo zimekuwa ni endelevu kutokana na hali inavyokwenda siku hadi siku, miongoni mwa changamoto hizo ni hizi zifuatazo:

*(i)* Uhaba wa magari ya kuzimia moto na vifaa vya kisasa katika vituo vya Wilaya.
*(ii)* Uchakavu wa gari la kubebea wagonjwa katika kiwanja cha ndege cha Pemba.
*(iii)* Kamati pia, imebaini kuwepo kwa tatizo la jamii kuchelewa kutoa taarifa kwa wakati linapotokea janga la moto katika makaazi ya watu.
*(iv)* Kamati imebaini kuwepo kwa uchache wa vituo vya kuzimia moto hali inayopelekea ugumu wa kufika eneo la tukio na kuchelewa kwa waokozi kutokana ujenzi holela usiofuata mipango miji.

**Maoni na Ushauri na Kamati**

*(a)* Kamati inashauri Serikali kuimarisha mpango wa kuboresha vifaa vya zimamoto na uokozi ikiwemo kununua magari ya kisasa, nguo za kuzimia moto na vifaa vyengine ambavyo vitaimarisha mazingira za kazi zao.
*(b)* Kamati inashauri kikosi kuongeza nguvu katika ujenzi wa vituo vya zimamto na uokozi katika maeneo ya mashamba na maeneo ya bandari ndogo ndogo.
*(c)* Kamati inakishauri kikosi kufanya ukarabati wa magari yake mara kwa mara ili kuwasaidia katika kazi zao za kila siku.

*(d)* Kamati inashauri kikosi kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa taasisi za umma na zile binafsi ili kupunguza upotevu wa maisha na mali za wananchi.

*(e)* Maafisa wa kikosi wapatiwe mafunzo ya kitaalamu mara kwa mara ili kupambana na majanga haya na kuepusha kutumia njia za kienyeji katika kufanya uokozi ili kunusuru maisha ya watu.

*(f)* Kamati inashauri kikosi kulinda na kuboresha maslahi ya askari wake kwa kuwapatia haki na fursa zote za msingi kwa kwa wakati na kwa lengo la kuimarisha mazingira ya kazi.

*(g)* Kamati inashauri KZU kwa kushirikiana na Kamisheni ya Maafa Zanzibar kufanya utafiti wa maafa yanayotokea mara kwa mara katika taasisi za umma.

*(h)* Kamati pia, inaishauri Serikali kufanya utaratibu wa kuwapatia mafuta KZU nje ya Matumizi Mengineyo kwa lengo la kuweka uhakika wa kazi zao.

## 6.6 KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ)

Serikali iliamua kuanzisha Kikosi cha Valantia Zanzibar *(KVZ)* kwa mujibu wa Sheria Nam. *5* ya mwaka *2004* na kukipa majukumu ya kuweka amani na utulivu nchini, kupambana na janga lolote litakaloikumba jamii, kulinda viongozi na mali za Serikali pamoja na kufanya kazi za kijeshi kwa madhumuni ya kuzuia hali inayohatarisha ulinzi na usalama nchi yetu.

Kwa upande wa huduma za ulinzi na usalama wa raia KVZ wamefanikiwa kuimarisha doria za ulinzi na usalama kwa maeneo ya mijini, kuimarisha ulinzi katika vituo mbali mbali zikiwemo nyumba za viongozi na taasisi za umma, sambamba na kuwasaidia wananchi kuendelea na shughuli zao za uchumi na kijamii kwa amani na utulivu.

Pia, Kikosi kinaendelea na mradi wa ujenzi wa mahanga, nyumba za maafisa na ofisi katika maeneo ya Pangatupu, Mto wa Maji, Mwanyanya, Kikungwi na Muyuni kwa Unguja na Pujini kwa upande wa Pemba.

Aidha, Kamati imeridhishwa na maendeleo ya mradi huu na kuwataka viongozi wake kuzidi kusimamia miradi hii ili ikamilike kwa wakati. Ni imani ya Kamati kwamba kukamilika kwa mradi huu kutaondosha kabisa changamoto ya makaazi ya askari katika kambi zao pamoja na kuwepo ofisi mpya na za kisasa.

Kamati pia, inaipongeza Serikali kwa kuwaamini KVZ na kuwapa mradi wa ujenzi wa Ofisi za Masheha kwa Unguja na Pemba ambapo kazi za ujenzi zitaanza hivi karibuni.

**Changamoto za Kikosi Cha Valantia Zanzibar**

Licha ya mafanikio makubwa yaliyofikiwa na Kikosi cha Valantia Zanzibar, pia kikosi hiki kinakabiliwa na changamoto mbali mbali ambazo katika utekelezaji wa majukumu yake imekuwa zikirudisha nyuma nguvu zao. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo:

*(i)* Ukosefu wa miundombinu ya barabara zinazoingia kambini ni tatizo kubwa katika harakati za uimarishaji wa mawasiliano. Kwa mfano barabara inayoingia Kambi ya Mwanyanya, Kamabi ya Mto wa Maji, Kambi ya Kikungwi na Kamabi ya Ndugu Kitu zote hizi zipo katika hali mbaya na zinahitaji kufanyia mpango wa ujenzi.
*(ii)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri katika kambi za KVZ pia ni changamoto katika uimarishaji wa doria za ulinzi na usalama katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu.
*(iii)* Uhaba wa fedha za matumizi mengineyo kutokana na kiwango kidogo kinachopatikana lakini pia ufinyu wa bejti wenyewe ni tatizo kwa kikosi hiki kutokana na kasi waliyonayo katika uibuaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo.
*(iv)* Kuwepo kwa uhaba wa wataalamu wa fani mbali mbali ambazo zitasaidia kuimarika kwa maendeleo ya kikosi. Kwa mfano ukosefu wa Madaktari wabobezi katika fani za afya, ukosefu wa wahandisi katika fani za usanifu wa majengo, ukosefu wa wahandisi katika TEHAMA na kadhalika.
*(v)* Kutokamilika kwa wakati mradi wa ujenzi wa nyumba na mahanga ya askari katika kambi ya Kikungwi kutokana na mkandarasi kuchelewesha kazi kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba.
*(vi)* Kuchelewa kukamilika kwa marekebisho ya Sheria Nam. *5* ya mwaka *2004* ya KVZ kumepelekea kikosi kuchelewa kufanya kazi ya ulinzi kibishara.

**Maoni na Ushauri wa Kamati Kwa KVZ**

*(i)* Kamati inashauri KVZ kuzidisha kasi ya doria za ulinzi na usalama katika maeneo ya mijini hususan maeneo yaliyoathirika zaidi na makundi ya uhalifu kama vile mitaa ya Kinuni, Nyarugusu, Kwarara, Kianga, Mbuzini na Chuini.
*(ii)* Kamati inaishauri Serikali kuzidisha kasi ya kutuma fedha za miradi ya maendeleo kwa kikosi ili kukamilisha kazi zao za ujenzi.

*(iii)* Kamati inashauri Kikosi kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa askari wake ili waendane na kasi ya maendeleo.
*(iv)* Kamati pia inashauri Serikali kuzidisha bidii katika kufanya marekebisho ya sheria yake ili kuweza kulinda kibishara.
*(v)* Kamati inaishauri Serikali kufanya utaratibu wa kuongeza vyombo vya usafiri kwa KVZ Unguja na Pemba, sambamba na kuimarisha mawasiliano ya barabara zote zenye hali mbaya ambazo zinakwaza shughuli za kila siku.
*(vi)* Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua stahiki kwa Kampuni ya Zenji Holding Co. Ltd ambaye ameshindwa kwenda sambamba na matakwa ya mkataba wa usambaazaji wa vifaa kwa KVZ na hivyo kupelekea kambi ya Kikungwi kushindwa kukamilika kwa wakati na kusababishia kikosi hasara. Aidha, Kamati inashauri mkandarasi huyu kurejesha fedha za Serikali ambazo alipatiwa na hakuzifanyia kazi.

## 6.7 OFISI YA MKOA WA MJINI MAGHARIBI

Mkoa wa Mjini Magharibi ni miongoni mwa Mikoa mitano ya Zanzibar ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Ibara ya 2(a) na Sheria Nambari 08/2018 Sheria ya Tawala za Mikoa. Kiutawala Mkoa wa Mjini Magharibi ni mkusanyiko wa Wilaya tatu; (Mjini, Magharibi 'A' na Magharibi 'B') na Shehia 121 ukiwa na jukumu la kusimamia na kutekeleza Sera, Sheria, Mipango na Miongozo ya Serikali.

Aidha, Kamati inaupongeza uongozi wa Mkoa wa Mjini Magharibi chini ya Mkuu wa Mkoa mahiri Mhe. Idrisa Kitwana Mustafa kwa juhudi zake za kuleta maendeleo kwa wananchi za mji wa Zanzibar. Sambamba na hayo, Kamati imeridhika na utekelezaji wa Mkoa huu kutokana na mafanikio yafuatayo:

*(a)* Kuimarika kwa hali ya ulinzi na usalama kwa wananchi na wageni wanaoishi ndani ya Mkoa.
*(b)* Mkoa umeratibu maagizo na ahadi mbalimbali za viongozi wa SMZ na SMT zilizotolewa wakati wa ziara zilizofanywa ndani ya Mkoa.
*(c)* kufuatilia na kusimamia miradi ya maendeleo ambayo ndio msingi wa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.
*(d)* Kufanikiwa kwa Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar
*(e)* kufuatilia na kusimamia matukio ya udhalilishaji ambayo yamekuwa yakiripotiwa katika Ofisi ya Mkoa.

**Changamoto za Mkoa wa Mjini Magharibi**

(i) uhaba wa fedha za matumizi mengineyo katika uendeshaji wa ofisi.

(ii) Uchakavu wa miundombinu katika Mkoa kama vile maji na barabara

(iii) Hali hatarishi kwa baadhi ya maeneo ya ng'ambo ya mji kutokana na kuibuka kwa makundi ya vijana wenye kutishia usalama wa raia na mali zao kwa kutumia silaha za jadi kuwahujumu wananchi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mkoa wa Mjini Magharibi**

*(a)* Kamati inashauri Mkoa kusimamia na kuzidisha kasi ya kufanya doria katika maeneo yenye viashiria vya uvunjifu wa amani kwa kujitokeza vikundi viovu ambavyo vinahatarisha maisha ya wananchi kwa kutumia silaha za jadi. Maeneo haya yanajumuisha maeneo ya Wilaya ya Magharibi 'A'.

*(b)* Kamati inashauri mpango wa ujenzi wa Ofisi za Masheha kufanywa kwa haraka na kuzingatia mahitaji mahususi licha ya changamoto ndogo ndogo zinanazojitokeza katika upatikanaji wa maeneo ya ujenzi.

*(c)* Pia, Kamati inashauri Mkoa kuzidisha kasi ya kufuatilia ujenzi wa miradi ya maendeleo ambayo inaendelea kwa kasi katika maeneo yake ili inapokamilika iwe na ubora na yenye kukidhi mahitaji ya wananchi kwa muda mrefu.

## 6.8 BARAZA LA JIJI LA ZANZIBAR

Baraza la Jiji la Zanzibar lilianzishwa mwaka 2019 chini ya kifungu cha 18 cha Sheria Nam. 7 ya Mwaka 2014. Majukumu ya msingi ya Baraza la Jiji yameainishwa katika kifungu cha 19(a), (b), (c), (d), (e), (f), (g) na (h) cha Sheria hiyo. Katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza, Kamati imeridhishwa na hatua iliyopo katika utekelezaji wake licha ya kuwepo changamoto ndogo ndogo ambazo zinarudisha nyuma juhudi zao. Aidha, Kamati inaupongeza uongozi wa Baraza kwa kusaidia kukuza maendeleo ya jiji la Zanzibar pamoja na kulifanya liweze kutambulika ndani na nje ya Zanzibar kutokana na utekelezaji wake.

**Changamoto za Baraza la Jiji la Zanzibar**

Katika utekelezaji wa Bajeti, Baraza la Jiji la Zanzibar linaendelea kusimama na changamoto zake za muda mrefu ambazo kimsingi hazijapatiwa utatuzi kama ifuatavyo:

*(a)* Ukosefu wa jengo la kudumu la Baraza pamoja na vifaa vya kufanyia kazi na vyombo vya usafiri;
*(b)* Ukosefu wa vyanzo vya mapato katika maeneo ya Jiji la Zanzibar;
*(c)* Uhaba wa wataalamu katika sekta ya Uchumi na miundombinu.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

Ili kukabiliana na changamoto hizo, Kamati inashauri hatua zifuatazo:

*(i)* Serikali kuchukua hatua za makusudi kwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa, Nam. 7 ya Mwaka 2014 ambayo itaweka muundo utakao liwezesha Baraza la Jiji kujitegemea katika eneo lake la kiutawala pamoja na kuwa na vyanzo vyake vya mapato bila kuwepo mgongano na taasisi nyengine.

*(ii)* Kamati inashauri Baraza kuendelea kubuni na kuibua vyanzo vya mapato na miradi ya kiuchumi na kijamii ambayo italiwezesha Baraza kujikimu kwa kipato na hivyo kupata nguvu kiuchumi.

*(iii)* Baraza liandae mpango maalumu utakaowawezesha kupata ofisi yake ya kudumu pamoja na kuwa na wataalamu ambao watasaidia kukuza maendeleo ya Jiji.

## 6.9 BARAZA LA MANISPAA MJINI

Baraza la Manispaa Mjini limeanzishwa kwa Mujibu wa Sheria Nam. 7 ya Mwaka 2014, Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na lina jukumu la kutoa huduma kwa wananchi ikiwemo kutoa huduma za usafi wa mji na mazingira, kukusanya mapato, kusimamia na kutekeleza mpango mkuu wa mji.

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hiki ni kama ifuatavyo:

*(i)* Kuimarisha usafi wa mji na haiba yake kwa kuzoa taka na kusimamia usafi wa mji.

*(ii)* Kufanikiwa kutoa elimu ya usafi katika jamii kupitia vyombo vya habari.
*(iii)* Kuimarisha mazingira bora ya wafanyabiashara wadogo wadogo kwa kuwapatia vitambulisho vya ujasiriamali.
*(iv)* Kuboresha vyanzo vya mapato na ukusanyaji wa mapato kwa kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa matumizi ya risiti na mashine za kielektroniki.
*(v)* Kuimarisha huduma za jamii na masuala mtambuka kwa kutoa elimu ya usafi wa mazingira na namna ya kujinga na maradhi ya mripuko.

**Changamoto za Baraza la Manispaa Mjini**

Licha ya mafanikio mbali mbali yaliyofikiwa katika kipindi hiki, Baraza la Manispaa ya Mjini linakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

*(i)* Kushuka kwa kiwango cha ukusanyaji wa mapato kutokana na kuondoshwa kwa vyanzo vya mapato vilivyomo ndani ya Mamlaka ya Mji Mkongwe baada ya kufanyika marekebisho ya sheria ya Mamlaka ya Mji Mkongwe.
*(ii)* Mwamko mdogo wa wananchi katika kushirikiana na Baraza la Manispaa juu ya masuala ya usafi.
*(iii)* Mwamko mdogo wa wajasiriamali katika kujisajili na kupatiwa vitambulisho vya biashara.
*(iv)* Kuongezeka kwa uzalishaji wa taka kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu na makaazi.
*(v)* Muitiko mdogo wa wafanyabiashara juu ya uliopaji wa ada na tozo mbali mbali za Manispaa na hivyo kupelekea kushuka kwa mapato.
*(vi)* Kuvunjwa kwa soko la Mombasa kwa ajili ya ujenzi wa soko jipya kumepelekea kupungua kwa mapatao ya Manispaa katika kipindi hiki cha utekelezaji wa bajeti.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Baraza la Manispaa ya Mjini:**

Kutokana na changamoto hizi ambazo Kamati imeziibua na kimsingi zinarudisha nyuma maendeleo ya Manispaa ya Mjini, Kamati inashauri na kupendekeza mambo yafuatayo:

*(i)* Baraza liongeze programu za uhamasishaji jamii juu ya masuala ya usafi upitia televisheni, redio, mikutano ya jamii pamoja na mitandao ya kijamii.

(ii) Baraza litie nguvu katika matumizi ya kanuni za papo kwa papo ili uweka nidhamu katika mji na kuongeza vyanzo vipya vya mapato baada ya kuondoka vile vya Mamlaka ya Mji Mkongwe.

(iii) Baraza lihakikishe limeendeleza zoezi la usajili wa wajasiriamali pamoja nakuwapatia vitambulisho vya kazi kwa mujibu wa maeneo yao ili kupunguza vijana wanaozurura mitaani.

(iv) Baraza lizidishe kasi ya usafi wa mji pamoja na kutia nguvu katika ukusanyaji wa taka kwa kutafuta wawekezaji ambao watashughulika na ukusanyaji wa taka ili kupunguza kwa kiasi kikubwa taka zinazozagaa mitaani.

(v) Kamati inashauri Baraza kuwatumia Madiwani wao katika utoaji wa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kulipa kodi na kuzidisha kazi ya usafi wa mitaani.

(vi) Baraza la Manispaa liandae mpango maalumu utakaowasaidia kupata magari ya kubea taka pamoja na gari la majitaka ambalo ndio tatizo kubwa katika sekta ya usafi wa mji.

(vii) Baraza liongeze juhudi katika kusimamia vyanzo vya mapato vilivyopo kwa kufanya operesheni mbali mbaali kwa ajili ya wafanyabiashara na wananchi wanaokwepa kulipa ada na tozo kwa hiari.

## 6.10 BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI "A"

Baraza la Manispaa Magharibi 'A' limeanzishwa kwa Sheria Nam. 7 ya Mwaka 2014, Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na linajukumu la kutoa huduma kwa wananchi ikiwemo kutoa huduma za usafi wa mji na mazingira, kukusanya mapato, kusimamia na kutekeleza mpango mkuu wa mji.

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika Baraza la Maanispaa ya Magharibi 'A' ni kama ifuatavyo:

(a) Kuimarika kwa usafi wa Mazingira;
(b) Kusimamia na kuboresha mazingira ya wafanyabiashara wadogo wadogo;
(c) Kusimamia na kufuatilia ujenzi wa soko la Chuini.
(d) Kuongeza kasi katika ukusanyaji wa mapato.

**Changamoto za Baraza la Mji Magaharibi 'A'**

Licha ya mafanikio ambayo Baraza limeyafikia kwa mwaka huu, lakini bado zipo changamoto ambazo zinahitaji mikakati maalumu ya kuweza kuzitatua.

Miongoni mwao ni kama zifuatazo:

*(a)* Uhaba wa vitendea kazi ikiwemo magari ya taka na vifaa vya ofisini;
*(b)* Elimu ndogo kwa wananchi juu ya umuhimu wa uhifadhi wa mazingira ya mji na maeneo ya kibiashara.
*(c)* Kuwepo kwa vyanzo vichache vya mapato kwa Manispaa.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

*(i)* Baraza lianzishe mpango ambao utawasaidia kupata vitendea kazi kwa mashirikiano na Serikali kuu ili kufikia malengo iliyojiwekea.
*(ii)* Baraza lizidishe kasi ya kufanya usafi wa mazingira na kuielimisha jamii juu ya matumizi sahihi ya mazingira.
*(iii)* Baraza liombe Serikalini ajira za wataalamu ambao watasimamia miradi yake ya ujenzi na ukusanyaji wa mapato.
*(iv)* Baraza lifuatilie kwa ukaribu vyanzo vyake vya mapato na kutoa elimu kwa wafanyabiashara kuhusu malipo ya tozo na ada.
*(v)* Katika kukabiliana na changamoto ya taka mitaani, Kamati inaishauri Manispaa kutafuta muwekezaji ambaye atawekeza katika ukusanyaji wa taka na kupunguza mrundikano wa taka majumbani. Aidha, kufanya hivyo kutaisaidia Manispaa kupata chanzo kipya cha mapato.
*(vi)* Kamati pia, inashauri Manispaa waharakishe ujenzi wa kituo cha daladala Mndo na soko la Kwakisasi.

## 6.11 BARAZA LA MANISPAA YA MAGHARIBI "B"

Baraza la Manispaa Magharibi 'B' limeanzishwa kwa Mujibu wa Sheria Nam. 7 ya Mwaka 2014, Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na linajukumu la kutoa huduma kwa wananchi ikiwemo kutoa huduma za usafi wa mji na mazingira, kukusanya mapato, kusimamia na kutekeleza mpango mkuu wa mji.

Miongoni mwa mafanikio ya Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" ni kama yafuatayo:

*(a)* Kuimarisha usafi wa mji kwa kuendeleza programu za usafi siku hadi siku kupitia maeneo ya biashara na makaazi ya watu;

(b) Kuhamasisha ukusanyaji wa mapato kupitia vyombo vya habari na kutoa elimu kwa walipakodi;
(c) Kukamilisha ujenzi wa miradi ya masoko ya Mwanakwerekwe na Jumbi pamoja na kuendeleza ujenzi wa maduka ya wajasiriamali Mombasa Sheli;
(d) Kukuza ustawi wa jamii na kupunguza umasikini kwa kuwafikishia wananchi huduma za kijamii;
(e) Kuwajengea mazingira bora wajasiriamali wadogo wadogo kwa kuwasajili na kuwapatia vitambulisho.

**Changamoto za Baraza La Manispaa Magharibi 'B'**

Yapo mafanikio kadhaa yaliyofikiwa na Baraza la Manispaa Magharibi 'B' kutokana na utendaji kazi wao ambao hauna shaka umefanyika kwa mujibu wa sheria na taratibu za Manispaa, pia zipo changamoto ambazo zinakwaza shughuli zao za kazi.

Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatavyo:

(i) Kuongezeka kwa uzalishaji wa taka katika maeneo ya mji na hivyo kufanya maeneo mengi ya makaazi ya watu kuwa na hali isiyoridhisha.
(ii) Kuwepo kwa uhaba wa vitendea kazi kama vile magari ya kuzolea taka na mashine za kisasa za ukusanyaji wa mapato.
(iii) Uelewa mdogo wa wananchi katika ukusanyaji wa ada na tozo pamoja kutofanya malipo kwa wakati.
(iv) Ukosefu wa mipango miji ambayo inakwaza zoezi la usafi na kusababisha kuenea kwa taka katika maeneo mbali mbali ya mji.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

Kwa kuwa Kamati imeridhishwa na mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa majukumu ya Baraza kwa kipindi hiki, pia haikusita kushauri mambo mbali mbali ambayo kimsingi yanadhamira ya kuimarisha maendeleo ya Manispaa hii. Hivyo, miongoni mwa mambo ambayo Kamati inashauri ni kama ifuatavyo:

(i) Kamati inashauri Baraza kuongeza nguvu katika suala zima la usafi ili kukabiliana na ongezeko la taka katika maeneo ya mji.
(ii) Baraza liweke utaratibu wa kununua vitendea kazi pamoja na kuweka mpango maalumu utakaowasaidi kupata magari ya taka.
(iii) Uelewa mdogo wa wananchi katika ukusanyaji wa ada na tozo pamoja kutofanya malipo kwa wakati iwe ni kipaumbele cha Baraza katika kuwapatia wananchi elimu ya ulipakodi.

*(iv)* Baraza lihakikishe baada ya kumalizika kwa ujenzi wa miradi ya masoko ya Mwanakwerekwe na Jumbi kipaumbele kimetolewa kwa wafanyabiara ambao waliondolewa kupisha ujenzi ili kuwapunguzia ukali wa maisha kwa kuwapatia sehemu za kudumu za biashara.

## 6.12 OFISI YA MKOA WA KUSINI UNGUJA

Mkoa wa Kusini Unguja umeundwa kwa mujibu wa Sheria Nam. *8* ya Tawala za Mikoa ya mwaka *2014.* Mkoa wa Kusini Unguja unajukumu la kuratibu, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa sera, mipango na miongozo ya Serikali. Aidha, Mkoa unasimamia na kuratibu shughuli za ulinzi na usalama na kuhakikisha kuwa rasilimali watu na vitu vinatumika kwa maendeleo ya uchumi na jamii kwa ujumla. Kamati inampongeza Mkuu wa Mkoa huu Mhe. Ayub Mohammed Mahmoud kwa juhudi zake kubwa za kuleta maendeleo katika uongozi wake.

Katika utekelezaji wa majukumu ya Mkoa, mafanikio makubwa yamepatikana ikiwa ni pamoja na:

*(a)* Kusimamia na kuendeleza hali ya ulinzi na usalama kwa kuimarisha amani na utulivu kwa wananchi;
*(b)* Kuendeleza mapambano dhidi ya dawa za kulevya, ajali za barararani na matukio ya moto;
*(c)* Mkoa umefanikiwa kuratibu ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa pamoja na Utekelezaji wa maagizo ya viongozi kupitia ziara ya Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi na kutembelea maeneo ya miradi ambapo utekelezaji wake upo katika hali ya kuridhisha.

**Changamoto za Mkoa wa Kusini Unguja**

Katika jitihada za kukuza uchumi wa nchi na kupunguza umasikini katika jamii, hatuna budi kukabiliana na changamoto ambazo zinakwaza katika maendeleo yetu. Changamoto hizo ni kama zifuatazo:

*(i)* Kushamiri kwa vitendo vya wizi wa mifugo na mazao;
*(ii)* Ongezeko la matumizi ya dawa za kulevya katika maeneo ya ukanda wa bahari; na
*(iii)* Kushamiri kwa vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa wanawake na watoto.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mkoa wa Kusini Unguja:**

Katika kujenga mustakbali uliobora na wenye kuleta ufanisi kwa wananchi wetu, hatunabudi kuishauri Serikali ya Mkoa huu kukabiliana na changamoto hizo.

Aidha, Kamati inashauri kama ifuatavyo:

*(a)* Mkoa uzidishe doria za ulinzi na usalama katika juhudi za kupambana na makundi hatarishi yanayojitokeza katika jamii ili kulinda na kuendeleza usalama kwa wananchi wetu na wageni.

*(b)* Mkoa udhibiti matamasha yanayofanyika katika maeneo yake na kufahamu uhalali wa kila tamasha na malengo yake. Aidha, Kamati inashauri kusimamia, kufuatilia na kuchukua hatua za kisheria kwa wale wote wanaokaidi amri ya muda maalumu kwa kumaliza sherehe za usiku.

*(c)* Mkoa uanzishe kampeni maalumu za kumaliza vitendo vya wizi wa mazao na mifugo pamoja na kuwachukulia hatua kali za kisheria wale wenye kupatikana na hatia.

## 6.13 BARAZA LA MJI KATI

Baraza la Mji Kati ni miongoni mwa Serikali za Mitaa ambayo imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa Nam. 7 ya Mwaka 2014 na imekasimiwa majukumu yake kwa mujibu wa sheria hiyo. Kamati imefuatilia vya kutosha utekelezaji wa majukumu ya Baraza na kujionea jinsi wanavyojitahidi katika kufikia malengo waliyokusudia.

Mafanikio yaliyopatikana katika Utekelezaji wa Baraza la Mji Kati ni kama yafuatayo:

*(a)* Kuimarisha programu za usafi wa mazingira kwa maeneo yote ya makaazi ya watu na yale ya kibiashara;
*(b)* Kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa kuhifadhi taka hatarishi na matumizi salama ya vyoo.
*(c)* Kukamilisha mradi wa ujenzi wa Soko la Dunga Kiembeni;
*(d)* Kuimarisha mazingira ya wajasiriamali na makundi maalumu ili yaweze kujikwamua na umasikini.

(e) Kamati inawashukuru Baraza la Mji Kati kwa kutekeleza agizo la Kamati katika ujenzi wa vyoo vya skuli ya Uchukuni.

**Changamoto za Baraza la Mji Kati**

Katika mafanikio makubwa yaliyopatikana na kuisaidia jamii kufikia maendeleo endelevu, Baraza la Mji Kati linakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Ukosefu wa gari la kubebea taka na kuzipeleka jaa kuu Kibele;
*(ii)* Uhaba wa vyombo vya usafiri katika utekelezaji wa majukumu yao;
*(iii)* Uelewa mdogo wa wafanyabiashara katika ulipaji wa ada na tozo kwa wakati na kwa maslahi ya nchi yetu; na
*(iv)* Kasi ndogo ya usajili wa wajasiriamali na kutoa vitambulisho.

**Maoni, Mapendekezo na ushauri wa Kamati**

Ili kuweza kufikia hatua ya mafanikio katika Baraza la Mji Kati na kufikia hatua iliyokusudiwa, Kamati inashauri mambo yafuatayo:

*(a)* Kuzidisha kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa kutoa elimu kwa wafanyabiashara pamoja na kubuni vyanzo vipya vitakavyosaidia ongezeko la mapato.
*(b)* Baraza liwafikie wajasiriamali wadogo wadogo na kutatua changamoto zao ambazo zinarudisha nyuma maendeleo yao, sambamba na kuwapatia vitambulisho kwa wakati.
*(c)* Baraza liongeze kasi ya usafi wa miji hususan sehemu za hoteli za kitalii kwa kutafuta wawekezaji watakao fanya usafi kwa uhakika.

### 6.14 HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI UNGUJA

Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja ni miongoni mwa taasisi za Serikali za Mitaa ambayo imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa, Nam. 8 ya Mwaka 2014.

Katika utekelezaji wa majukumu ya Halmashauri hii, Kamati imeelezwa mafanikio yafuatayo:

*(a)* Kuimarika kwa usafi wa mazingira ya miji na vijiji.
*(b)* Kuwawezesha wajasiriamali kiuchumi kwa kusimamia mradi wa ujenzi wa jengo la Wajasiriamali Kitogani.

(c) Kamati pia, imeridhishwa na mradi wa ujenzi wa eneo maalumu la wajasiriamali na wafanya biashara wa Wilaya ya Kusini katika eneo la Kitogani.

**Changamoto za Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja**

Mbali ya mafanikio hayo ambayo Halmashauri imefanikiwa kuyapata lakini bado Kamati imebaini changamoto mbali mbali ambazo kimsingi zinafanana na Halmashauri nyengine za Zanzibar. Changamoto zenyewe ni kama zifuatazo:

*(i)* Kushuka kwa ukusanyaji wa mapato siku hadi siku.
*(ii)* Katika zoezi la ukusanyaji wa taka, Kamati ina mashaka na kampuni za wawekezaji wa ukusanyaji wa taka kwa jinsi utaratibu uliotumika wa kuzipata kampuni hizo na namna ya utaratibu wa ugawaji wa majukumu ya ukusanyaji taka uliotumika.
*(iii)* Uhaba wa vitendea kazi vya kisasa katika ukusanyaji wa mapato.
*(iv)* Uelewa mdogo wa wananchi katika ukusanyaji wa mapato na kulinda vyanzo vya mapato.
*(v)* Uhaba wa vyombo vya usafiri kwa watendaji wa Halmashauri.
*(vi)* Uhaba wa watendaji wa Halmashauri hususan wataalamu wenye ujuzi na uzoefu wa kutosha katika fani za miradi na mapato.
*(vii)* Uwepo wa tatizo la wizi wa mifugo, ukosefu wa malisho na elimu ndogo ya ufugaji wa kibiashara kwa wakulima.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja**

*(i)* Kamati inashauri Halmashauri kutoa elimu zaidi juu ya ukusanyaji wa mapato na uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato.
*(ii)* Kamati inashauri Halmashauri kuzidisha kasi ya usajili wa wajasiriamali ili kupata takwimu zao halisi na kuwafikia katika shughuli mbali mbali.
*(iii)* Kamati inaishauri Halmashauri kuzidisha usafi katika maeneo yenye hoteli na kusimamia shughuli zote zinazofanyika katika maeneo yao.
*(iv)* Kamati pia, inashauri Halmashauri kutafuta muwekezaji wa kizalendo atakaefanya kazi ya ukusanyaji wa taka katika hoteli za kitalii na endapo atashindikana mwenyeji basi fursa hii wapatiwe wageni.
*(v)* Kamati inashauri Halmashauri waandae programu maalumu ya kutoa elimu kwa wafanyabiashara wadogo wadogo katika kuendeleza na kukuza biashara zao.

## 6.15 OFISI YA MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Mkoa wa Kaskazini Unguja ni miongoni mwa Mikoa mitano ya Zanzibar ambao umeanzishwa chini ya Sheria ya Tawala za Mikoa, Nam. *8* ya mwaka *2014* na una majukumu ya kuratibu, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa sera, mipango na miongozo ya Serikali. Aidha, Mkoa unasimamia na kuratibu shughuli za ulinzi na usalama na kuhakikisha kuwa rasilimali watu na vitu vinatumika kwa maendeleo ya uchumi na jamii kwa ujumla ambapo Kamati inampongeza kwa dhati kabisa Mkuu wa Mkoa huu Mhe. Rashid Hadid Rashid kwa namna anavyotekeleza majukumu yake kwa weledi na kufuta misingi ya nchi na Ilani ya CCM ya 2020 – 2025.

Mkoa wa Kaskazini Unguja unajumla ya Wilaya mbili; Wilaya ya Kaskazini “A” na Wilaya ya Kaskazini “B” pamoja na Halmashauri za Baraza la Manispaa Kaskazini “A” na Baraza la Mji Kaskazini “B”.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi wa Kitaifa ilifanikiwa kutembelea Baraza la Manispaa Kaskazini “A” na Baraza la Mji Kaskazini “B” Unguja kwa lengo la kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika Halmashauri hizi pamoja na kufahamu namna gani wamefanikiwa katika utekelezaji wao wa matumizi ya fedha.

## 6.16 BARAZA LA MANISPAA KASKAZINI “A”

Baraza la Manispaa Kaskazini “A” Unguja ni moja ya Halmashauri mbili zilizomo katika Mkoa wa Kaskazini Unguja zilioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mabaraza ya Miji Sheria Nam. 7 mwaka 2014 kwa madhumuni ya kuanzisha Serikali za Mitaa, uwezo wake, kazi na wajibu, muundo, mpangilio, fedha na mambo mengine yanayohusiana na utaratibu uliowekwa katika sheria hiyo. Baraza la Manispaa Kaskazini “A” limepata mafanikio mbali mbali kutokana na utekelezaji wake na usimamizi madhubuti ya fedha za bajeti.

Miongoni mwa mafanikio yake ni kama ifuatavyo:

*(a)* Kupandishwa hadhi kwa Baraza la Mji na kuwa Baraza la Manispaa kama zilivyo Manispaa nyengine za hapa Zanzibar;
*(b)* Kusimamia usafi wa mazingira ya miji na fukwe;
*(c)* Kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
*(d)* Kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa kutumia vyanzo mbali mbali vya Manispaa;

*(e)* Kuendelea kusajili na kuwatambua wajasiriamali; na
*(f)* Kuwasaidia wajasiriamali kwa kuwajengea mazingira rafiki ya kibishara.

**Changamoto za Baraza la Manispaa Kaskazini "A" Unguja**

Baraza la Manispaa Kaskazini "A" Unguja, linakabiliwa na changamoto tofauti ambazo zinarudisha nyuma maendeleo yao, miongoni mwa changamoto hizo ni: -

*(i)* Uhaba wa vyombo vya usafiri na vitendea kazi vya Manispaa;
*(ii)* Uhaba wa watumishi katika fani mbali mbali ikiwemo wataalamu wabunifu katika masuala ya mapato na miundombinu;
*(iii)* Mwamko mdogo wa wananchi juu ya ulipaji kodi kwa hiari;
*(iv)* Kuchelewa kwa mgao wa fedha za mali zisizorejesheka kutoka Serikali Kuu.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Baraza la Manispaa Kaskazini "A" Unguja: -**

*(a)* Kamati inaishauri Manispaa kusimamia kikamilifu suala la usafi wa mji pamoja na hoteli sambamba na kutafuta wawekezaji zaidi ambao wataekeza katika ukusanyaji wa taka.
*(b)* Kamati inashauri Manispaa hii mpya iweze kuwashirikisha wananchi katika maamuzi ya miradi ya maendeleo na kuibua vyanzo vipya vya mapato;
*(c)* Kamati inashauri Manispaa kuchukua kwa vitendo juu ya suala la upatikanaji wa vyombo vya usafiri kama taratibu zinavyoelekeza;
*(d)* Kamati inashauri Manispaa kutoa elimu ya ulipaji wa ada na tozo kwa wafanyabiashara wadogo wadogo kupitia vyombo vya habari na mikutano ya wajasiriamali.
*(e)* Kamati inashauri Manispaa kusimamia upatikanaji wa vitambulisho kwa wajasiriamali na kuzidisha kasi ya usajili ili kuwa na taarifa za uhakika za biashara.

## 6.17 BARAZA LA MJI KASKAZINI "B"

Baraza la Mji Kaskazini "B" Unguja ni moja ya Halmashauri mbili zilizomo katika Mkoa wa Kaskazini Unguja zilioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mabaraza ya Miji Sheria Nam. 7 mwaka 2014 kwa madhumuni ya kuanzisha Serikali za Mitaa.

Katika utekelezaji wa malengo ya Baraza kwa mwaka 2023/2024 Kamati yetu imeridhishwa na juhudi zilizochukuliwa na uongozi wa Baraza la Mji Kaskazni "B" kwa ajili ya kuimarisha maendeleo yake.

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni haya yafuatayo: -

*(a)* Kuendelea kutoa huduma bora kwa jamii, ikiwemo kuwapatia taaluma wananchi juu ya usafi wa mazingira na ulipaji wa ada kwa hiari.
*(b)* Baraza kuendelea kusajili wajasiriamali wadogo wadogo kwa lengo la kuboresha maendeleo yao.
*(c)* Baraza limeweza kuibua miradi ya maendeleo na kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kujenga soko la Donge Mtambile, soko la wajasiriamali Kitope, skuli ya Kinduni na kituo cha TuTu wadi ya Donge Vijibweni.
*(d)* Kukuza na kuimarisha vyanzo vya mapato kwa kuibua vyanzo vipya na kuongeza idadi ya wajasiriamali.

**Changamoto za Baraza La Mji Kaskazini "B"**

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, pia zipo changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa shughuli za Baraza, miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatavyo: -

*(a)* Kuondoshwa kwa baadhi ya vyanzo vya mapato katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kupelekwa Serikali kuu kumepelekea kushuka kwa kiwango cha mapato.
*(b)* Uchache wa vyanzo vya mapato katika Halmashauri hii kumepelekea kuathiri ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri.
*(c)* Kuwepo kwa uhaba wa vyombo vya usafiri katika kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara katika vyanzo vya mapato.
*(d)* Uelewa na mwamko mdogo wa wananchi kujisajili na kupatiwa vitambulisho vya ujasiriamali.
*(e)* Uhaba wa wataalamu katika fani mbali mbali ikiwemo ukusanyaji wa mapato na miundombinu.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Baraza la Mji Kaskazini "B"**

Katika kukabiliana na changamoto hizo juhudi na mikakati mbalimbali inahitajika ili kupatiwa ufumbuzi wa changamoto hizo hatua kwa hatua. Hivyo, basi Kamati inashauri mambo yafuatayo:

*(a)* Kamati inashauri Mamlaka husika kufanya mgao wa rasilimali fedha ambao wamepangiwa kupatiwa Mabaraza kupitia mali zisizorejesheka ili kwenda sambamba na bajeti zao.
*(b)* Baraza la Mji Kaskazini 'B' liendelee na kubuni vyanzo vipya vya mapato ambavyo vitasaidia kuongeza mapato na kuacha kutegemea chanzo cha mali zisizorejesheka kama chanzo kikuu cha mapato.
*(c)* Baraza liendelee kutoa elimu juu ya ulipaji wa ada na tozo kupitia wajasiriamali katika maeneo ya biashara.
*(d)* Baraza liweke kipaumbele cha kuwasomesha watumishi wake katika kupata elimu ili kukabiliana na changamoto ya wataalamu.
*(e)* Baraza lizidishe kasi ya kufanya usafi wa mji na fukwe ambazo ni kivutio kikubwa cha utalii katika ukanda wa bahari.
*(f)* Aidha, Baraza liongeze kasi katika ukusanyaji wa mapato na kutoa wito kwa wafanyabishara kulipa kodi kwa wakati.

## 6.18 OFISI YA MKOA WA KUSINI PEMBA

Mkoa wa Kusini Pemba umeanzishwa chini ya Sheria ya Tawala za Mikoa, nambari *8* ya mwaka *2014* na una majukumu ya kuratibu, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa sera, mipango na miongozo ya Serikali. Aidha, Mkoa unasimamia na kuratibu shughuli za ulinzi na usalama na kuhakikisha kuwa rasilimali watu na vitu vinatumika kwa maendeleo ya uchumi na jamii kwa ujumla.

Kamati imeupongeza Mkoa huu kwa kuona utekelezaji wa shughuli zake zikifanikiwa kwa kiwango kikubwa na hivyo kuwafanya wakaazi wake kuishi kwa amani na utulivu chini ya uongozi mahiri wa Mkuu wa Mkoa huu, Mhe. Matter Zahor Masoud.

Katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Mkoa wa Kusini Pemba umeweza kufanikiwa katika mambo yafuatayo: -
(a) Kuimarika kwa hali ya ulinzi na usalama katika mkoa.
(b) Utekelezaji wa mpango mkakati wa kitaifa juu ya kupambana na masuala ya udhalilishaji ya Mkoa.
(c) Utoaji wa huduma za utumishi na uendeshaji katika Mkoa.
(d) Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mradi wa ujenzi wa soko la samaki na matunda la Machomane.

(e) Kusimamia na kufuatilia ujenzi wa bustani ya Mwanamashungi.
(f) Kusimamia na kuratibu ziara za viongozi wakuu wa nchi katika Mkoa.

**Changamoto za Mkoa wa Kusini Pemba:**

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku bado kuna changamoto ndogo ndogo ambazo Kamati imezibaini na zinafaa kuchukuliwa hatua. Changamoto zenyewe ni kama zifuatavyo:

(a) Uchakavu na ufinyu wa majengo ya Ofisi za Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya ya Chake Chake na Mkoani.
(b) Ukosefu wa vyombo vya usafiri katika Ofisi za Mikoa na Wilaya.
(c) Uwepo wa tabia mbaya za wizi wa mazao na mifugo kwa baadhi ya maeneo ya miji na vijijini.
(d) Ongezeko la uingizaji na utumiaji wa dawa za kulevya kwa rika tofauti hususan vijana.

**Maoni na ushauri wa Kamati kwa Mkoa wa Kusini Pemba**

*(i)* Kamati inaishauri Serikali kuanzisha mpango wa kujenga ofisi za Wakuu wa Wilaya ili kupata makaazi bora pamoja na kuzikarabati nyumba wanazoishi au kujengwa upya pale ambapo uwezo utaruhusu.
*(ii)* Kamati pia, inaiomba Serikali kuwapatia watendaji wa ofisi za Wilaya na Mkoa vifaa vya kazi ikiwemo vyombo vya usafiri ili kuimarisha mazingira yao ya kazi.
*(iii)* Kamati inashauri watendaji wa Mkoa kuzidisha kasi ya utendaji ili kumsaidia Mkuu wa Mkoa kwa kutoa huduma bora katika jamii.
*(iv)* Kamati inaomba Mkoa kuzidisha kasi ya doria za wizi wa mifugo na mazao ya wakulima ili kujenga matumaini mema kwa wananchi wetu.
*(v)* Mkoa uzidishe kasi ya kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo mbali mbali ili kuimarisha amani na utulivu uliopo katika jamii.

## 6.19 BARAZA LA MANISPAA CHAKE CHAKE

Kama ilivyo kwa Halmashauri nyengine za Zanzibar; Baraza la Mji la Chake – Chake ni moja ya Mabaraza mawili yaliyomo katika Mkoa wa Kusini Pemba yalioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za

Serikali za Mitaa, Sheria Nam. 7 mwaka 2014 kwa madhumuni ya kuanzisha Serikali za Mitaa. Katika utekelezaji wa malengo ya Baraza la Manispaa kwa mwaka 2023/2024 Kamati yetu imeridhika na utendaji wa Baraza la Manispaa ya Chake – Chake kutokana na kukua kwake kwa kasi na hivyo kulifanya Baraza kupandishwa hadhi na kuwa Manispaa ya kwanza kwa upande wa Pemba.

**Mafanikio ya Baraza la Manispaa ya Chake – Chake: -**

(a) Kuongezeka kwa kasi ya ukusanyaji wa mapato na kuongeza vyanzo vipya katika maeneo ya mjini;
(b) Kuimarika kwa huduma za uendeshaji na Kuwajengea uwezo wafanyakazi;
(c) Kuimarika kwa usafi wa mazingira katika maeneo ya Miji na vijijini;
(d) Kuyawezesha makundi maalum kujiimarisha kiuchumi;
(e) Kukamilika kwa ujenzi wa soko la samaki na matunda la Machomane, kukamilika kwa soko la wajasiriamali la Michakaini; na
(f) Kuendelea kwa mradi wa ujenzi wa bustani ya Mwanamashungi.

**Changamoto za Baraza la Manispaa ya Chake – Chake:**

Pamoja na kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato na kukuwa kwa hali ya usafi wa Mji kwa kuzifikia Shehia nyingi zaidi bado Ofisi ya Baraza la Manispaa Chake – Chake inakabiliwa na changamoto kadhaa katika utekelezaji wa majukumu yake.

Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto hizo zinarudisha nyuma maendeleo ya Mji na Vitongoji vyake. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatavyo:-

*(i)* Mwamko mdogo wa wananchi katika ukusanyaji wa ada na tozo za Manispaa.
*(ii)* Mwamko mdogo wa wajasiriamali kujisajili na kudai vitambulisho.
*(iii)* Uhaba na uchakavu wa gari la kukusanyia taka.
*(iv)* Ukosefu wa eneo la maegesho ya magari katika soko jipya la Michakaini.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Baraza la Manispaa ya Chake – Chake:**

*(a)* Kamati inalishauri Baraza la Manispaa kusimamia wafanya bishara kuweza kulipa kodi kwa wakati bila ya kuwaonea muhali kama ilivyo mazoea.
*(b)* Kamati inashauri Manispaa kuandaa programu maalumu za kutoa elimu kwa wajasiriamali kupitia vyombo vya habari na vikundi vya hamasa.
*(c)* Kamati inashauri Serikali kusaidia Manispaa hii mpya na changa kuweza kupata vyombo vya usafiri ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi zaidi.
*(d)* Manispaa pia, ijikite katika usafi wa mji, ukusanyaji wa mapato na kutoa huduma kwa jamii kwani hizo ndio kazi kuu za Manispaa kwa mujibu wa Sheria.
*(e)* Manispaa pia, iangalie kutoa kazi ya ukusanyaji wa taka kwa taasisi binafsi ili kusaidia kufanya usafi wa mji lakini pia kuongeza chanzo kipya cha mapato.
*(f)* Kamati inashauri kujenga eneo la maegesho ya magari na bustani katika soko la Michakaini ili kuondoa usumbufu kwa watumiaji wa soko hili.

## 6.20 BARAZA LA MJI MKOANI – PEMBA

Katika muendelezo wa shughuli za Kamati katika kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali imefika Baraza la Mji Mkoani kama moja ya Mabaraza yaliyomo katika Mkoa wa Kusini Pemba lilioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mabaraza ya Miji Sheria Nam. 7 mwaka 2014 kwa madhumuni ya kuanzisha Serikali za Mitaa. Katika utekelezaji wa malengo ya Baraza kwa mwaka 2023/2024

**Mafanikio ya Baraza la Mji Mkoani:**

*(i)* Kufanya usafi wa mazingira katika maeneo ya Mji;

*(ii)* Kulipa stahiki za wafanyakazi kwa wakati;

*(iii)* Kuimarisha bustani za mji ili kujenga haiba yake;

*(iv)* Kuyawezesha makundi maalum kujiimarisha kiuchumi.

**Changamoto za Baraza La Mji Mkoani**

Licha ya Baraza kufanikiwa katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi lakini bado kuna changamoto mbali mbali zinazolikabili katika kufanikisha shughuli hizo kwa asilimia mia moja, miongoni mwa Changamoto hizo ni pamoja na:

*(i)* Mwamko mdogo wa wafanyabiashara katika kufanya malipo ya ada na tozo kunapelekea kushuka kwa madairio ya mapato;
*(ii)* Ufinyu wa Ofisi ukilinganisha na wafanyakazi waliopo ambapo hulazimika kila chumba kutumiwa na wafanyakazi zaidi ya wawili;
*(iii)* Uhaba wa vitendea kazi kama vile vyombo vya usafiri na gari la kuzolea taka pia ni kikwazo katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza.
*(iv)* Upungufu wa wataalamu katika fani ya miundombinu ya ujenzi na ukusanyaji wa mapato.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

*(i)* Kamati inashauri Baraza kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato ili kuimarisha miradi yake inayotekeleza.
*(ii)* Kamati inalishauri Baraza kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza ufanisi wa makusanyo.
*(iii)* Kamati inalishauri Baraza kuongeza kasi ya usafi wa mji na mazingira yake.
*(iv)* Baraza pia liongeze juhudi katika kuwasajili wajasiriamali na kuwashawishi kulitumia zaidi soko jipya la wajasiriamali kama sehemu sahihi kwa biashara zao.

## 6.21 OFISI YA MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Mkoa wa Kaskazini Pemba umeanzishwa chini ya Sheria ya Tawala za Mikoa, nambari *8* ya mwaka *2014* na una majukumu ya kuratibu, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa sera, mipango na miongozo ya Serikali. Aidha, Mkoa unasimamia na kuratibu shughuli za ulinzi na usalama na kuhakikisha kuwa rasilimali watu na vitu vinatumika kwa maendeleo ya uchumi na jamii kwa ujumla.

Mkoa wa Kaskazini Pemba umeunganishwa na Wilaya Mbili (2), Wilaya ya Wete na Wilaya ya Micheweni pamoja na Wilaya ndogo ya Kojani. Mkoa pia, una Halmashauri mbili za miji ambazo ni

Halmashauri ya Micheweni na Baraza la Mji Wete. Aidha, Kamati inampongeza kwa dhati kabisa Mkuu wa Mkoa huu, Mhe. Salama Mbarouk Hatib kwa namna alivyojasiri na kusimamia maendeleo ya Mkoa huu.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Mkoa wa Kaskazini Pemba umefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

*(i)* Kuimarisha hali ya ulinzi na usalama wa Mkoa.

*(ii)* Kuimarika kwa kampeni ya mapambano dhidi ya udhalilishaji na ukatili ndani ya Mkoa.

*(iii)* Kuimarika kwa utoaji wa huduma za afya katika jamii.

*(iv)* Mkoa umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kusimamia miradi yake ya maendeleo na kuhakikisha imekamilika kwa wakati na kiwango kinachostahili.

*(v)* Mkoa umehakikisha kuendeleza mapambano dhidi ya makundi maovu yanayopelekea wizi wa mali, mazao na mifugo ya wananchi.

**Changamoto za Mkoa wa Kaskazini Pemba**

Katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Mkoa wa Kaskazini Pemba, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo:

*(a)* Ufinyu wa nafasi na uchakavu wa jengo la ofisi.
*(b)* Ufinyu wa Bajeti kutokana na mahitaji ya ofisi.
*(c)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri kama vile magari kwa ajili ya ufuatiliaji na utendaji wa ofisi.
*(d)* Kuwepo kwa kesi za wizi wa mifugo na mazao katika maeneo mbali mbali ya Mkoa.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

*(i)* Kamati inashauri Mkoa kuzidisha kasi ya kuzisimamia Halmashauri zake kuzidisha bidii ya kufanya usafi wa mazingira yake ili kujenga haiba ya miji.

*(ii)* Ofisi ya Mkoa izidishe kasi ya kupambana na vitendo vya wizi wa mali, mazao na mifugo katika jamii.

## 6.1 BARAZA LA MJI WETE

Baraza la Mji Wete ni miongoni mwa taasisi za Serikali za Mitaa ambapo Kamati katika kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali imefika na kuona majukumu yanayotekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sheria namba 7 mwaka 2014. Katika utekelezaji wa malengo ya Baraza kwa mwaka 2023/2024 utekelezaji wake umekuwa ukikua siku hadi siku kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Katika utekelezaji wa shughuli za Baraza la Mji Wete wamefanikiwa kwenye mambo mbali mbali ambayo Kamati inapongeza kwa hatua hizo kutokana na kukua kwake kiuchumi, miongoni mwa mafanikio yaliyofikiwa ni kama yafuatayo:

*(a)* Kuimarika kwa mfumo wa ukusanyaji wa mapato;
*(b)* Kuimarika kwa huduma za usafi wa mazingira katika mji;
*(c)* Kuyawezesha makundi maalum kuimarika kiuchumi na kijamii;
*(d)* Kukamilika kwa ujenzi wa miradi mbali mbali ya maendeleo ikiwemo mradi wa ujenzi wa soko la wajasiriamali la Kifumbikai.

**Changamoto za Baraza La Mji Wete**

Baraza la Mji Wete inakabiliwa na changamoto kadhaa katika utekelezaji wa majukumu yake, miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo:

*(i)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri katika shughuli za kiofisi pamoja na ukosefu wa gari la kukusanyia taka;
*(ii)* Upungufu wa wataalamu husuan katika sekta ya mapato na majenzi.
*(iii)* Kushuka kwa mapato kutokana na kupungua kwa vyanzo vya mapato pamoja na kutokuwepo kwa vyanzo vipya ambavyo vitasaidia kuongeza mapato.
*(iv)* Idadi ndogo ya wajasiriamali waliosajiliwa na kutambulika kihalali.
*(v)* Mwamko mdogo wa wananchi na wafanyabiashara kulitumia soko la wajasiriamali la Kifumbikai.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

*(i)* Kamati inashauri Serikali kuangalia kwa ukaribu umuhimu wa vyombo vya usafiri kwa Baraza ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

*(ii)* Kamati inashauri Baraza kufanya juhudi za makusudi katika kuibua vyanzo vipya vya mapato kwa kutumia wataalamu wake au kuomba kupatiwa wataalamu wa mapato ambao watasaidia kuimarisha hali ya mapato;

*(iii)* Baraza liongeze kasi ya kufanya usafi kwa maeneo yake ya wazi na kuwashirikisha wananchi katika program mbali mbali za usafi katika maeneo yao.

*(iv)* Baraza lisimamie wafanyabiashara wadogo wadogo na wale wa kati kulitumia soko la Kifumbikai kwa lengo la kuimarisha mapato yake na kutimiza malengo na azma ya Serikali.

## 6.2 HALMASHAURI WILAYA YA MICHEWENI

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ni miongoni mwa Serikali za Mitaa iliyopo katika Mkoa wa Kaskazini Pemba na imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sheria Nam. 7 mwaka 2014 kwa madhumuni ya kuanzisha Serikali za Mitaa, Zanzibar. Halmashauri hii imekuwa mstari wa mbele katika kusimamia huduma za kijamii na kuhakikisha suala la mapato na usafi wa mazingira yake imekuwa kipaumbele siku hadi siku.

**Mafanikio ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni**

*(a)* Halmashauri imefanikiwa kuibua na kusimamia utekelezaji wa miradi mipya ya Maendeleo;

*(b)* Halmashauri imeyawezesha makundi Maalumu kujiimarisha Kiuchumi na kijamii kwa kuwapatia mazingira bora ya kujikwamua na hali ngumu ya maisha;

*(c)* Halmashauri imeweza kuimarisha usafi wa mazingira katika maeneo mbali mbali ya miji;

*(d)* Kutoa elimu kwa jamii juu ya utunzaji, usafishaji na udhibiti wa mazingira na ulipaji wa ada na tozo kwa hiari.

*(e)* Kutoa elimu kwa Wajasiriamali juu ya umuhimu wa kujisajili na kupatiwa vitambulisho.

*(f)* Kamati inaipongeza Halmashauri kwa kufanikiwa kukamilisha mradi wa ujenzi wa kituo cha stendi ya daladala cha Kinoe.

**Changamoto za Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni**

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri.
*(ii)* Ukosefu wa magari ya kukusanyia taka katika miji na hoteli za kitalii.
*(iii)* Mwamko mdogo wa wananchi katika kulipa ada na tozo.
*(iv)* Wafanyabiashara waliowengi hawatumii mashine za risiti na hivyo kushindwa kutoa risiti kwa kufuata utaratibu husika.
*(v)* Uhaba wa vyanzo vya mapato na wataalamu wa sekta ya mapato.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni**

*(i)* Kamati inashauri Halmashauri kuendelea kutoa elimu ya ulipaji wa ada na tozo kwa wananchi ili kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato.
*(ii)* Kamati inashauri Halmashauri kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo vyake ili kusaidia ongezeko la miradi ya maendeleo.
*(iii)* Kamati inashauri Halmashauri kuendelea kuwasajili wajasiriamali na kuwapatia vitambulisho kwa lengo la kufahamu mahitaji yao.
*(iv)* Kamati pia, inaishauri Halmashauri kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mazingira Zanzibar kuweka na kusimamia utaratibu mzuri wa ukataji wa matofali kwa maeneo yote ya Micheweni na Vitongoji Pemba.

## 6.3 WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, Nam. *3* ya mwaka *2018*.

Ofisi ya Wakala inatekeleza majukumu yake kama Ofisi nyengine za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbali mbali ya Serikali kwa lengo la kutoa huduma bora na endelevu kwa jamii.

**Mafanikio ya Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar**

*(a)* Wakala imefanikiwa kuongeza kasi ya utoaji wa huduma katika Wilaya zote kwa kusajili na kutoa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, vyeti vya kuzaliwa, vifo, ndoa na talaka.

*(b)* Wakala imefanikiwa kufanya uboreshaji wa taarifa za wananchi katika mfumo wa usajili kutokana na mwamko mkubwa wa wananchi wa kupata huduma kwa njia rahisi.

*(c)* Wakala imefanikiwa kukusanya mapato stahiki yatokanayo na usajili wa matukio ya kijamii.

*(d)* Wakala imefanikiwa kuweka mfumo wa online (CRVS) katika uombaji wa vyeti vilivyopitwa na wakati, kukata rufaa, kufanya marekebisho ya vyeti vya vizazi hai na vifo pamoja na ndoa na talaka.

*(e)* Wakala pia, imeboresha mfumo wa *e-multi-Id* kwa vitambulisho vya wafanyakazi, wanafunzi na taasisi binafsi.

*(f)* Vile vile, Wakala wamefanikiwa kutoa vishkwambi (tablets) kwa Masheha kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma za vizazi na vifo kwenye shehia.

**Changamoto za Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar**

Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii katika utekelezaji wa majukumu yake imekuwa ikipambana na changamoto zifuatazo:

*(i)* Upungufu wa Wafanyakazi katika vituo mbali mbali hususan katika Wilaya ya Micheweni ambayo imeathirika zaidi katika utoaji wa huduma.

*(ii)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri katika vituo vya Wilaya na ofisi kuu Unguja.

*(iii)* Ufinyu wa ofisi kwa Wilaya ya Wete ambapo hupelekea utoaji usioridhisha wa huduma kwa wananchi, sambamba na kuwepo kwa uhaba wa vitendea kazi vya ofisi kama vile uhaba wa magamba ya kutolea vyeti kuzaliwa, magari na samani za ofisi.

*(iv)* Kuwepo kwa vitambulisho vingi ambavyo havijachukuliwa na Wananchi na hivyo kupelekea kuwepo kiwango kikubwa cha vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi katika ofisi za wakala.

*(v)* Mwamko mdogo wa wananchi kujisajili katika matukio ya ndoa na talaka.

*(vi)* Wananchi wengi kutosajili matukio ya vifo mpaka wanapohitaji vyeti kwa ajili ya matumizi ya mirathi, kuomba udhamini wa masomo ya elimu ya juu au mahitaji ya Serikali.

*(vii)* Bajeti ndogo ya Wakala na kuchelewa kupatiwa fedha za matumizi mengineyo kunaathiri mipango mikakati ya ofisi pamoja na kushindwa kulipa maslahi ya watendaji kwa wakati kama vile maposho ya likizo na malipo ya muda wa ziada.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Ofisi ya Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar**

*(i)* Kamati inaishauri jamii kuona umuhimu katika kusajili wa matukio mbali mbali ya kijamii kama sheria na taratibu zinavyoelekeza.

*(ii)* Kamati inaishauri Serikali kuzidi kuziboresha ofisi za usajili wa matukio ya kijamii kwenye Wilaya kwa kupatiwa vifaa na watendaji ili wananchi wapatiwe huduma za uhakika na kwa wakati.

*(iii)* Kamati inashauri Wakala kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa usajili ya matukio ya kijamii na kueleza faida na hasara zake kwa maendeleo ya nchi yetu.

*(iv)* Kamati inashauri Serikali kuboresha bajeti ya Wakala na kuwapatia fedha za matumizi kwa wakati ili waweze kununua magamba ya kutosha kwa ajili ya vyeti vya kuzaliwa.

*(v)* Sambamba na hayo, Kamati inaishauri Serikali katika bajeti ya mwaka 2024/2025 kuongeza fedha za matumizi mengineyo kwa Wakala ili kutatua changamoto zao kwa kuwepo rasilimali fedha.

*(vi)* Mwisho, Kamati inawashauri watendaji wa Wakala kufanyakazi kwa uadilifu, busara na mashirikiano ili kutoa huduma zenye ufanisi kwa maslahi ya wananchi na Serikali kwa ujumla.

## 6.4 AFISI YA MRAJISI WA JUMUIYA ZISIZO ZA KISERIKALI (NGO's)

Jumuiya zisizo za Kiserikali (NGO's) Zanzibar zimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Nam. 6 ya mwaka 1995 ya Jumiya zisizo za Kiserikali ambapo kazi, muundo na majukumu yake yameleezwa ndani ya sheria hiyo.

**Mafanikio ya Afisi ya Mrajis wa Jumiya**

Afisi ya Mrajisi wa Jumuiya zisizo za Kiserikali imefanikiwa katika kuzisaidia jumuiya zilizopo Unguja na Pemba kufanya kazi kwa weledi na kwa kufuata matakwa ya sheria za nchi. Aidha, afisi imekuwa ikifanya ukaguzi wa mara kwa mara katika jumuiya zake kwa lengo la kubaini uhai na changamoto zinazowakabili na kutafuta namna bora ya kuzitatua.

**Changamoto za Afisi ya Mrajisi wa Jumuiya zisizo za Kiserikali:**

*(i)* Jumuiya kushindwa kuwasilisha Ripoti zao kwa wakati kwa mujibu wa Kifungu cha 29 cha Sheria Nam. 6 ya Mwaka 1995 ya Jumuiya Zisizo za Kiserikali Zanzibar.

*(ii)* Kuwepo na taaluma ndogo ya matumizi ya mifumo ya Tehama ambapo imechangia kudumaza maendeleo ya Jumuiya nyingi za Unguja na Pemba hasa ukizingatia kuwa maombi ya Miradi na uwasilishaji wa Ripoti za mwaka za *NGO's* unaegemea katika matumizi ya Mifumo ya TEHAMA.

*(iii)* Kuwepo uhaba wa Wataalamu wa uandishi wa Miradi unaopelekea kushindwa kupata fedha za kutekeleza malengo yake waliyosajiliwa na baadhi yao kusita kufanya kazi kabisa.

*(iv)* Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la ufinyu wa Ofisi ya Mrajisi kwa upande wa ofisi zake za Unguja na Pemba.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Afisi ya Mrajisi wa Jumuiya Ziziso za Kiserikali Zanzibar:**

*(i)* Kamati inaishauri Afisi kuendelea kuzikumbusha NGO’s wajibu wa kutekeleza majukumu yao kwa kufuata Sheria ipasavyo na kuacha kufanya shughuli ambazo zinahatarisha usalama wa nchi.

*(ii)* Kamati inashauri Afisi ya Mrajis kuendelea kutoa taaluma kwa NGO’s ili ziweze kutekeleza vyema malengo waliyoainisha katika katiba zao.

*(iii)* Aidha, Kamati inashauri Afisi kushirikiana na Wadau wengine wa maendeleo ambao watasaidia kufanikisha kuzijengea uwezo Jumuiya zao.

*(iv)* Kamati inashauri Afisi kuendelea kufanya ukaguzi wa Jumuiya zake kwa lengo la kubaini uhai na ufuataji wa Sheria na kutambua mchango wao katika maendeleo ya Nchi. Aidha, Kamati inaigiza Afisi kuzichukulia hatua ya kuzifuta Jumuiya zote ambazo watabaini zinaenda kinyume na matakwa ya katiba yake kwa kutofuata sheria za nchi.

## SEHEMU YA TATU

## 7.0 MAONI , USHAURI NA MAPENDEKEZO YA JUMLA YA KAMATI

Katika sehemu hii, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inaeleza maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla pamoja na hitimisho la ripoti kwa afisi tano zilizo chini ya Kamati hii.

Kwa ujumla, Kamati imeridhishwa na utendaji wa Taasisi zote ambazo zinasimamiwa na Kamati hii kutokana na juhudi zao kubwa wanazozichukua katika utekelezaji wa majukumu yao kufuata muongozo na taratibu za kisheria.

Hivyo, mbali ya maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa kwa kila Sekta na kila Taasisi, Kamati pia inatoa maoni, ushauri na maelekezo ya jumla kwa Taasisi hizo kama ifuatavyo:

### Ofisi ya Rais Ikulu

*(a)* Kamati inatoa pongezi za dhati kabisa kwa Ofisi ya Rais Ikulu kutokana na mafanikio mbali mbali yaliyopatikana katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti yake kwa mwaka 2023/2024. Sambamba na utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020/2025. Aidha, Kamati imeridhika na namna Ofisi inavyosimamia Taasisi za Umma katika kutekeleza maaelekezo ya Serikali.

*(b)* Kamati inaipongeza Serikali kwa kujali na kuboresha maslahi ya wafanyakazi kupitia taasisi mbali mbali kwa lengo la kuwapunguzia ukali wa maisha. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuangalia zaidi maslahi ya watendaji wa Ikulu pamoja na Baraza la Mapinduzi kutokana na unyeti wa kazi wanazotekeleza kwani kwa muda mrefu maslahi yao hayajafanyia mapitio.

*(c)* Kamati inaishauri Serikali kupitia Taasisi ya Nyaraka na Kumbumbu za Taifa kuongeza mashirikiano na Taasisi za Umma na binafsi kwa lengo la kuimarisha mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu na kutunza historia ya Zanzibar. Aidha, Kamati inaishauri wakuu wa taasisi kutilia umuhimu suala la uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu kwa ajili ya matumizi ya baadae.

*(d)* Kamati inaipongeza Taasisi ya Nyaraka kwa kufanikiwa kununua nyumba za karibu na ofisi za Nyaraka Kilimani na hivyo kuweza kuongeza eneo la kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi mpya. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha taratibu wa ujenzi wa ofisi hii kutokana na kuwepo kwa changamoto mbali mbali katika jengo linalotumika kwa sasa.

*(e)* Kamati inashauri Ofisi ya Rais Ikulu kwa upande wa Pemba **kutafuta** eneo la kutosha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi mpya ya Nyaraka.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

(a) Kwa ujumla, Kamati imeridhika na utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais kwa kutekeleza vyema Mipangao, Sera na Miongozo ya Serikali kwa lengo la kutimiza wajibu wake. Kamati inampongeza kwa dhati kabisa Makamu wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Massoud Othman kwa namna anavyotekeleza majukumu yake na kuhakikisha Zanzibar imekuwa na maendeleo endelevu.

(b) Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Zanzibar ya Mwaka 2022 na 2023; Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya umuhali kwa wananchi katika kushirikiana na Mamlaka kutoa taarifa na ushahidi wa vitendo vya dawa za kulevya katika jamii. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuielimisha jamii umuhimu wa kutoa mashirikiano na taasisi husika kwa lengo la kufichua na kutoa taarifa za wahalifu wa dawa za kulevya bila muhali.

(c) Katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya; Kamati inasikitishwa kuona taasisi zenye kusimamia kesi za dawa za kulevya kuwaachia na kutowachukulia hatua stahiki wahalifu wa dawa kwa kisingizio cha ushahidi huru jambo ambalo linaifanya jamii kuiona Serikali inatoa fursa kwa wahalifu kuzidisha kasi ya uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya.

(d) Sambamba na hayo, Kamati inaishauri Mamlaka ya Dawa za Kulevya kuimarisha programu za kutoa elimu kwa jamii juu ya kujitambua kwa watoto, kuwajengea uwezo, kuwapa taaluma ya malezi bora na athari za dawa za kulevya katika maisha ya kila siku.

(e) Kamati inaishauri Serikali kutumia nguvu kubwa ya kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuwatunza na kuwalinda waathirika wa dawa za kulevya wakati wanapoacha kutumia dawa na kuwa wananchi wema katika jamii. Pamoja na hilo. Kamati inaitaka Serikali kutafuta uwezekano wa kujenga nyumba ya waraibu wa dawa za kulevya iliyo salama na kuachana na nyumba za kukodi ambazo zipo katikati ya makaazi ya watu kisiwani Pemba.

(f) Sambamba na hayo, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira kwa kufanikiwa kutekeleza vyema majukumu ya kusimamia na kutunza mazingira. Aidha, Kamati inashauri ZEMA kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya namna bora ya matumizi endelevu ya rasilimali zisizorejesheka.

(g) Kamati inashauri Mamlaka ya ZEMA kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira kuzidisha kasi ya mradi wa ujenzi wa tuta la kuzuia maji chumvi eneo la Sipwese katika Wilaya ya Mkoani na kuwashauri wahisani wa mradi huu kuongeza kasi ya maendeleo kwa mradi kabla ya mvua kubwa za masika.

(h) Kamati inaishauri Serikali kufikiria njia mbadala kwa wakaazi wa maeneo ya Micheweni ambao wamejikita katika shughuli za ukataji wa matofali na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira. Vile vile, Kamati inatoa wito kwa jamii kuyalinda mazingira yetu kwa kuepuka kufanya kazi ambazo zinaweza kusababisha majanga makubwa katika mazingira.

(i) Kamati pia, inaishauri Serikali kuongeza programu za kutoa elimu ya kujikinga na maradhi ya kuambukiza ikiwemo virusi vya VVU na UKIMWI, sambamba na kuongeza bajeti ya Tume hiyo ili kuepuka kufanya kazi kwa kutegemea wafadhili.

(j) Kamati inaipongeza Tume ya Ukimwi katika kuyadhibiti maradhi ya UKIMWI na kubaki chini ya asilimia moja kwa muda wa miaka 37. Hata hivyo, inapaswa kuongeza juhudi za kusimamia ushiriki wa sekta zote katika kupambana na maradhi ya UKIMWI pamoja na Serikali kulibeba jukumu la kuongeza matumizi ya fedha za ndani katika shughuli za kupambana na UKIMWI Zanzibar ili mafanikio haya yaweze kuleta tija.

(k) Kamati pia, inaishauri Serikali kuongeza programu za kutoa elimu ya kujikinga na maradhi ya kuambukiza ikiwemo VVU na UKIMWI, sambamba na hilo, kamati inashauri kuongeza bajeti ya Tume hiyo ili kuepuka kufanya kazi kwa kutegemea wafadhili.

(l) Kamati inaishauri Serikali kuzidisha kasi ya kuipatia msaada Idara ya Watu wenye Ulemavu Pemba kwa kuwajengea afisi yenye nafasi na kuwapatia vifaa na mazingira bora ambayo yatawezesha kutekeleza majukumu yao kwa urahisi na kupata maslahi yatakayosaidia kujenga maisha yao.

(m) Vile vile, Kamati inaishauri Serikali kuzidisha kasi ya kuipatia misaada Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu Pemba kwa kuwajengea Ofisi yenye nafasi na kuwapatia vifaa na mazingira bora ambayo yatawezesha kutekeleza majukumu yao kwa urahisi na kupata maslahi yatakayosaidia kujenga maisha yao.

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

(a) Kamati inaishauri Serikali kuzidisha kasi ya kufuatilia na kusimamia taasisi za umma katika kutoa huduma zilizobora na kuhakikisha kuwa miongozo na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inatekelezwa ipasavyo.

(b) Kamati inaishauri Serikali kuboresha ofisi ya Uratibu wa SMZ Dodoma na ile ofisi ndogo ya Dar es Salaam kwa kupatiwa nyenzo muhimu za utendaji pamoja na kuangaliwa suala la kuongezewa watendaji wenye uwezo wa kufanya kazi kwa uzalendo na kujitolea. Sambamba na hilo, Kamati inaomba Serikali kutatua changamoto ya usafiri kwa ofisi ya Dodoma kutokana na uhaba na uchakavu wa gari wanazotumia.

(c) Kamati inaishauri Serikali kuanzisha mfuko wa maafa ambao utaiwezesha Kamisheni ya Maafa kutekeleza shughuli zake kwa uhakika. Kamati imebaini Mfuko wa Maafa hauna fedha za kutosha na hivyo kuwepo kwa changamoto kadhaa ambazo kimsingi haziwezi kutatuliwa bila ya kuwepo kwa fedha za kutosha.

(d) Kamati imeridhika na maendeleo ya mradi wa TASAF kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini kwa namna jamii zilivyonufaika

kujikwamua na umasikini uliokithiri. Aidha, Serikali iwahamasishe wananchi kuilinda na uharibifu miradi inayotekelezwa pamoja na jamii kujitolea kutekeleza miradi inayoibuliwa vijijini.

(e) Kamati inashauri Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kushirikiana na wizara kuzidisha kasi ya kusimamia na kufuatilia haki na fursa za watendaji wa Baraza katika kuboresha maslahi na mafunzo ili kufanya kazi kwa weledi na ufanisi.

(f) Vile vile, Kamati inashauri Serikali kuharakisha mpango kuwa kupatiwa gari kwa ajili ya shughuli za Kamati za Baraza kwani mpango huu ulipangwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 ambapo hadi kamati inawasilisha ripoti hii hakuna muelekeo wa suala hili.

(g) Kwa upande mwengine, Kamati inashauri Tume ya Uchaguzi Zanzibar kuharakisha mradi wa ujenzi wa afisi za Wilaya kwani baadhi ya Wilaya tayari zimepata viwanja kwa ajili ya ujenzi. Aidha, Serikali ni vyema kuongeza nguvu ya Tume kwa kuwapatia watendaji wa kutosha katika afisi za Wilaya kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi.

**Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora**

(a) Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa Ofisi hii kwa kusimamia vyema majukumu yake na kutoa miongozo kila inapostahiki juu ya masuala ya sheria na utumishi. Kamati inashauri Ofisi kufuatilia zaidi utendaji wa Tume za Utumishi na kuzishauri kufuatilia na kusimamia watumishi wao katika kutoa huduma bora kwa jamii.

(b) Kwa upande mwengine, Kamati imeridhishwa na utendaji wa Taasisi za Dini katika kujenga amani kwa waumini wa Dini zote pamoja na kuhakikisha amani na utulivu wa nchi yetu umelindwa kwa misingi ya Dini. Aidha, Kamati inaipongeza Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar katika utekelezaji wa majukumu yake na kuhakikisha migogoro ya Dini imepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na hatua mbali mbali zinazochukuliwa katika kukabiliana na changamoto za waumini. Hata hivyo, Kamati inaishauri Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar isichoke kuchukua hatua na kutoa miongozo ya kidini wakati wote wanapoona inafaa kufanya hivyo.

(c) Katika kujenga misingi bora ya Haki na mustakbali uliobora katika nchi yetu, Kamati inaishauri Serikali kuzitumia Taasisi za kusimamia Haki Jinai kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na uwezo wake wa kuendesha kesi za udhalilishaji katika jamii na athari za kuacha kutumia sheria katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

(d) Kwa upande wa Sekta ya Utumishi wa Umma, Kamati inashauri kuchukuliwa hatua za haraka changamoto ya upotevu wa Majalada au baadhi ya taarifa muhimu kwa baadhi ya wastaafu waliotumikia utumishi wao zaidi ya Taasisi moja katika Serikali na kukosekana kwa baadhi ya vielelezo muhimu katika majalada ya wastaafu mfano; mikataba, aridhilhali, barua za vizuizi vya mishahara vithibitisho vya kifo, barua za bodi ya madaktari nakadhalika.

(e) Kamati inasikitishwa na kitendo cha ujazaji usioridhisha wa taarifa za mishahara katika kalamazuu na kupelekea kukosekana kwa usahihi wa taarifa za hesabu za mafao kwa baadhi ya wastaafu. Kamati inashauri taasisi inayohusika kufanya ukaguzi wa suala hili kufuatilia kwa kina kuona chanzo cha changamoto hii ili taasisi zitakazobainika kuchukuliwa hatua za msaada.

(f) Sote tunaelewa kwamba jukumu la msingi la Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni kusimamia Maadili ya Viongozi wa Umma kama Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma inavyoelekeza. jukumu hili la kusimamia Maadili ya Viongozi wa Umma si la Tume peke yake bali ni la wananchi na viongozi wote kwa ujumla. Kwa msingi huo, kamati inashauri kuwa mafaniko haya ya utekelezaji wa majukumu ya Tume yanahitaji kupata ushirikiano kutoka kwa wananchi, viongozi, sekta binafsi, jumuiya za kiraia na kidini pamoja na vyombo vya habari.

(g) Kamati pia inaipongeza Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa kwa lengo la upatikanaji wa haki za jinai wenye kuleta amani, utulivu na maendeleo ya kiuchumi. Ili kukamilisha malengo hayo hakuna budi kuwepo kwa upatikinaji kamili wa makadirio ya matumizi iliyojiwekea sambamba na jamii kutoa ushirikiano wa kutosha katika kutoa ushahidi pale itakapo hitajika. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kwa ujumla kuwaongezea taasisi za Serikali fedha za matumizi mengineyo ili ziweze kuwajibika ipasavyo.

(h) Kwakuwa Ujenzi wa jengo la Chuo cha Utawala wa Umma Tawi la Pemba unatarajiwa kuanza mwaka huu wa fedha 2023/2024. Na imeelezwa Chuo kilipanga bajeti ya milioni 500 kwa ajili ya ujenzi huo kwa mujibu wa mahitaji ya awali, hatahivyo kutokana na mabadiliko ya mahitaji halisi bajeti iliyotengwa haitotosha hivyo Kamati inaishauri Serikali kuongeza nguvu ya Kukisimamia Chuo hicho kwa kufanya mazungumzo na baadhi ya mabenki ili kuona kwa jinsi gani yataweza kuwajengea ili waweze kulipa baadae kwa mujibu wa tutakavyokubaliana.

(i) Kwa upande wa Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Kamati inaipongeza kwa kuweza kupiga hatua kwa kiasi kikubwa kwa kutekeleza majukumu yake kutokana na Ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Serikalini kupitia Taasisi mbali mbali za Serikali.

(j) Mwisho, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa Ofisi hii kwa kusimamia vyema majukumu yake na kutoa miongozo kila inapostahiki juu ya masuala ya sheria na utumishi.

**Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ**

*(a)* Kamati inaishauri Serikali kusimamia zoezi la ujenzi wa ofisi za Masheha kwenda kwa haraka ili kuweza kukamilika kabla ya uchaguzi wa mwaka 2025 kwa kuzingatia zaidi kuwa shehia nyingi zimeshapata viwanja na mkandarasi wa ujenzi ameshapatikana;

*(b)* Kamati inaishauri Serikali kuziagiza Mamlaka zinazohusika na kutoa mgawanyo wa fedha za maliasili na kuzipatia Mamlaka za Serikali za Mitaa fedha hizo kwa wakati na kuzitumia katika mipango yao ya bajeti;

*(c)* Kamati inashauri Serikali kuaandaa programu maalumu ya kutoa elimu kwa wafanyabiashara wadogo wadogo katika kuendeleza na kukuza biashara zao kwa kila Halmashauri za Unguja na Pemba;

*(d)* Kamati inaishauri Serikali kuzidisha kasi ya usimamizi kwa Serikali za Mitaa kuhakikisha wanatekeleza vyema jukumu la usafi katika maeneo yao. Kamati inazitaka Halmashauri na Mabaraza kutoa fursa kwa

kampuni za ndani na nje kuwekeza katika ukusanyaji wa taka kwa lengo kuongeza kasi ya usafi wa miji;

*(e)* Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuhakikisha kuwa wapiganaji na watendaji wote wa Vikosi vya SMZ wanalipwa stahiki zao za likizo pamoja na fedha za muda wa ziada (over time) kwa mujibu wa sheria na miongozo ya kiutumishi;

*(f)* Kamati inashauri Serikali kuupitia upya mkataba wa ushirikiano baina ya Serikali ya Misri na SMZ na kuangalia maslahi ya nchi kupitia JKU kwani mkataba huu umeisha muda wake na haujawahi kufanyiwa mapitio. Sambamba na hilo, Kamati inapata mashaka kuwa mkataba huu haukuzingatia maslahi ya JKU;

*(g)* Kamati haijaridhishwa na biashara ya uzalishaji na uuzaji wa miwa kwa Kikosi JKU na Chuo cha Mafunzo Zanzibar katika kambi mbali mbali. Hivyo, tunaiomba Serikali kuangalia upya makubaliano kati ya mnunuzi na muuzaji kwa manufaa ya pande zote mbili;

*(h)* Kamati inaishauri Serikali kuunganisha nguvu za Idara Maalumu katika kupiga vita matukio ya kihalifu katika jamii kwa kufanya doria za kila siku katika maeneo yanayoashiria uvunjifu wa amani na usalama wa raia;

*(i)* Sambamba na hayo, Kamati pia inaishauri Serikali kuweka fungu maalum la mafuta kwa vyombo vya KMKM, KZU na KVZ katika kuendeleza doria za baharini na nchi kavu kutokana na misingi ya kazi zao kwa kupambana na matukio ya kihalifu;

*(j)* Kamati inaishauri Serikali kusimamia ukamilishaji wa miradi ya ujenzi wa nyumba za maafisa na mahanga ya askari wa KMKM Fundo na Kisiwa Panza kutokana na kutelekezwa kwa mradi huu licha fedha nyingi za umma kutumika bila kufikia malengo;

*(k)* Kamati inaishauri Serikali kuzidisha kasi ya kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kujisajili katika matukio ya kijamii, sambamba na kuchukua vitambulisho au vyeti kwa wakati kwa wale wananchi wanaojisajili; na

*(l)* Kamati inazitaka Taasisi zisizo za Kiserikali kuongeza juhudi katika kutekeleza majukumu yao na kuhakikisha hawaendi nje ya malengo ya jumuiya husika. Aidha, serikali isichoke kuchukua hatua kwa jumuiya yoyote yenye kwenda kinyume na malengo ya katiba zao.

## 8.0 HITIMISHO

Katika kukamilisha kazi hii, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa haina budi kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kusimamia vyema sera na mipango ya Serikali katika utekelezaji wa shughuli zake za kuwaletea wananchi maendeleo ambao ni msingi wake ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Kwa upande mwengine, Kamati inatoa shukurani za dhati kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar; Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar; ndugu Raya Issa Msellem, Mratibu wa Kamati za Baraza ndugu, Khamis Hamad Haji, Mkuu wa Idara ya Uratibu wa Baraza la Wawakilishi Pemba; ndugu Abdulghani Abdallah Said pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa msaada wao ambao umekuwa ni chachu ya mafanikio kwa Kamati.

===========xxx============